Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Kumi na Moja - Tarehe 23 Juni, 2009**

*(Mkutano ulianza saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika* (M*he. Anne S. Makinda*) *Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 85

**Matatizo Yanayovikabili Vituo vya Afya Iramba Magharibi**

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH** aliuliza:-

Kwa kuwa, Hospitali ya Iramba iko umbali wa Km.21 kutoka barabara kuu iendayo Dar es Salaam; na kwa kuwa, idadi kubwa ya wananchi wanaoishi kwenye maeneo ya Shelui, Ndago, Ulemo, Masigiri, Kinampanda, Iguguno na Nduguti wanashindwa kupata huduma kwenye vituo vya afya vilivyoko kwenye maeneo hayo kwa sababu vinakabiliwa na matatizo kama upungufu wa Ikama ya Wafanyakazi, vitendea kazi na dawa; na kwa kuwa, kutokana na hali ya jiografia ya Wilaya ya Iramba, mara nyingi wananchi wa maeneo yaliyotajwa hulazimika kwenda kutafuta huduma nje ya Wilaya, kama vile Hydom, Igunga, Singida na kadhalika.

(a) Je, Serikali iko tayari kurekebisha upungufu uliopo kwenye vituo vya afya vya Mgongo (Shelui), Ndago, Mkalama na kadhalika, ili viweze kutoa huduma zinazotakiwa na kuwaondolea wananchi adha na usumbufu wa kufuata huduma nje ya Wilaya ambako huchelewa kupata huduma, gharama kubwa na wakati mwingine kupoteza maisha?

(b) Kwa kuwa, Hospitali ya Wilaya ilijengwa mwaka 1943 na hakuna ukarabati wowote uliokwishafanywa tangu wakati huo mbali na kupaka rangi; na kwa kuwa, idadi ya watu imeongezeka na maeneo mbalimbali ya hospitali ni mabovu kama vile chumba cha kuhifadhia maiti, jiko, mahali pa kufulia nguo, eneo la kupumzikia ndugu wa wagonjwa na kadhalika. Je, Serikali ipo tayari kufanya marekebisho (ukarabati) katika Hospitali ya Wilaya ili kuboresha huduma?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Kilimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Iramba ina tarafa saba (7) na kati ya hizo, ni Tarafa 4 ndizo zina vituo vya afya ambavyo ni, Ndagu, Shelui, Kingangiri na Mkalama. Tarafa ambazo hazina vituo vya afya ni Nduguti, Kinampanda na Kisisiri. Hata hivyo, Tarafa za Kinampanda na Kisisiri zinaizunguka hospitali ya Wilaya. Hali ya majengo katika vituo hivi ni nzuri, na kuna huduma ya magari ya wagonjwa na mawasiliano ya simu za upepo (*radio calls*). Mpango mpya wa uagizaji wa dawa (*Intergrated Logistic System*) unatumika na unasaidia vituo kuwa na dawa za kutosheleza kwa muda mrefu kulingana na mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, lipo tatizo la upungufu wa wataalam wa kada ya Afya. Aidha, hilo ni la nchi nzima na ni kubwa zaidi katika maeneo yenye jiografia kama ya Iramba.

Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, imekuwa ikihakikisha kuwa, watumishi wa kada mbalimbali za afya wanapangiwa kazi katika Halmashauri hii ambao wengi wao wamekuwa hawaripoti kama ilivyotarajiwa.

Ili kupunguza ukali wa tatizo la watumishi wengi kutopenda kufanya kazi katika baadhi ya maeneo hapa nchini, kuanzia mwaka wa fedha 2009/2010, Serikali itaanzisha utaratibu ambao utatoa vivutio kwa watumishi wa maeneo haya.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Wilaya ya Iramba, ilijengwa mwaka 1933 na Wamisionari wa Kilutheri kutoka Amerika na siyo mwaka 1943. Hospitali hii ikakabidhiwa Serikalini mwaka 1967 baada ya kufanyiwa upanuzi. Mwaka 1997 Serikali ilifanya ukarabati mkubwa wa ndani ukihusisha dari, madirisha, milango, kupaka rangi na kurekebisha mfumo wa umeme. Hata hivyo, ukarabati huu haukuhusisha paa na mfumo wa maji safi na maji taka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 10 Februari, 2009, Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, ilituma maombi maalum ya shilingi Milioni 702 Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala

za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa barua yenye Kumbukumbu Na. KH/B.10/2/277 na kunakilisha Wizara ya Afya na vidadisi bei vya makisio ya gharama ya ukarabati wa Hospitali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na maombi haya, Halmashauri inatarajia kupata shilingi milioni 400 katika mwaka wa fedha wa 2009/2010. Aidha, Halmashauri ya Wilaya imetenga shilingi milioni 12 kwa madhumuni hayo. Fedha hizo zikipatikana zitaendeleza ukarabati wa hospitali ili kuboresha huduma zinazohitajika.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kipengele (a) ameeleza juu ya kwamba, bahati nzuri kwamba vituo vya afya nilivyovitaja mimi na yeye kavitaja kwamba, vina *ambulance* lakini mwaka 2006 ndani ya Bunge hili Tukufu 2007, kwa mfululizo nimewahi kueleza tatizo la juu ya *ambulances* hizo kutokwenda kwenye vituo vya afya vilivyo tajwa na vipo katika eneo la Wilaya, na Mheshimiwa Waziri, wakati huo akiwa Naibu Waziri wa Wizara hii aliahidi atashughulikia hilo tatizo, sasa aniambie kwamba, mpaka sasa hivi *ambulances* hizo hazipo na ziko makao makuu ya Wilaya, wanalichukuliaje hilo tatizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Nashukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri ameelza na ameiongeza umri hospitali yetu, amesema ya mwaka 1933, hilo nashukuru, sasa nataka niwaleze kitu kimoja. Hiyo *mortuary* ninayoizungumza inahifadhi maiti watatu mpaka hivi sasa, nilichokuwa nataka niombe, naiomba Serikali na hasa kupitia Wizara ya TAMISEMI mpanue hiyo *mortuary* kwa sababu hali ya sasa hivi ongezeko la watu limekuwa kubwa tofauti na mwaka 1933.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kilimbah uliza swali sasa ukipiga hotuba hapa itakuwa ngumu.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, ninachotaka hapa naiomba serikali ipo tayari sasa kuipanua hiyo *mortuary* kwa ajili ya kuweza kuhifadhi maiti zaidi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kilimbah kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mimi nafurahi kwamba, Mheshimiwa Mbunge anakiri kwamba, *ambulances* zimepelekwa lakini zimepelekwa katika Halmashauri ya Wiala ya Iramba. Kwa kawaida sisi kama Wizara, hatuendi tena kwenye vituo na kuanza kuwapangia kwamba peleka kituo hiki, peleka kijiji kile, kazi yetu sisi tunapeleka pale

kwenye Halmashauri ya Wilaya kwa sababu ndipo panapotambulika kama eneo la mipango ya Halmashauri ya Wilaya.

Kwa hiyo, ninachoomba hapa ni kwamba Mheshimiwa Kilimbah ashirikiane na wenzake pale waone jinsi ambavyo wanaweza wakafanya hizo *arangements* ili kuweza kupeleka katika yale maeneo ambayo kwa kweli mimi nakubaliana naye kwamba, ni muhimu kama yatapelekewa huduma hiyo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumza suala la upanuzi wa *mortuary* hapa na upanuzi wa *mortuary* maana yake ni kwamba, tunatakiwa tuwe na hela. Nimezungumza humu ndani nimesema kwamba, katika Bajeti ya mwaka 2009/2010 tumetenga shilingi Milioni 400 kwa ajili ya shughuli mbalimbali zitakazokuwapo pale. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sasa ni suala la kwenda kuangalia vile vipaumbele na kama anavyosema Mheshimiwa Kilimbah kwamba, anaona *Mortuary* ni muhimu *then* itatakiwa Halmashauri sasa iweke katika *items* zake kuonyesha kwamba, ni muhimu ili tuweze kusaidiana nayo. Lakini nataka nikiri hapa kwamba, tutaendelea kushirikiana naye kusaidia tatizo hili liweze kuondoka.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali la nyongeza. Kwa kuwa, Wizara ya Afya ina mpango mzuri wa kuanzisha kada ya *Clinical Assistant* (Tabibu Msaidizi) na watapata mafunzo ya miaka miwili badala ya miaka mitatu, ili kupunguza upungufu wa waganga katika zahanati zetu na vituo vya afya.

Je, Mpango huo utaanza lini? Hayo mafunzo yataanza lini? Naomba maelezo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa George M. Lubeleje, kama ifuatavyo;-

Mheshimiwa Naibu Spika, huo mpango umeanza na tunategemea wahitimu wa kwanza watatoka mwaka kesho. Ahsante.

Na. 86

**Upatikanaji wa Namba na Hati kwa Vijiji vilivyopimwa**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA (K.n.y MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA**) aliuliza:-

Kwa kuwa, Vijiji vya Maleza (Kata ya Mbagala) na Ndaga (Kata ya Mbuyuni) vilivyoko kwenye Jimbo la Songwe vilikwishapimwa na kuandikishwa kwa muda mrefu sasa lakini havijapatiwa namba na Hati zao:-

(a) Je, ni lini Vijiji hivyo vitapatiwa Namba na Hati?
(b) Kama kazi ya kuvipatia namba vijiji hivyo itaendelea kuchukua muda mrefu. Je, isingekuwa vyema vijiji hivyo vikaingizwa kwenye utaratibu wa kupatiwa ruzuku?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Guido Gorogolio Sigonda, Mbunge wa Songwe lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kijiji cha Maleza kilichopo katika Kata ya Mbagala, kimeandikishwa baada ya kutimiza vigezo vyote. Hata hivyo, Kijiji hicho hakikupatiwa Hati ya kuandikisha Vijiji rasmi. Kutokana na kuwepo kwa maombi mengine yaliyokuwa yanachambuliwa ili uandikishaji wa Vijiji vyote vitakavyokuwa vimetimiza vigezo viweze kupatiwa Namba na Hati za kuandikishwa kwa pamoja. Kijiji cha Maleza ni miongoni mwa Vijiji vitakavyopatiwa Hati na Namba baada ya kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali *(GN)* linaloandaliwa kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Kuhusu kijiji cha Ndanga naomba kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge kuwa, Ndanga ni kitongoji katika kijiji cha Mbuyuni, Kata ya Mbuyuni, ambacho kiliwasilishwa na Halmashauri ya Wilaya katika maombi ya 16 ya kutaka kipandishwe hadhi ya kuwa kijiji kamili. Hata hivyo, uchambuzi uliofanywa na wataalam, ulibaini kuwa hakikidhi vigezo na hivyo hakikuwekwa kwenye mapendekezo ya kuwa kijiji kamili.

(b)Utaratibu wa kutoa ruzuku, unavihusu Vijiji vyote vilivyosajiliwa na Halmashauri ya Wilaya husika.Kijiji kipya cha Maleza, kinapata ruzuku, kama Vijiji vingine vyote vilivyomo katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ambavyo vimeandikishwa.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kumwuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika zoezi la Serikali mwaka jana na mwaka juzi la kupima Vijiji, katika Kijiji cha Lwalaje, Kata ya Lwalaje imeonekana kwamba mpaka ambao ni Mto Lwalaje, umepita katikati ya Kijiji, ambapo sehemu ya Kijiji iko Wilaya ya Mbarali, sehemu nyingine ya Kijiji iko Wilaya ya Chunya.

Hiyo sehemu ambayo iko Wilaya ya Mbarali, ndiyo kuna miundombinu ya kudumu kama Ofisi za Kijiji na Makanisa na vitu vingine.

Je, serikali iko tayari kurekebisha mpaka huo ili miundombinu hii iwe ndani ya Kijiji?

**NAIBU SPIKA:** Hili swali ni kweli lakini Lwalage huyu hakuajiandaa na Lwalage, alijiandaa na Ndauga. Haya Naibu Waziri jibu kama unaweza.*(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuiona *dilema* ambayo nilikuwa naipata. Lakini pamoja na hayo kwa niaba ya Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la nyongeza la rafiki yangu Mheshimiwa Mwambalaswa, kama ifuatavyo.

Mimi nimechukua hizi takwimu na hili Lwalaje, Kata ya Lwalaje na kwamba, kuna mto umepita pale, nitaomba tu Naibu Spika, uruhusu halafu tuangalie wote kwa pamoja, halafu nitawaita na wataalam wetu ili tuweze kuliangalia kwa pamoja tuweze kulipatia ufumbuzi.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa fursa, niweze kuuliza swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa zoezi la kuandikisha Vijiji, kuvipa Namba na Hati ni zoezi muhimu sana, pamekuwa na maombi mengi ya vitongoji kupandishwa kuwa vijiji, na baadhi ya vijiji kadhaa kutengeneza Kata Mpya, tarafa na kadhalika.

Tulitarajia kwamba, kwa hotuba ya jana ya Mheshimiwa Waziri Mkuu,ingetoka orodha ya vitongoji ambavyo vimekubaliwa kuwa Vijiji, na Vijiji kuwa Kataa, lakini orodha hiyo haijatoka na Bajeti ndiyo hii na uchaguzi wa Vitongoji na Vijiji, ni Oktoba keshokutwa; Mheshimiwa Waziri, analiambia nini Bunge lako, ndiyo basi tena hilo zoezi, maanake sasa kwenye bajeti haipo? Naomba majibu.( *Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Jana alisoma hotuba Waziri wa nchi TAMISEMI, sasa ajibu swali hilo. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ndugai, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema kwenye hotuba yangu ya jana kwamba, zoezi hili limekamlika, sasa hivi Vijiji na Vitongoji viko kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, na ukiangalia kwenye Jedwali linaonyesha tu kwamba, kila Wilaya, Vijiji vingapi vimepitishwa na Mitaa mingapi Imepitishwa. Lakini orodha kamili na *GN* ya Serikali, tutawapatia kabla ya Bunge hili halijamalizika.

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa baada ya kugawa Wilaya ya Dodoma Vijijini kuwa Wilaya ya Bahi na Chamwino, ilizaliwa Tarafa ambayo mpaka

sasa haijawa *gazzeted* nayo ni Tarafa ya Muhayungu, nimekuwa nikifuatilia jambo hili kwa siku nyingi sana sasa karibu ni mwaka wa tatu.

Je, Serikali inasema nini juu ya ku-*gazzete* hii Tarafa mpya ili iweze kuendeshwa kama Tarafa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa, Mzee Malecela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipokee hii taarifa na kwa vile amekuwa anaifuatilia nitawasliana naye ili tuweze kupata hizi kumbukumbu zote na tuweze kulishughulikia kama anavyotaka.

Na. 87

**Fedha za Mfuko wa Kuwezesha Wajasiriamali**

**MHE. JAMES P .MUSALIKA (K.n.y. MHE. ERNEST G. MABINA**) aliuliza:-

Kwa kuwa, Fedha za Mfuko wa J.K. kwa Geita zimefikia kwenye *SACCOS* mbili tu za Geita na Kaseme *SACCOS n*a zote zipo miji tofauti na madokezo kwamba, fedha hizo zimewafikia watu wa chini:-

(a)Je, fedha hizo zitawafikia lini Wananchi Vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina, Mbunge wa Geita, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba, wakati wa utoaji fedha za mikopo ya mpango wa Uwezeshaji Wananchi kiuchumi wa shilingi Bilioni 21, Wilaya ya Geita ilipata jumla ya shilingi 573,245,000/= zaidi ya kiwango kilichotengwa kwa kila Wilaya, cha shilingi 200 milioni. Fedha hizi zilitolewa kwa *SACCOS* mbili tu za Geita na Kaseme zilizopo mjini Geita.

Ni kweli pia kwamba, wananchi wa Geita vijijini hawakuweza kupata mikopo ya fedha za uwezeshaji Wananchi kutokana na kukosekana kwa huduma ya Benki Vijijini kwa Benki za CRDB na NMB zilizokuwa na jukumu la kutoa awamu ya kwanza ya mpango huo. Aidha, Benki hizo hazina uwezo wa kutoa huduma zaidi ya umbali wa kilomita 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, Napenda kuchukua nafasi hii kumfahamisha Mheshimiwa Mabina, Mbunge wa Geita kwamba, utaratibu unaotumika kuanzia awamu ya pili ni kushirikisha pia Benki na Asasi za fedha zenye mtandao wa kutoa huduma kwa wananchi waliopo vijijini.

Aidha napenda kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge, kuwa mpango huu ni endelevu hivyo, wananchi waliokosa mikopo katika Vijiji vya Geita, wataweza kupata mikopo hiyo baada tu ya wenzao kurejesha mikopo iliyochukuliwa awali.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Jana imetangazwa bei ya Pamba, shilingi 360 kwa kilo, wananchi wanalalamika Serikali iongeze iwe shilingi 400 baada ya hayo naomba kuuliza kama ifuatavyo;-

Kwa kuwa swali hili la pesa za wajasiriamali limekuwa likiulizwa pia na mimi na kwamba Serikali imeishawahi kutoa majibu tofauti ikiwemo kwamba, Asasi inatafutwa ya kwenda mpaka Nyang’wale, ambapo zimekwishatengwa Milioni 100, mara pesa hii itapalekwa kwenye Halmashauri na inaonyesha majibu tofauti tofauti si kawaida ya Serikali; inamaanisha kwamba, majibu yanayotolewa siyo ya serikali, ni ya waziri mwenyewe. Je, anaweza kujibu kama Serikali, pesa zitakwenda lini sasa? Ajibu kama Serikali sasa. (*Makofi/kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwenye Bajeti ya Kilimo. Kilimo kimetengewa ziada ya asilimia 30 sawa na Bilioni 666.9.

Je, Serikali sasa haiko tayari kujipanga vizuri ili wananchi hawa Vijijini ambao tayari wanaweza wakalima Pamba, Mahindi, Mpunga wanahitaji pesa za JK za Wajasiriamali hawajazipata. Je, hizi za Bajeti bilioni 666 Serikali inaweza kujipanga vizuri ziwafikie wakopeshwe walime pamba waongeze pato la Taifa la mahindi na Mpunga, Serikali inaweza kufanya hivyo kwenye Bajeti hii? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge wa Nyangw’ale, kama ifuatavyo:-

Kwanza kuhusu suala la fedha kwenda katika jimbo la Nyangw’ale. Kama tulivyojibu mara ya mwisho, baada ya wataalamu kushauriana, Wizara ya fedha na Benki Kuu, ilionekana kwamba, kwa sababu fedha hizi zinakwenda kiwilaya na siyo kijimbo na kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, fedha zilizokwenda Wilaya ya Geita, kwa ujumla ni mara mbili ya ambazo zilikwenda wilaya nyingine nyingi. Sasa ni utaratibu tu wa kuhamasishana ni *SACCOS* zipi, ndiyo maana kwa kweli *SACCOS* au wajasiriliamali katika jimbo la Nyang’wale hawakupata na siyo Nyang’wale tu, hata kwenye majimbo mengine tumeona kwamba ni *SACCOS* mbili tu pale Geita ziliweza kupata.

Ningeshauri kwamba kwa kweli tuwe waangalifu kwenye awamu zinazokuja hasa katika kuhamasishana na kuona kwamba, fedha zile zifike vijijini kama alivyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii vilevile inahusisha hilo suala la Kilimo. Tutajipanga hasa tunapojaribu kufanya tathimini ya mpango huu kabla mpango haujaendelea mwaka huu wa fedha tuone namna gani tutaelekeza fedha hizi vijijini zaidi ili kufaidisha watu wengi na kuondoa kasoro ambazo zimejitokeza kama tulivyoona kule Geita. (*Makofi*)

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kuniona. Naomba kumuuliza, kwa kuwa, ngazi ya Kata ni ngazi muhimu sana katika kuleta maendeleo katika Taifa letu, na kwa kuwa katika jibu lake la msingi amesema kwamba, zilikwenda katika ngazi ya Wilaya na siyo maeneo mengi yaliyopata hela hizo na kwa kuwa tatizo hilo halikujitokeza tu Geita, ila liko pia katika Mkoa wangu wa Kilimanjaro na katika wilaya zote. Je, Serikali iko tayari sasa kuelekeza hela hizo ziende katika ngazi ya Kata?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shally Raymond, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema sisi tulipopeleka fedha kiwilaya ilikuwa ni jukumu la Asasi za kifedha ambazo zilikuwa zinatoa fedha zile kwa mfano, *CRDB* na *NMB* na Halmashauri ile kuweza kuhamasisha wajasiriamali na *SACCOS* zote zilizoko kwenye ngazi za Kata, kwa sababu wilaya haiwezi kuwa Wilaya kama haina Kata. Kwa hiyo, maana yangu haikuwa kuwa sasa zilitumika tu pale Makao Makuu ya Wilaya, maana yangu ni kwamba zilipelekwa Makao Makuu ya Wilaya, lakini uhamasishaji ulitakiwa ufanyike mpaka huko vijijini kwenye Kata mbalimbali na viongozi wa Wilaya.

Tunakiri kwamba, tumeona kasoro zilizojitokeza na tutarekebisha kwenye awamu zinazokuja za mpango huu ili tuone kwamba, hizi Asasi tunazozipa pesa zisione tu kwamba, yeyote anayekuja mradi yupo pale mjini kwa haraka watoe mikopo bila kuangalia wale wa vijijini wanapata fedha na wenyewe.

**MHE. MOHAMEDI H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa, mara nyingi tumeeleza hapa Bungeni humu kwamba, fedha hizi za Mheshimiwa JK, ambazo zimetolewa kwa ajili ya kuwasaidia wananchi, kwa kweli waliofaidika zaidi ni watu wa mijini, watu wa vijijini ambao ndiyo asilimia kubwa ya wananchi wa Tanzania, hawajafaidika na wengine hata hawajazisikia hizi fedha. Hivi serikali ina mkakati gani wa makusudi wa kuhakikisha kwamba, wananchi wa vijijini ambao ndiyo masikini zaidi kulikoni huko mijini, wanafaidi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Missanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hili tumeanza kulirekebisha katika awamu ya pili kwa kuhakikisha kwamba, fedha hizi sasa zinapitia kwenye zile asasi za kifedha ambazo zina mtandao mpaka vijijini badala tu ya kutumia *CRDB* na *NMB* ambao kwa kweli tuliona katika awamu ya kwanza walizingatia zaidi watu wa mijini. Tunaamini kabisa kwamba, hizi Asasi ndogondogo ambazo kwa kawaida huwa zinakwenda mpaka vijijini, zitafanya kazi nzuri zaidi. Nia yetu ni kwamba, awamu nyingine kama itakuja basi tutazingatia hilo kuendelea kutumia hizi Asasi ndogondogo zinazokwenda huko vijijini, na ikiwezekana hata zile Asasi kubwa ambazo ziko vijijini, tuzipelekee hela moja kwa moja badala ya kupitia kwenye Asasi kubwa za kifedha.

Na. 88

**Uharamia wa Sanaa Nchini**

**MHE. MARTHA M. MLATA** aliuliza:-

Kwa kuwa uharamia wa kazi za Muziki na Sanaa Tanzania ulianza kutokana na kuingia kwa Teknolojia ya Kanda na kaseti nchini miaka ya 1980 na kufuatiwa na utengenezaji wa muziki katika *CD*, *VCD* na *DVD*; na kwa kuwa, biashara hii ilianzishwa hapa Tanzania na makampuni ya nje ambayo yalihamisha shughuli zao hapa nchini, kwani hakukuwa na Sheria kali ya kuzuia uharamia huo:-

(a)Je, Serikali inatambua kuwa, sheria ya mwaka 1999 ya Hati Miliki ya kazi za sanaa haijaweza kutatua tatizo la uharamia wa sanaa?

(b)Je, Serikali inajua ukubwa wa biashara hii na imekusanya kodi kwa kiwango gani?

(c)Je, ni kazi ngapi za sanaa zilizokwishakamatwa na kufikishwa mahakamani na hukumu yake ni nini?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Moses Mlata, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b), na ( c ) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, si kweli kwamba, Sheria Na. 7 ya mwaka 1999 ya Hakimiliki na Hakishiriki, inayohusiana na kazi za sanaa, haijaweza kutatua tatizo la uharamia wa sanaa. Ukweli ni kwamba, sheria hii imesaidia kwa kiasi kikubwa kutatua tatizo hilo hapa nchini.

Sheria hii imewezesha wasanii na watengenezaji wa kazi za sanaa kutambua haki zao kama wamiliki au pale wanaposhirikishwa katika kuandaa na kuzitengeneza. Aidha, hivi sasa kazi nyingi za sanaa zinafanyika kwa kuwekeana mikataba mbalimbali.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inajua ukubwa wa biashara ya kazi za sanaa kama vile muziki ambapo biashara ya *CD, VCD* na *DVD*, inafanyika. Ukubwa wa biashara hii, unatokana na kukua kwa sekta ya utamaduni, kuongezeka kwa wasanii na wapenzi wa muziki na filamu mbalimbali zikiwemo za kitanzania na za nje ya nchi na hivyo kulifanya soko la bidhaa hiyo kuongezeka. *(Makofi)*

Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2005 hadi 2009, Serikali imekuwa ikikusanya kodi mbalimbali kutokana na biashara ya kazi za sanaa kama ifuatavyo:-

Tangu mwaka 2005, makusanyo kutokana na kodi ya mapato ya kazi za sanaa kwa watu binafsi imeongezeka kutoka shilingi 14,002,091.00 hadi kufikia shilingi 90,916,343.60 Mwezi Mei mwaka huu 2009.

Makusanyo kutokana na kodi ya mapato kwa makampuni, yaliongezeka kutoka shilingi 26,597,678.00 mwaka 2005 hadi kufikia shilingi 342, 532,020.82 mwezi Mei mwaka huu 2009.

Kodi ya mirahaba imeongezeka kutoka shilingi 53,005,525.00 mwaka 2006 hadi kufikia shilingi 146,193,972.00 mwezi Mei mwaka huu 2009, wakati mapato ya kodi ya maendeleo ya ujuzi au utaalam imeongezeka kutoka shilingi 2,520,559.25 mwaka 2005 hadi kufikia shilingi 323,614,968.06 mwezi Mei mwaka huu.

Aidha mapato ya kodi ya pango imeongezeka kutoka shilingi 26,226,573.90 mwaka 2006 hadi kufikia shilingi 118,247,986.36 mwezi Mei mwaka huu. Kodi inayotozwa kwa ajili ya ongezeko la thamani *(VAT)* imeongezeka kutoka shilingi 46,026,280.93 mwaka 2005 hadi kufikia shilingi 1,064,671.08 mwezi Mei mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya kodi iliyokusanywa kutokana na biashara ya kazi za sanaa nchini kwa kipindi cha mwaka 2005 hadi Mei mwaka, huu ni shilingi 2,086,472,366.92.

( c ) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2004 hadi sasa jumla ya kesi Nane (8) zinazohusiana na kazi za sanaa, zimekwishafikishwa mbele ya vyombo vya dola katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

Kati ya hizo, kesi Tano (5) zilisikilizwa katika mahakama ya Kisutu,Jijini Dar es Salaam, moja Mahakama ya Wilaya ya Kinondoni na mbili katika Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Musoma.

Kesi hizo zinahusu kutumia picha za sinema bila kibali, utengenezaji *CD* na Kaseti na utoaji wa nakala za *CD* kwenye kompyuta bila kibali cha mwenye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wale waliopatikana na makosa katika kesi zilizosikilizwa walitozwa faini ya kati ya shilingi 20,000/= hadi 200,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ningependa kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Martha Mlata, kwa juhudi kubwa anazozifanya katika kufuatilia maendeleo na matatizo yanayoikabili sekta ya utamaduni, hususani kazi za sanaa.

Kwa kutambua mchango wake, Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, amemteua Mheshimiwa Mlata, kuwa mjumbe wa Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza, jambo ambalo litasaidia kupata mchango na mawazo yake katika kutatua matatizo mbalimbali yanayoikabili fani ya sanaa.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri naomba nishukuru kwa kuteuliwa kuingia kwenye Bodi hii naamini nitatetea vizuri haki za wasanii hawa. Lakini pamoja na hayo ninaomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri maswali mawili madogo ya nyongeza.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba kwa kutokuwa na Kitengo au Idara maalum pale Wizarani ya kushughulikia biashara hii ambayo yeye mwenyewe anakiri kwamba Serikali inatambua ukubwa wake. Atakubaliana kwamba imeisababishia Serikali hasara kubwa ya mapato kwa sababu usimamizi wake umekuwa ni hafifu ukilinganisha na *data* hizi ambazo amezitaja hapa si sawa na ile kazi kubwa ambayo inafanywa na wasanii na vipato wanavyopata?

Lakini swali lingine la pili ninapenda kumwuliza Mheshimiwa Naibu Wziri kwamba amekiri mwenyewe kesi ambazo zimepelekwa Mahakamani kile kiwango kidogo walichotozwa wale waliokutwa na kazi ambazo sizo halali za sanaa 20,000 hadi laki mbili haoni kwamba hiyo ni dhuluma kubwa sana? Je, atakuwa tayari kuleta sheria hiyo ya mwaka 1999 kwa ajili ya mabadiliko ili kuweka kiwango kikubwa zaidi kwa maharamia hawa ili kukomesha uharamia huu wa kuwadhulumu wasanii nchini Tanzania? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli alivyosema Wizara sisi hatuna kitengo, lakini Serikali inafanya kazi kwa pamoja. Ni vizuri Mheshimiwa akafahamu kabisa kwamba pamoja na kwamba Wizara haina kitengo lakini sisi tuna Kurugenzi ya Utamaduni Tanzania tunashughulika na sera.

Lakini wenzetu wa Wizara ya Viwanda na Biashara wao wana *COSATA* ambacho ndicho chombo kinachoshughulikia masuala yote ya wasanii kwa mapato na matumizi na kuendeleza na kila kitu. Hata hizi *data* ambazo nimezitoa hapa hatukuzipata Wizarani kwangu nimezipata *COSATA* ambao wao ndio wamepewa dhamana ya kuendeleza sanaa na mapato ya wasanii katika nchi yetu kwa sababu wao ndio wanaoshughulikia

sheria ya Hai Miliki na Hati Shiriki. Kwa hiyo, tutaendelea kushirikiana kama Wizara kuona tunalifanikisha hili ili wasanii waweze kupata haki yao. *(Makofi)*

La pili kuhusu kesi, nataka nikubaliane naye Sheria namba 7 ya mwaka 2000 ambayo ilitungwa najua ina mapungufu. Wizara yetu inajitahidi kuihuisha ili tuilete Bungeni tuweze kuboresha zaidi ili wasanii waweze kupata mafao yao vizuri. *(Makofi)*

Na. 89

**Programu ya Mafunzo Kwa Waandishi wa Habari**

**MHE. ESTHERINA J. KILASI (K.n.y. MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE)** aliuliza:-

Kwa kuwa, mwezi Aprili, 2006 Serikali kwa kutambua umuhimu wa vyombo vya habari kwa maendeleo ya nchi iliahidi kuanzisha programu maalum ya mafunzo kwa Waandishi wa Habari ndani na nje ya nchi ili kuwaendeleza kitaaluma na kuwawezesha kubobea kwenye nyanja mbalimbali kama vile Uchumi, Sheria, Uhasibu, Kilimo, Utamaduni na Michezo:-

Je, ni Waandishi wa Habari wangapi waliosomeshwa chini ya programu hiyo tangu itangazwe miaka mitatu iliyopita?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mbunge wa Kyela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, Serikali kwa kutambua umuhimu wa vyombo vya habari kwa maendeleo ya nchi iliahidi kuanzisha programu maalum ya mafunzo kwa Waandishi wa Habari ndani na nje ya nchi ili kuwainua kitaaluma na kuwawezesha kubobea katika nyanja mbalimbali kama vile Uchumi, Sheria, Uhasibu, Kilimo, Utamaduni na Michezo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu haukuweza kuanza kutekelezwa kutokana na shughuli zake kuwemo kwenye mapendekezo ya Muswada wa Sheria Mpya ya Kusimamia vyombo vya Habari ambao mchakato wake bado unaendelea hivi sasa na umefikia katika ngazi ya Baraza la Mawaziri ili uweze kufikishwa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya masuala yaliyomo kwenye mapendekezo ya Muswada huo yanahusu kuanzishwa kwa Bodi itakayosimamia viwango vya elimu na taaluma ya uandishi wa habari pamoja na maadili ya taaluma hiyo. Aidha, pendekezo lingine linahusu kuanzisha Mfuko wa Mafunzo ya Waandishi wa Habari.

Mapendekezo haya mawili yana uhusiano na programu iliyotarajiwa kuanzishwa. Hivyo basi, Serikali iliona ni vizuri ikasitisha kuanza kwa utekelezaji wa programu hiyo ili mapendekezo ya Muswada mpya yakishafikishwa iwe rahisi kwa Bodi ya Mfuko utakaonzishwa kuweza kusimamia ipasavyo progamu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na programu hiyo kutoanza rasmi lakini baadhi ya wamiliki wa vyombo vya habari kwa kutambua umuhimu wa Waandishi wa Habari, katika nyakati tofauti wamekuwa wakiwasomesha Waandishi wao ili kuinua taaluma zao. Tangu mwaka 2006 hadi sasa, baadhi ya vyombo vya habari vimewasomesha wafanyakazi wake (Waandishi wa Habari) masomo ya juu zaidi ili kuwainua kitaaluma kama ifuatavyo:-

1. *Daily News*/Habari Leo waliopata mafunzo ya:-

   · Shahada ya Kwanza - 4
   · Stashahada - 3

2. Uhuru/Mzalendo waliopata mafunzo ya:-

   · Shahada - 12
   · Shahada ya Uzamili - 4

3. *TBC* waliopata mafunzo ya:-

   · Shahada ya Uzamili - 3
   · Shahada - 5
   · Stashahada - 3

4. Idara ya Habari (MAELEZO) waliopata mafunzo ya:-

   · Shahada ya Uzamili - 4
   · Shahada - 2
   · Stashahada - 3

5. *Radio Tumaini* waliopata mafunzo ya:-

   · Shahada ya Kwanza - 1
   · Uandaaji vipindi - 41
   · Teknolojia ya Habari - 2
   · Usalama na Ishara - 5
   · Urushaji wa Vipindi - 3

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo haya yamepatikana nje ya nchi, Ujerumani, Italia na Zambia. *(Makofi)*

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri na nina swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa amekiri kwamba kuna umuhimu sana wa kupata mafunzo na hali halisi inaonekana kwamba kwa masomo haya aliyopendekeza ni dira kubwa sana kwa Waandishi wa Habari na kupunguza malalamiko mengi ya wananchi ambao Waandishi wa Habari wamekuwa wakiandika?

Aidha, sio kwa kupenda kwa sababu ya kutokujua utaalamu, haoni kwamba ni vitu viwili tofauti kusubiri Muswada na kuanza kufanya mafunzo kama Msimamizi Mkuu wa Kitengo hiki na Waziri mwenye dhamana habari ili kuondokana na haya matatizo, sheria ifuate wakati programu inaendelea kufanyiwa kazi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na yeye na ndio maana nimetoa mfano nimesema pamoja na kwamba tunasubiri sheria mpya ije ambayo itahusika na Bodi pia itahusika na Mfuko wa Kuwaendeleza Waandishi wa Habari.

Lakini nimesema vyombo vya habari vyenyewe tayari vimeshaanza kusomesha watu, ndio maana nimetoa mfano hapa nikitegemea kwamba suala hilo lingeulizwa kwamba Uhuru wanasomesha, *Daily News* wanasomesha, Habari Leo wanasomesha nategemea *ITV* na vyombo vingine navyo vinaendelea kusomesha. Sisi kama Serikali pia fungu dogo tunalolipata tunaendelea kusomesha.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. *(Makofi)*

Kwa kuwa vyombo vya habari vingi baadhi vina tabia ya kupotosha ukweli wa mambo. Kama ni nchi iliyoendelea, hakuna nchi iliyoendelea kama Marekani na juzi ilifika pahali *CIA* kumkemea aliyekuwa *running mate* kwa kutoa habari dhidi ya Rais Obama kuhusu sera zake. Inakuwaje Serikali yetu inashindwa hata kukemea baadhi ya vyombo vya habari vinavyopotosha habari ambazo zinahusu Serikali iliyoko madarakani ambayo imepigiwa kura na wananchi wengi, kwa nini wasiheshimu maamuzi ya wapiga kura? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikubaliane naye kwamba ni kweli kuna baadhi ya vyombo vya habari vinakiuka maadili. Lakini Waheshimiwa Wabunge naomba mkubaliane na mimi kwamba ndio maana unaona tumechukua muda mrefu sana kuleta sheria hii mpya ndani ya Bunge. Tumefanya hivyo makusudi ili tuweze kutoa mwanya mkubwa kwa ajili ya wadau wengi kutoa mawazo yao katika sheria hii mpya ambayo tunaamini sheria hii itakuwa na uwezo wa kuweza kutatua baadhi ya matatizo ambayo Mheshimiwa Rished ameyasema.

Ni kweli hakuna uhuru wa habari usiokuwa na mpaka duniani kote. Haijatokea kwamba mtu akaandika tu anavyotaka yeye lazima afuate matakwa ya sheria na

kuheshimu sheria za nchi. Sheria hii mpya inatuwezesha kuanzisha Bodi itakayosimamia taaluma ya habari kitu ambacho sasa hivi hamna, sheria hii mpya itatuwezesha kuwa na Mfuko wa Mafunzo kwa wanahabari ili wawe na taaluma ya kutosha. Moja ya tatizo ambalo tumeliona ni weledi, Waandishi wengi bado wana tatizo la weledi. Tunaamini sheria hii ule Mfuko utusaidie kuwasomesha ili waweze kuwa na maadili mazuri na kuelewa taaluma yao inavyostahili. Kwa hiyo Serikali tutahakikisha kwamba sheria hiyo tunaileta haraka ili tuweze kupambana na matatizo haya.

**NAIBU SPIKA:** Naomba yawe *brief* maswali yenyewe. Sema maswali yawe mafupi. Hamia nyingine haisikiki. Narudia, sema lakini maswali yawe mafupi. Kwani nyie wengine mnahusika nini na kwamba haisikiki, mimi nasema haisikiki. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Imewaka kabla hata sijaweka kile kidudu , sijui nzima hii, iko sawa. (*Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru naomba niulize swali dogo moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa programu ya mafunzo inalenga kuboresha taaluma ya uandishi. Na kwa kuwa mojawapo ya mambo ambayo yanaathiri taaluma hii ni pamoja na Waandishi wengi kutokuwa na *scheme of service* pamoja na uhakika wa mshahara hasa *correspondent* katika magazeti binafsi na vyombo vya habari binafsi. Je, Serikali itatoa mwongozo kwa wenye vyombo hivyo ili waweze kuboresha mambo hayo pia au sheria mpya itakuja kuzingatia hayo mambo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri naomba majibu yawe mafupi tunachukua dakika 15 swali moja.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumhakikishia kwamba sheria mpya itazingatia hayo ambayo ameyazungumza.

Na. 90

**Serikali Kukarabati Nyumba na Vituo vya Walemavu**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilikwishaahidi kukarabati nyumba za walemavu katika kituo cha Sukamahela Tarafa ya Kilimatinde pamoja na nyumba na vyoo katika Chuo cha Wasioona cha Singida Mjini ambacho kina hali mbaya sana:-

Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa pekee wa kutoa fedha kwa ajili ya ukarabati huo ili kunusuru majengo na nyumba hizo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-_

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali iliahidi kukarabati nyumba za wazee na wasiojiweza katika makazi ya Sukamahela na Chuo cha Wasioona Singida. Hivi sasa, Wizara imekwisha kamilisha taratibu zote za manunuzi zinazoelekeza ukamilishaji wa mikataba kati ya Wizara, Wakala wa Majengo na Wakandarasi walioteuliwa kufanya kazi hizo. Shilingi 105,229,800/= zimetengwa kwa ajili ya kukarabati nyumba 20, ujenzi wa jiko, bafu na vyoo katika makazi ya Sukamahela. Kazi hiyo wamepewa wakandarasi wawili, Kyombo *Photo Fast* na Kisulubu *General Supplies*, wote wa Singida na "*notification of award*" zilitolewa tangu mwezi Aprili, 2009. kwa upande wa Chuo cha Wasioona Singida, chuo hicho kimetengewa shilingi 66,210,000 katika Bajeti ya 2009/2010 kwa ajili ya ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya kukamilisha taratibu hizo za kisheria, kazi ya ukarabati wa majengo ya Chuo cha Wasioona Singida na Makazi ya Sukamahela sasa utaanza hivi karibuni na kuendelezwa katika mwaka ujao wa fedha (2009/2010)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na nashukuru majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba yanatia moyo. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa kituo cha Sukamahela pamoja na Chuo cha Wasioona hata Bajeti ya chakula wanachopelekewa kwa kila kota ni ndogo sana. Mfano Chuo cha Wasioona wanapelekewa shilingi 1,000,000 kwa miezi mitatu. Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kuongeza Bajeti kwa chuo hiki kwa kuwa wako wengi sana pamoja na kituo cha Sukamahela.

Pili, kwa kuwa Chuo cha Wasioona kina tatizo la usafiri na chuo hicho kina walemavu wa aina mbili wako wasioona na wako walemavu wa viungo maana hawatembei. Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuwapatia usafiri ili uweze kuwasaidia hata kuwapeleka hospitali pale wanapoumwa? (*Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Chilolo kwa kufuatilia sana masuala ya walemavu na wasioona katika mkoa wake wa Singida. Nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha zinazotolewa shilingi 1,000,000 kwa kila miezi mitatu hazitoshi kutokana na kupanda kwa gharama za maisha kama inavyofahamika.

Wizara tunaliangalia hili kwa hiyo tunalifanyia kazi pamoja na vyuo vingine ili fedha za chakula ziweze kuwa za kutosha lakini hii itategemea vile vile na Bajeti iliyokuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu gari la kuwapa Chuo cha Wasioona pamoja na wale wengine Sukamahela nitakachosema ni kwamba Wizara tunalifahamu, kama nilivyokuwa nikisema katika Bunge lako Tukufu kwamba tunayo Makambi mengi sana na Vyuo vya Watu wenye ulemavu Wasioona pamoja na walemavu wa aina nyingine, Makambi ambayo ya Serikali ni zaidi ya 17. Serikali sasa hivi kupitia Wizara ya Afya inafanya mkakati wa kuweza kuona uwezekano wa kuwapatia magari hata kama sio mapya lakini yale yaliyopo katika Wizara tunafanya utaratibu sasa hivi wa kuweza kuhakikisha kuangalia yale ambayo yako ya ziada tuweze kuyachukua na kupeleka katika vyuo pamoja na Makambi kuweza kutoa msaada huo.

Na. 91

**Gharama za Matunzo ya Mtoto Aliyezaliwa Nje ya Ndoa**

**MHE. SALIM ABDALLAH KHALFANI** aliuliza:-

Kwa kuwa, sheria imeweka gharama ya shilingi 100/= kwa mwezi au shilingi 15,000/= kwa mkupuo kutunza mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa lakini viwango hivyo vinaonekana kupitwa na wakati:-

Je, ni lini Serikali italeta Bungeni Muswada wa Sheria Kufanya Marekebisho kwenye sheria husika ili kuweka viwango vinavyofaa vya kutunza watoto waliozaliwa nje ya ndoa kulingana na hali halisi ya maisha ya sasa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfani, Mbunge wa Tumbe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majukumu mengine Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inasimamia huduma ya mafunzo kwa watoto wanaozaliwa nje ya ndoa, huduma hii hutolewa chini ya Sheria ya Matunzo ya Watoto waliozaliwa nje ya ndoa, Sura Na. 278 ya mwaka 1949.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati sheria hii ilipotungwa kiwango cha shs. 100/- kwa mwezi au shs. 15,000/= kwa mkupuo kilikuwa kinakidhi mahitaji ya kumtunza mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa kwa kipindi kile. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya kiuchumi na kupanda kwa gharama za maisha nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa viwango hivyo havikidhi mahitaji ya kumtunza mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria zinazohusu watoto ni nyingi na zinasimamiwa na Wizara mbalimbali. Baadhi ya sheria hizi ni za zamani sana na haziendani na mabadiliko katika nyanja za kijamii, kisayansi na kisiasa. Hii imepelekea Serikali

kufanya mapitio ya sheria zote hizi ikiwemo sheria ya matunzo kwa watoto waliozaliwa nje ya ndoa.

Hivi sasa tumeandaa rasimu ya Muswada jumuishi kuhusu watoto kwa lengo la kurekebisha mapungufu yaliyobainishwa. Sheria jumuishi itakapopitishwa italinda haki za watoto kulingana na matakwa ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto. Baada ya rasimu ya Muswada kupita hatua zote za awali Muswada utawasilishwa hapa Bungeni ili kuwapa fursa Waheshimiwa Wabunge kuujadili na kuutolea mapendelezo ikiwa ni pamaoja na kima stahiki cha kuwatunza watoto hao.

Katika kipindi hiki cha mpito, wakati tunangojea sheria mpya kutungwa, Idara ya Ustawi wa Jamii inafanya majadiliano na wazazi husika ili wakubaliane kuhusu kiwango wanachoona kitatosheleza mahitaji ya matunzo kwa mtoto hao kulingana na uwezo wa mzazi.

**MHE. SALIM ABDALLAH KHALFANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza suala la nyongeza.

Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo yanaonesha kujirudiarudia katika suala hili, naomba kuuliza swali. Hivi Serikali haioni uwepo wa haja ya udharura wa kukamilishwa kwa Muswada huu kuletwa hapa Bungeni ili kuwatendea haki hawa watoto pamoja na wazazi wao ambao wanawashughulikia?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu langu la msingi nimesema kwamba sheria inayotumika sasa hivi ni ya mwaka 1949. Na vile vile nimesema kwamba haki za mtoto zina sheria nyingi ambazo zimepitwa na wakati na sasa hivi Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wizara nyingine wanazipitia na kuhakikisha kwamba wanazileta hiyo sheria jumuishi sasa itakapokuwa tayari tutaileta hapa.

Sasa sioni kwamba haya mambo yangu ya kujirudia ni yapi kwa sababu ninasema kwamba sheria itakapokuwa tayari tutaileta hapa na Waheshimiwa Wabunge mtaijadili na baadae tutapata sheria moja ambayo itamlinda mtoto.

Na. 92

**Mawasiliano ya Simu za Mkononi – Tarafa ya Mgwashi**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Kampuni ya Simu za ZAIN ilikwishachagua eneo la kujenga mnara wa mawasiliano ya simu katika kijiji cha Mgwashi, Tarafa ya Mgwashi Jimbo la Bumbuli sasa yapata mwaka mzima na katika kufuatilia nimejulishwa kuwa kinachochelewesha ni kutopatiwa kwa wakati taarifa ya athari za mazingira *(Environmental Impact Assessment Study (EIA):-*

Je, ni nani anayehusika kutoa taarifa khiyo na itatolewa lini ili kuiondolea lawama Kampuni hiyo yenye ufanisi wa hali ya juu *ZAIN?*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI YA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli napenda kutoa maelezo yenye ufafanuzi kidogo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imekuwa inakabiliwa na tatizo kubwa la uharibifu wa mazingira unaotokana na shughuli mbalimbali za maendeleo. Moja ya shughuli hizo za maendeleo ni usimikaji wa minara ya mawasiliano ya simu za mkononi.

Kutokana na kasi ya kuendelea kuharibika kwa mazingira ya sehemu mbalimbali nchini, Baraza la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira nchini *National Environmental Management Council* (NEMC,) lilitoa maelekezo kwamba Kampuni za Simu zifanye tathmini ya uharibifu wa mazingira (*Environmental Impact Assessment*) kabla ya kusimika minara ya mawasiliano ili Halmashauri za Miji na Serikali za Mitaa ziweze kutoa kibali cha kusimika minara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo mafupi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Willliam H. Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli kama ifuatavyo. Ni kweli kuwa Kampuni ya Simu za Mkononi ya *ZAIN* ilichagua eneo la kujenga mnara wa mawasiliano ya simu katika kijiji cha Mgwashi, Tarafa ya Mgwashi, Jimbo la Bumbuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni hiyo ya ZAIN imetakiwa na Baraza la Usimamizi na Udhibiti wa mazingira nchini *"NEMC"* kufanya *"Environmental Impact Assessment"* ili ipitiwe na *"NEMC"*. Mnamo mwezi Februari 2009, Kampuni hii iliwasilisha mpango wao wa ujenzi wa mnara (*Project Brief)* kwa Baraza la Usimamizi na Udhibiti wa Mazingira *"NEMC"*.

Kufuatana na utaratibu wa kisheria taarifa hiyo ilifanyiwa uchambuzi (*screening)* ili kubaini kama inakidhi mahitaji ya kanuni za tathmini ya Athari kwa Mazingira *(EIA and Audit Regulations*, 2005), Sheria ya Mazingira (*EMA Cap. 191*) inaeleza kuwa Kampuni/Mwekezaji anaweza kupewa hati katika hatua za awali za utekelezaji wa mradi kama itaonekana kuwa tathmini ya kina (*full EIA*) haihitajiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya ripoti ya *ZAIN* ilionyesha mapungufu yafuatayo:-

1. Taarifa kuhusu ushirikishwaji wa majirani walio karibu na eneo la mradi hazikuwa zinatosheleza.

2. *ZAIN* hakuwa amepata kibali cha Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga (*Tanzania Civil Aviation Authority (TCAA)* ambayo ilionekana ni muhimu kwa ajili ya usalama wa ndege *(aircraft safety*) zinazopita eneo hilo.

3. Kampuni ya ZAIN ilitakiwa kupata kibali cha Ardhi chenye ushahidi wa Serikali za Mitaa *(Land Lease Agreement and Local Government Endorsment).* Kibali hiki ni kigezo kwa miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Machi 2009, Kampuni ya ZAIN ilijulishwa kuhusu mapungufu haya ya kuelekezwa kuyakamilisha, tangu muda huo ZAIN haijawasilisha ripoti iliyokamilika kama ilivyoelekezwa na "NEMC".

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia tayari tumemuandikia Mkurugenzi Mtendaji wa ZAIN kutaka kujua ni kitu gani kilichomkwamisha, na iwapo tunaweza kutoa msukumo wa kusaidia kukamilisha matakwa ya "NEMC" ili shughuli za ujenzi wa mnara huo zisichukue muda mrefu sana.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya kitaalamu ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuwa sasa tumeshaelewa tatizo ni nini.

Je, atakubaliana na mimi kwamba kuna haja ya kukutana pengine baada ya Mkutano huu wa Bunge katika Ofisi yake wawepo watu wa Usafiri wa Anga, watu wa NEMC na ZAIN na mimi ili tuone kila mmoja jukumu lake litatekelezwa katika muda gani na kuwekeana *time frame*?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**: Mheshimiwa Naibu Spika, sioni tatizo kwa sisi kukutana, lakini nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge hata sisi tayari tumeshawaandikia watu wa TCAA kujua kama wao wana *objection* yoyote katika hili na wewe mwenyewe uliniahidi kwamba utatoa msukumo katika masuala ya *Land.*

Kwa hivyo si tatizo ninaweza nikaitisha hicho kikao sote watatu tukakutana tukaona namna gani tunaweza ku-*solve problem* hii.

Na. 93

**Mawasiliano ya Simu za Mkononi – Namtumbo**

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imesaidia upatikanaji wa simu katika Jimbo la Namtumbo kwa sehemu kubwa lakini bado kuna Kata kubwa zenye watu wengi na uchumi mzuri kama vile Kitanda, Namabengo, Magazini, Luchili ambazo hazina minara ya simu hivyo kukosa mawasiliano kabisa na maeneo mengine:-

Je, Serikali inaweza kuendeleza busara zake kwa kuwakumbusha na kuzisimamia Kampuni za Simu kuja kuweka mawasiliano katika Kata hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *VODACO*M imefanya utafiti katika maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge kwa lengo la kufikisha mawasiliano katika maeneo hayo. Tathmini ya kiufundi imefanyika katika Maeneo ya Magazini, Chiwana na Namabengo ambayo wanategemea yatakidhi mahitaji ya huduma ya mawasiliano katika maeneo hayo na maeneo jirani ya Kitanda na Luchili. Maeneo mengine yaliyofikiwa katika tathmini hiyo ni pamoja na Ligera na Lusewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya kiufundi, ikikamilika hatua za utekelezaji wa kuweka mtambo wa mawasiliano zitafanyika. Hivi sasa Kampuni ya *VODACO*M inaendelea na ujenzi wa mtambo wa mawasiliano katika eneo la Mkongo Wilayani Namtumbo na unategemewa kuanza kazi wakati wowote mwezi huu wa Juni, 2009. Kampuni ya *ZAIN* tayari imeshafikisha mawasiliano katika jimbo la Namtumbo; na Kampuni ya *ZANTEL*, imepanga kuyaingiza katika mipango yake ijayo maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge (Kitanda, Namabengo, Magazini na Luchili), kwa hivi sasa *ZANTEL* haina mawasiliano katika Wilaya ya Namtumbo.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niipongeze Serikali hususan Naibu Waziri Dr. Maua Daftari na nampa pole kwa kifua anachoumwa.

**NAIBU SPIKA:** Ulizwa swali bwana habari hizo (*Kicheko*)

**MHE. VITA R. KAWAWA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza kwa kusimamia vyema sekta hii na mpaka sasa hivi nazungumzia maeneo machache ya kukamilika kwa simu za viganjani. Swali; kwa kuwa mpaka Juni, 2006 Wilaya ya Namtumbo ilikua haina kabisa mawasiliano ya simu za viganjani; na kwa kuwa sasa hivi imebakia asilimia 25 tu ya maeneo hayo kukamilishwa. Je, Naibu Waziri atakua tayari kuja Wilayani Namtumbo katika uzinduzi wa minara hii aliyoitaja ili tuje kumpongeza na kuipongeza Serikali.

Swali la pili, kwa kuwa kuna teknolojia ya mkonga ambayo inakuja na kwa kuwa tuna kampuni yetu ya simu ya *TTCL* ambayo ipo mahututi je, Serikali inaweza kuipa uwezo wa kujiendesha ili iweze kuja ku-manage network hiyo na kuanzisha *telecentres* katika Wilaya zetu zitakazoingiza katika mkongo huo na kusaidia utoaji wa huduma hii katika *tele medicine* na *e-government? (Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba radhi kwa sababu ya kifua. Kwanza nakubaliana na Mheshimiwa Vita Kawawa pindi watakaponialika wenye kampuni na mimi wananihitaji basi sina budi nitakuja. Nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Vita na Halmashauri ya Namtombo kwa juhudi mnazozifanya.

Wiki iliyopita tulikuwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Namtumbo pamoja na Mkurugenzi wa Namtumbo na Mtaalam wao wa *ICT* tukijadili namna gani tunaweza kusaidiana kufikisha mawasiliano katika maeneo yake. Ni kweli hali ya *TTCL* sio nzuri lakini hivi sasa Serikali inafanya juhudi ya kuifufua *TTCL* ili iweze kufanya kazi yake inayotakiwa na waweze kuisimamia ipasavyo masuala haya ya mkongo. Kubwa ni kupata capital ambayo tayari Waziri wa Fedha anashughulikia na kujipanga vizuri wao wenyewe namna ya kulishughulikia suala hili.

Lakini nategemea kwamba mkongo utakuwa ni wa manufaa kwetu sote iwe kwenye *e-government* au *tele medicine e-tourism* na *electronics* zozote. Nia ya Serikali ni kuona mkongo unafikishwa maeneo yote.

**NAIBU SPIKA:** Kwa kuzingatia kanuni zetu tumeshindwa kumalizia swali namba 94 kwa sababu muda wa maswali umefika na hatuna sababu hata moja ya kuongeza muda. Lakini Waheshimiwa Wabunge tumeshaanza kuhutubia maswali badala ya kuulizwa maswali matokeo yake ni haya. Tunashindwa kumaliza maswali maana mtu anatumia muda mwingi kuulizwa swali.

Nimefanya *statistics* ya muda wa maswali kuna swali moja limechukua dakika kumi, kuna jingine limechukua dakika tisa, lingine dakika tisa, kumbe wastani wetu ni dakika tano kilwa swali pamoja na nyongeza. Kwa hiyo naomba Mawaziri wajibu maswali kifupi na Wabunge pia waulize maswali ya nyongeza kifupi. Mimi nadhani tukifanya hivyo itakua rahisi kwa kila mtu. Kwa hiyo baada ya kusema hivyo imebidi tuliache swali namba 94 naomba kesho liweze kuingia kwenye order paper.

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni mbele yetu. Kuna mgeni wa Mheshimiwa Lucy Nkya Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ambaye ni mtoto wake anaitwa Petro Nkya. Tuna wageni wa Mheshimiwa Diana Chilolo ambao ni Salum Mnanji na watoto wao wawili ambao ni wafanyabiashara na makada wa CCM Singida. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Shah ambao ni Afisa Habari Mkuu kutoka Kampuni ya *Softnet* Bwana Gilbert Herman na John Gama, karibuni sana. Tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge Monica Mbega, Mheshimiwa Dr. Ishengoma na

Mheshimiwa Dr. Msekela ambao ni Baba Askofu Damas Mkasa kutoka Dodoma na Baba Askofu Alpha Modigae kutoka Mwanza. Karibuni sana. Tuna wageni wa Mheshimiwa Emmanuel Luhahula ambao ni wapigakura wake ambao ni Moses Joshua, Reuben Malume na Samuel Mshikona. Karibuni sana Bungeni kwetu. Tunao, wageni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambao ni Baba Askofu Amos Mhagachi kutoka Dayosisi ya Kati ya Kanisa la Mennonite Tanzania na Rev. Manase Katibu wa Dayosisi Tanzania. Karibuni sana. Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Pwani ambao hawa wageni ni viongozi wanne wa Chama cha Soka wanawake Mkoa wa Pwani wakiongozwa na Mwenyekiti na Katibu wa Chama hicho.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Susan Lyimo ambao ni watoto wake wanaosoma *St. James Seminary* Moshi na *Mlimani Primary School University of Dar es Salaam* Aman Ngowi na Baraka Ngowi. Tunao wanafunzi kumi kutoka shule ya Sekondari ya *Central* Dodoma pamoja na walimu wao. Karibuni sana. Ninaye mgeni wa Mheshimiwa Muhonga Said Ruhwanya ambaye ni Ester Jonas anatokea Kigoma Manyovu karibu sana. Naomba uandike na sio kuleta kwa vikaratasi.

Baada ya hapo nina matangazo mawiali tu. Mwenyekiti wa Kamati wa Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Mheshimiwa Wilson Massilingi anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo leo tarehe 23 Juni saa saba mchana ukumbi namba 231. Tangazo lingine, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anawaalika Wakuu wa Mikoa wote, Makatibu Tawala na Waheshimiwa Wabunge kutoka Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Mbeya, Mwanza, Tabora, Tanga na Ruvuma kwenye tafrija fupi ya kugawa magari ya sinema kwa ajili ya kampeni ya elimu ya UKIMWI katika viwanja vya Bunge itakua saa saba na nusu mchana. Kwa hiyo nadhani Mikoa hiyo mmejitambua. Nafikiri na wengine mtakaribishwa. Baada ya kusema hayo tunaendelea na shughuli za leo.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2009/2010 – Ofisi ya Waziri Mkuu

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jana Mheshimiwa Spika, alipoahirisha Kikao cha Bunge aliwataja wazungumzaji wa kwanza wanne halafu wengine tutaendelea nao baadaye. Hao ni Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Vita Kawawa na Mheshimiwa Grace Kiwelu pia ajiandae.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia. Awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ajili ya hotuba yake nzuri lakini pia nimpongeze kwa kazi nzuri anayoifanya pamoja na Mawaziri wote wa Wizara zote na Makatibu Wakuu,

Watendaji wote lakini kipekee nimpongeze sana Waziri wa TAMISEMI, Mama Kombani pamoja na Naibu Waziri. Lakini hapa kipekee kwa sababu Wizara hii nadhani wamenichoka kwa usumbufu naomba niwataje hasa Bwana Nyimbi, Mama Macha, Bwana Kabuje, Mama Itanisa, Eng. Shemangwale na Bwana Lemnge.

Kwa kweli nimeonekana msumbufu maeneo mengi na Wizara nyingi sio siri lakini lengo lilikuwa si baya ni kutaka maendeleo. Kama niliwakwaza mahali basi naomba mnisamehe lakini nawapongeza sana kwa kazi nzuri ambayo mmefanya hasa kwangu mimi, maana Kilindi sio sifa ya kwangu mimi. Ni kweli nimechangia kwa kiwango kikubwa, wengi mtakumbuka Kilindi ilikua haijulikani hata ipo sehemu gani, sasa hivi kila mtu anaipenda Kilindi watu wanaimezea mate usiku na mchana na wanajitokeza. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kazi hii sio ya kwangu Mbunge pekee, pasipo mshikamano na msukumo mkubwa niliyoupata katika Serikali kwa kweli nisingefika hapa. Wizara zote, Mawaziri wote, Makatibu Wakuu wanajua mmoja mmoja. Hadi wakiniona madirishani wengine wanatamani wakimbie wanauliza sijui anataka nini leo. Lakini ni kwa nia njema kabisa wananchi wa Kilindi wanatoa shukrani kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kutoa shukrani za wananchi wa Kilindi kama mwakilishi wao. Kwa kweli sisi binafsi tunaishukuru sana Serikali. Sasa hivi ni Wilaya ya mfano mambo yote yanakwenda kwa kweli lazima niseme. Nimesimama tu kwanza kikubwa kutoa shukrani, barabara ilikua ikifika masika sisi basi tumekatwa mpaka baada ya masika. Ni shukuru sana sasa hivi barabara zinapitika wakati wote wenye magari madogo mnakaribishwa, umeme Disemba moja utawaka mpaka Makao Makuu, maji ukiacha maeneo machache, Bwawa la Saunyi ni maeneo ambayo yanafanyiwa kazi sasa hivi. Ndiyo maana siwezi kulalamika kwa sababu yapo kwenye mkakati niseme pia nako tunashukuru; miradi ya kilimo mbalimbali tumefaidika sana wanakilindi wanashukuru, ingawaje michakato imeanza kwingine imekamilika lakini bado tunaendelea. Upande wa elimu tumepata hosteli tumepata maabara moja. Kwa kweli tunashukuru sana na tuna mikakati ya kujenga Chuo cha Ufundi. Aidha kwenye upande wa ardhi hati miliki ziko kwenye *process* kwa ajili ya wananchi wetu, tunafanya kwanza *land use plan* halafu tuweze kuwapatia hati miliki. Kwa hiyo mambo yote kwa kweli yanakwenda. Nimefurahi nimeangalia jedwali tumeongezewa vijiji 33, kwa kweli tunaishukuru Serikali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya mawasiliano pia tunashukuru sana zimebaki Kata chache sana ambazo nazo ziko kwenye mchakato ambazo ni Kikunde, Lwande, Mswaki, Mkindi, Saunyi, Pagwi na Masagalu lakini nazo mikakati iko katika hali nzuri na jana niliongea na Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano kuhusu *TTCL* bado haijafika kwetu na ameniahidi kwamba atafanya kila linalowezekana akitoa tahadhari ya hali halisi ilivyo. Kwa hiyo kwa kweli kwa upande wetu sisi wanakilindi tunashukuru sana. Kipekee nichukue fursa hii niwapongeze sana Madiwani kwa kweli wanafanya kazi kubwa sana, wanakaa vikao bila kuchoka na ninashukuru sana kwamba maslahi yao jana Waziri Mkuu alisoma kwamba yanatetewa sasa hivi yataboreshwa.

Lakini vilevile niombe tu kwamba ingawaje mambo ya *(Capacity Building)* kupewa uwezo yapunguzwe au yasimame kwa muda. Lakini kwa Wilaya ya Kilindi, utuangalie kwe jicho la tofauti bado tunahitaji kupewa msukumo na nadhani kuna mchakato ambao unaendelea na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa alitakiwa atoe kibali kama hajatoa ninahakika kwa uzoefu wake atakuwa amekwishakitoa waendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kutokana na jiografia yetu, kwa kweli vyombo vya usafiri ni muhimu sana. Kwa waliofika Kilindi kona moja hadi nyingine si chini ya masaa manne. Kwa hiyo nadhani hili liwe kipaumbele kwao. Niwapongeze sana kupita nafasi hii watendaji wote pamoja na uchache wao mkubwa lakini kazi imeweza kwenda. Pamoja na pongezi nyingi lakini nina mambo mawili, matatu ya kusema. Tuna jengo la Halmashauri na jengo hili lilikuwa limekadiriwa kiasi cha milioni 800 pamoja na ukumbi. Limekwenda kwa sababu siku zinavyozidi kwenda sasa hivi tumeshapewa bilioni 1.3 lakini bado hata ukumbi haujaanza. Ninaomba sana uangaliwe mkakati angalau tuangalie namna nyingine za kufanya hizi kazi. Ninahakika kabisa kama tungelifanya sisi pale jengo lingekuwa limekwisha siku nyingi na gharama ingekuwa ni ndogo. Saa hapo tulipofikia nadhani kunahitajika karibu bilioni tena kuweza kumaliza. Ninaomba labda huyu mkandarasi alipofikia, wenye mamlaka kama itakubalika aishie pale atakapokuwa ameishiwa kulipwa halafu tuone utaratibu wa sisi wenyewe kuona tunamalizaje. Sambamba na hizo nyumba 10 ambazo zinakusudiwa kujengwa kwa milioni 30 kila moja. Nadhani tukiangalia utaratibu ambao kwa kweli ni mzuri tunaweza tukajenga kwa bei nafuu kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu elimu ya chini sasa iwe ni kidato cha nne. Tumejenga shule ni kweli kabisa, lakini kinachosikitisha unakuta mahali unaambiwa wanafunzi wamefeli na madarasa mengine bado yako tupu. Watafaulu vipi?

Wanafunzi wako 800 walimu wako watatu, unategemea watafaulu vipi hasa hawa watoto wa darasa la saba ni wadogo mno hawana cha kufanya na nadhani nyakati zimebadilika na tupandishe kiwango chetu cha elimu huku tunaboresha hayo mambo mengine ya walimu na kadhalika lakini kipande na kifikie mahali pale. Ili kwamba hata tukiwa na darasa moja kila sekondari kwa wanafunzi ambao hawakufanya vizuri waendelee kupewa mshukumo hasa pale tunapojua matatizo ni nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba niseme. Hili nalisema kwa unyenyekevu. Kuna ugonjwa mbaya na wa hatari umeingia Tanzania na ni hatari zaidi hata kuuzungumzia. Kila mtu anaugusiagusia halafu anaukimbia kwa sababu ni hatari sana. Ugonjwa huo dawa yake ipo kwa Waziri Mkuu na Rais na Makamu wa Rais.

Lakini vilevile makanisani na misikitini kwa dua na sala. Ugonjwa huo ni wa kukosa utekelezaji kwa wakati sahihi kwa makusudi yaliyopangwa na kukosa uamuzi kwa wakati sahihi. Tanzania ndiyo tatizo letu. Sasa hivi hakuna utekelezaji, haya maneno unayosikia yanaenda yakirudi tunawapa hoja wenzetu wa mkono wa kulia pale kwa sababu mambo hayatekelezeki ndiyo maana yanarudi. Jana nilimshangaa kumsikia Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha anamjibu Mheshimiwa Slaa kwamba tafuta hoja nyingine. Atatafutaje hizi mmeshindwa kutatua hizo zingine mtafanyaje?

Mimi nitazungumzia sasa hivi vitambulisho najua nitaambiwa labda nitafute hoja nyingine. Siwezi kunyamaza, lazima tupate ufumbuzi na bila kufanya hivyo kweli itakuwa ngumu. Sisi pia tunapoongea kazi yetu Bunge ni kusimamia, hatuangaliagi mtu, sisi tunaangalia hoja inayemkumba ni bahati mbaya yuko katika ile hoja. (*Makofi*)

Kwa hiyo majibu yatatoka, sasa tusieleweke kama sisi Bunge kazi yetu ni kunyosha vidole tunasema ambayo yanakusudiwa. Naomba tu niseme mambo mengi yanakua hayatekelezwi. Mimi nina wazee wangu wanadai pensheni, wakina Mzee Mabundo, pale Songea mpaka wamezeeka hawa wazee. Juzi wananiambia mama hebu tufanyie mpango twende tukamwone Mheshimiwa Waziri Mkuu Dodoma. Miaka zaidi ya 30 wanadai pensheni wako wengi sitaki kusema wote kwa sababu ya muda. Lakini tutanyosheana vidole, tutakosoana lakini tatizo ni utekelezaji na maamuzi sahihi kwa wakati sahihi hilo ndilo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala ambalo limeuma sana mtanisamehe mimi huwa ni mtu wa kusema kile ambacho ninakihisi. Wizara ya Afya Daktari wa kwenda India. Waziri amezungumza humu ndani akasema kwamba Daktari ameteuliwa kwenda India baada ya sisi kufuatilia sana, amepewa *passport* ya kidiplomasia mke wake kapewa pia amechukua *leave without pay* kwa sababu anakwenda, watoto wamesimamishwa shule wanasubiri uhamisho kuondoka, Katibu Mkuu mzoefu aliyekuwepo pale sasa hivi sijui yuko maji walimteua na Kamati. Kila kitu kimefanyika anasubiri fedha kwenye Wizara aindoke na ameshaaga na mizigo amepeleka alikoweka anakuja Katibu Mkuu mwingine kwa sababu anazozijua yeye anasema huyu hafai, hana sifa.

Kwa kweli hapana, inasikitisha. Huyu mtu mnategemea afanye kazi gani na kila kitu kimeshafanyika na nyenzo zote za Serikali zimeshafanya kazi anasema hana sifa za kwenda anasema subiri, ina maana yeye anauwezo wa kuchagua wenye sifa kuliko waliopita. Hatuwezi kuandelea namna hii, ni kwa sababu hakuna *control* ndo kila mtu anafanya anachokitaka. Ndiyo maana jana Mheshimiwa Anne Kilango alisema kila mtu anajifanya msemaji. Hakuna anayejulikana nani anasema. Mama Shellukindo ninaweza kuamka leo nikaanza kuongea kama vile Naibu Spika na Spika amenituma kumbe hapana, hakuna *control* kila mtu anashutumu anavyosema na pale kila mtu anajifanya nipo karibu na nami. Mimi siko karibu na yoyote labda na Mzee William Shellukindo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sina hofu ya kusema. Halafu cha kusikitisha anaenda kuteua mtu ambaye alishakua mtumishi ameacha, ameenda kwenye *NGO*, anaenda kumchukua kwa sababu tu sijui ni wifi au ana unasaba naye anamrudisha na kutoa *force* kwamba lazima kule Muhimbili wamkubali kama mtumishi na jana nimepewa taarifa aliitisha Kamati wakaandaa sifa upya ili ionekane huyu aliyekua amechaguliwa ambaye amekaa kwenye dawati la kupeleka watu nje hafai. Sawa basi huyu Dr. Sawe hafai. *(Makofi)*

Sawa Dr. Sawe hafai, kwanini watumishi wote usiwape uende ukamtoe wifi yako au Ndugu yako huko aliko kwenye *NGO* umpeleke? Mheshimiwa Waziri Mkuu no control no utekelezaji no maamuzi. *That's why* tunafikia hapo tunapofikia. Kwa kweli inasikitisha na mimi ninasema kwa uchungu sana. Je, huu ni utawala bora? Kwa kweli vitu vingine vinauma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli vitu vingine vinauma. Kwa sababu kama hili la Wizara ya Afya nimepeleka mpaka barua na ma-*document* yote mimi Ofisi ya Waziri Mkuu Katibu wake kayapokea. Nimekwenda kumwona Waziri wa Afya, nimewaona Watendaji Wakuu *no answer*. Ukienda huku unaambiwa kule, kule limeenda huku. Lakini ukija kwenye utawala bora, mambo ni *out of control* kabisa. Watu ambao unadhani ni kazi yao ya kusimamia utawala bora ndiyo ambao wanaubomoa *and nobody cares*. Kuna watu ambao na hili ninalijua na nalisema tu kwa wale wasilolijua lakini sitafafanua majina si kazi ya kufafanua mahali hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu ambaye amepewa dhamana tena siyo pengine kwa sifa ni kwa dhamana ya mwenye mamlaka lakini kwa sababu anapeperusha bendera ya Uwaziri au Unaibu Waziri anadiriki kufanya mambo kinyume. Niseme kitu kimoja, sisi Wabunge humu ndani, hatuna Hati Miliki ya Ubunge. Sisi tunafanya kazi kwa dhamana tuliyopewa na wananchi wetu ili tuweze kuwatumikia kwa kipindi cha miaka mitano. Ikifika wanahaki ya kutupa kama tunatosha, kama hatutoshi wanatuacha. Sasa tunapoanza kuona viongozi ambao wangekuwa ndiyo wasimamizi wakuu wanapita na magari yao *NW* au *W* inatisha na wanaingia wanafanya vitu vilevile ambavyo vinapingwa. Unagawa pesa nyumba moja moja na unaitisha vikao bila mamlaka za Mikoa, Wilaya na bila hata Mbunge wa Jimbo hilo kujua. Hatukatai lakini ni busara ndogo tu inahitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu najua ninachokiongea, vizuri kwa sababu nimeshakueleza, vyama vyote vinajua. Lakini huyu mtu anafanya anavyofanya. Mara ya mwisho ametoka pale Jumapili akifanya vitu vya ajabu.

Lakini mimi si kazi yangu kulalamika dhamana yangu ipo kwa wananchi. Hili ni mfano nimetoa kwangu lakini ndiyo yanayoendelea kila mahali, tufuate taratibu. Uchaguzi ni mpaka mwakani. Tumieni akili kupita, mbona watu tulipita wakati tunajua tunafanya nini. Sio lazima kila mtu ajue.

Lakini unakwenda unajitangaza na kwenye ofisi za vyama na nini na huyu ni kiongozi mkuu ambaye anajua hata zile mamlaka pale iwe ni takukuru iwe ni nini haziwezi kumchukulia hatua. Tumekaa tunaangalia, ugonjwa hautaki kupona.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye suala la vitambulisho. Nimeongea na Bwana Kitilya huyu wa *TRA* ananiambia na yeye alikuja na hiyo hoja. Sasa hivi wanaolipa kodi ni wale wafanyakazi sijui laki ngapi. Watu karibu milioni 17 wanaweza wakatoa kodi lakini utawatambuaje? Ni lazima kwa vitambulisho. Nikamwambia sasa wewe umekaa kwanini husemi. Anasema nimeandika, nimesema kila niliposema ugonjwa ule ule hatari *nothing a do*. Matokeo yake tunapoteza kodi ambayo pengine

tusingehitaji fedha za wafadhili. Tunaanza soko huria sasa hivi, tumeingia mikataba na wenzetu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wenzetu nchi nyingine wako *serious* wanatekeleza tutabaki sisi hapa tunalalamika. Tulitoa *grace period* ya miaka mitano, kwingineko miaka kumi kwamba wenzetu walipe kodi lakini sisi hapa tusilipe kodi watupe muda wa kujiandaa na soko letu. Miaka imekwisha Januari tunaanza zero rating nao hivyo hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, Mungu libariki Bunge na Mungu Ibariki Tanzania. (*Makofi*)

**SPIKA:** Suala la vitambulisho Serikali lazima ifanye haraka kwa sababu mambo mengi yanachelewa kwa sababu hiyo tu. Tunaendelea Mheshimiwa Dr. Bilith Mahenge.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE**: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupewa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kuhusu hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini kwanza nianze na kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa kwanza nataka sehemu ya kwanza nitumie nafasi hii kuishukuru Serikali kwa mambo makuu mawili. Kwanza kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Makete, napenda sana kuishukuru sana Serikali, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, *VETA* pamoja na Bodi yake kwa kusikia kilio cha wananchi wa Makete cha Janga la UKIMWI ambalo limeacha watoto 13,000 na zaidi na wale wanaoishi katika mazingira magumu kwa kuwajengea Chuo cha *VETA* Jimbo la Makete.

Nashukuru sana upendo huu ambao umeonyeshwa na Serikali kwa Jimbo la Makete Nashukuru sana kwa upendo huu ambao umeonyeshwa na Serikali ya awamu ya nne. Ninaamini kabisa huu ni msaada endelevu, ni msaada ambao unaweza ukalinganishwa na kwamba kuwapa watoto skills za *VETA* ni sawa na kuwajengea barabara ya dhahabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani yangu ya pili kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Makete ni kuhusu kilio chao cha barabara kusikilizwa. Natoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali hususan Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wizara ya Miundombinu, Watendaji wote pamoja na Wakala wa Barabara baada ya kufanya maamuzi ya kujenga sasa barabara za Makete toka Njombe – Makete mpaka Kikondo kwa kiwango cha lami kilometa tano zile sehemu sugu. Kama mnavyofahamu barabara za Makete sehemu kubwa zote na mara nyingi wakati wa masika hazipitiki. Ujenzi huu umeshaanza mkandarasi ameshaanza kujenga kati ya Tandala na Mang'oto Km 5 na tumepewa Km zingine 30 za kokoto. Kwa niaba ya wananchi wangu naishukuru sana Serikali ya awamu ya nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa pili nataka nijikite kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu na hasa ni ukurasa wa 40, ambapo naomba ninukuu. Anasema "*barabara zetu zikiwa nzuri zitarahisisha mazao mengi ya wakulima kupelekwa kwenye masoko ya ndani na nje na wao kupata bei nzuri na ari ya kuzalisha zaidi. Kumbe ni ukweli*

*usiofichika kwamba miundombinu ndiyo injini ya kukua kwa uchumi na kupunguza umaskini.*" (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inamaana kwamba uwekezaji katika ujenzi wa barabara na hasa za vijijini itakua ni suluhu ya kutatua tatizo la kukua kwa uchumi na vilevile kupunguza umaskini. Lakini tunaona wazi kwamba yapo mahusiano ya moja kwa moja kati ya sekta ya usafirishaji na umaskini na hii inajionyesha na nitaoa baadaye takwimu zangu.

Tatizo kubwa ambalo nataka kuliongelea ni kwamba Serikali yetu imekua ikitenga fedha imeweka kipaumbele kwenye miundombinu toka mwaka 2006/2007 na mwaka huu lakini tunashuhudia kwamba hapa kuna uwekezaji mkubwa kwenye *expenditure* ya barabara lakini matokeo yake au mafanikio yake ni kidogo. Hii ndiyo hoja ya msingi ambayo imenifanya nichangie. Lakini hoja nyingine ni kwamba huu uwekezaji ni kwa namna gani unamkomboa mwananchi ambaye ni mnyonge au ni kwa namna gani Bajeti hii inakua ni *pro-poor*. Hii ndiyo misingi miwili ambayo nataka kuilezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie mtandao wa barabara. Mtandao wa Barabara nchi nzima unafikia karibu Km 80, 000. Lakini ukiangalia hotuba ya Waziri wa TAMISEMI inasema karibu Km 56,000 ziko chini ta TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni sawa sawa na asilimia 70, na hizi zinasimamiwa na TAMISEMI, TAMISEMI ambao sidhani kama wana Wahandisi wa kutosha kama walivyo Wizara ya Miundombinu. Kwa hiyo, hapa kuna matatizo ya mfumo wa usimamiaji wa utekelezaji au ujenzi wa barabara hizi ambazo ni nyingi za kilomita 56,000 ambazo watumiaji wake ni wananchi wanaoishi vijijini, asilimia 80. Na tunaona kwamba katika bajeti ndio hizi barabara zinapewa asilimia 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ninakuja tena kunukuu hotuba ya Waziri Mkuu. Naomba ninukuu: "Matatizo ya kukarabati barabara mra kwa mara yatapungua kama tekinolojia sahihi na viwango vya kitaalam vitafuatwa katika hatua zote za ujenzi wa barabara zetu".

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani tatizo liko hapa kwamba tuna tatizo la kuchagua tekinolojia sahihi ya ujenzi wa barabara hasa hizi za vijijini *(rural roads)*, na hii ni changamoto kwa Wahandisi, hii ni changamoto kwa wanamipango, hii ni changamoto kwa wale wanaosimamia miradi mbali mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni namna gani viwango vya usanifu *(design standards)* vinaweza kupitiwa upya ili kuruhusu tekinolojia ya nguvu kazi *(labour based technology)* ikaweza kutumika na ikaweza kusaidia wananchi wengi. Kwa mfano; tunaona barabara ina kilomita 20, barabara hiyo imepangiwa milioni, mathalani 50, watalaam wetu wanasema kwamba kilomita 2.5 watazijenga kwa kiwango cha kifusi.

Lakini kilomita zilizobaki 17.5 watafanya *light shaping* au *light grading* ambayo inafanywa na greda, nalo linachukua hela nyingi sana. Najiuliza, na baada ya greda

kufanya vile kilomita 17.5 linaacha vumbi ambalo ni kero kwa wananchi kwa sababu hawaweki kifusi na baada ya mvua kufika, ile inakuwa ni matope na barabara inakuwa haipitiki.

Najiuliza, ni kwa nini hela hizi ambazo zingetumika na greda, kwa nini wasipewe wananchi wa maeneo yale, wakatumia hii tekinolojia ya nguvu kazi kutengeneza zile barabara. Kwanza, wangetumia hela kidogo, lakini pili wangefanya kazi ile ile nzuri ambayo ingefanywa na lile greda, na tatu ungekuwa ume-*create* ajira kwa wananchi hao wanaoishi vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, changamo ni kwa Serikali kupitia mfumo wa usimamizi wa barabara hizi za vijijini, kupitia upya mfumo wa utoaji wa fedha hizi zinazokwenda vijini, kwa sababu ukiangalia sasa hivi pale Halmashauri kuna kitengo cha ujenzi, hicho kitengo kiko chini ya Mkurugenizi.

Sasa, endapo Mkurugenzi hana uelewa wa uhandisi, basi kinachofanyika huko sidhani kama kinaweza kuwa ni kizuri. Na ningependa sana kumwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba wahandisi wamezoea kazi ngumu na ni watu ambao hawataki kukaa ofisini, jaribuni kuwaweka Wakurugenzi ambao pia wana elimu ya uhandisi. Mnafaham kwamba tuna Chuo Kikuu cha Sokoine, wanasomesha pale *Agricultural Engineering*, weka angalia mabadiliko yatakavyotokea. Lakini napongeza kwa muono wenu wa kwamba kuwe na Wakurugenzi wa elimu ya kilimo ambao pia watasaidia kusukuma suala zaima la ujenzi katika Wilaya zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe tu tafiti ndogo ambazo zimeonyesha mahusiano ya usafirishaji katika sekta hii ya rural roads. Upo utafiti ambao umefanywa nchi ya Ghana ambao unaonyeshwa kwamba katika barabar ya kilomita 25 wananchi vijijini kule alimia 90 wanatembea kwa miguu, wanabeba bidhaa zao kwa kichwa na wanapeleka sokoni kwa kichwa.

Utafiti kama huo umefanywa Uganda ambako umeonyesha kwamba vijijini aslimia 75 wananchi wanatembea kwa miguu na wanabeba mizigo kwa vichwa kupeleka sehemu mbali mbali, wakati aslimia 22 ndio wanaweza kuwa na matumizi ya baiskeli na asilimia 3 ya matumizi ya magari. Kwa upande wa Makete, asilmia 90 wanatembea kwa miguu, 80 wanabeba mizigo kichwani. Kwa hiyo, unaweza kuona ni namna gani hata mbolea inayopelekwa itawasaidia vipi wananchi kama usafirishaji katika sehemu za vijijini haupo, maana yake anakwenda sokoni kwa kubeba kichwani, anakwenda kupeleka shambani hivyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naenda haraka sasa. Suala zima hapa ni uchaguzi wa teknojia. Inatakiwa teknolojia inayochaguliwa izingatie ufinyu wa Bajeti *(Financial Constrants)*, izingatie *un-employment* tuliyo nayo, idadi kubwa ya watu ambao hawana kazi, izingatie kipato kidogo wanachopata wananchi na izingatie mapendekezo ya Benki ya Dunia ambayo inasema kwamba pale ambapo pato ni chini ya dola 4, basi teknolojia ya *Labour Based* iweze kutumika.

Nataka kupendekeza tekinolojia ya *labour based* (ya nguvu kazi) kwa sababu ianongeza ajira ambayo inaweza ikachukua watu wengi kule vijijini, karibu mara mbili au mara nne, lakini vile vile inapunguza mahitaji ya fedha za kigeni, inaongeza matumizi ya malighafi zetu wenyewe na inakuza uwekezaji ndani ya nchi na inapunguza utegemezi wa vifaa vya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mapandekezo yangu hapa, naiomba Serikali ijitahidi kuona kwamba inaanza kutumia hii nguvu kazi kwa ajili ya ujenzi wa barabara za vijijini ambayo inaweza kuajiri hii aslimia 80 iliyopo. Na kwa kweli mafanikio yamepatikana *South Africa,* wametumia teknolojia hii, imefanikiwa, Cambodia imefanikiwa, Bangladesh na sehemu zingine wamefanikiwa. Bangalesh wamegundua kwamba wakitumia muundo huu, kukua kwa kilimo ni karibu *32 percent* zimeongezeka na *house hold income* ni *33 percent* imeongezeka na maana yake Bajeti hiyo imekuwa ni *pro-poor*.

Kwa hiyo, napendekza Serikali iangalie upya namna ya kusimamia fedha na ujenzi wa barabara vijijini. Waangalie mtindo kama ule, kuwe na *rural road agents*. Lakini napendekeza Serikali iwe na dhamira ya kutumia *labour based technology* na mitaala katika vyuo vya elimu ya juu vianze kufundisha *labour based technology* ili wanafunzi waweze kujua kwa sababu wengi wanaotumia *wrong notion* kwa sababu wamesoma nje, wametumia mashine ambazo ni za kisasa na wao walifanya vile kwa sababu walikuwa wanapunguza tatizo la mishahara iliyokuwa inakua wakati ule Ulaya, ndio maana wakaenda kufanya hivyo. Mheshimiwa Naibu Spika, suala la msingi hapa ni kwamba kila kijiji kiwe na mtandao mzuri wa barabara ambao unaweza kuwarahisishia kufikisha mazao sokoni na kwa utalaam unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni kuhusu umeme Makete. Nataka kuishukuru Serikali kwa kutusaidia kusambaza umeme, mipango inaonyesha katika kata za Mfumbi, kata ya Matamba, Iwawa, kijijini cha Ujuni, Tandala. Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, ombi langu hapa, hii miradi najua *TANESCO* mwaka wa fedha unaanza mwezi Januari, lakini leo hii ni mwezi wa sita, bado hawajaanza hata kusambaza nguzo. Tunawaomba wafanye kazi kwa ari mpya, nguvu mpya, kasi mpya ili hizi fedha zisirudishwe bila kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kunipa nafasi na mimi kutoa yangu machache katika hotuba hii. Kwanza, nashukuru kwa Wizara hii pamoja na Waziri Mkuu kuweza kutupatia shule nyingi za msingi zinazoitwa shule za kata. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, na vile vile nashukuru kwa upande wa kwetu Kusini kwa kupata barabara, japo kuwa haijaisha, lakini tunaamini na sisi tutafaidi lami. Lakini pamoja na kushukuru kuhusu shule, nina machache ya kuzungumzia kuhusu shule za

Kata. Shule tumezipata, wanafunzi walio wengi wanaenda shule, lakini shule hizi zina utata. Licha ya upungufu wa walimu ambao tumekuwa tukiuzungumzia, lakini kuna utata mwingine mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ziaanzishwa hizi shule, tulielezwa kwamba zilianzishwa ili wanafunzi wanaoishi katika kata ile ili wasome. Lakini sasa hivi imekuwa ni kero na mzigo mzito kwa wazazi kwa sababu wanafunzi sasa hawasomi katika kata ambayo imejengwa shule yao. Wanafunzi walio wengi wanatoka wanaenda kusoma kata nyingine ambayo ni tofauti na eneo walilopo, ambapo inakuwa ni gharama kubwa kwa mzazi, anashindwa kumudu mahitaji ya mwanafunzi huyo, umbali unakuwa ni kero kwa mwanafunzi na shule hizo hazina *boading*. Halafu isitoshe, wanafunzi hao inabidi wakae majumbani, yaani wapangiwe vyumba.

Kwa sasa hivi shule za msingi wanafunzi wanamaliza wakiwa na umri mdogo sana, miaka 13 na wengine hadi 12. Unapomtoa mtoto katika shule ya kata ambayo ulikuwa umeijenga ili aweze kusoma pale karibu na mzazi, akaenda kusoma kwenye kata nyingine ambayo inabidi umpangishie chumba, huu umekuwa mzigo mzito kwa wazazi na kwa wanafunzi pia kwa sababu hakuna *supervision* yoyote ile ambayo itamsaidia mwanafunzi huyu kwa udogo wake nani atamwangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule nimesema tumezipata, tunashukuru, lakini imekuwa ni tatizo kubwa, halafu vile vile hata gharama zake zimekuwa kubwa kwa sababu ili ukampangishie kule, sio vile ambavyo tulikusudia kwamba itamwondolea mzigo mzazi labda wa ada na gharama mbali mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa ushauri, ikiwezekana katika kipindi kijacho, wanafunzi wa shule ya msingi wachaguliwe waende shule kwenye kata ile ile ambayo anaishi, wasiende kwenye shule nje ya kata ambayo mwanafunzi huyo anaishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi na mapato. Kama nilivyoeleza hapo awali kwamba sisi katika Mkoa ya Lindi, Mkoa wa Mtwara siyo maskini, tuna rasilimali nyingi za kutosha, tuna vitega uchumi ambavyo haviwezi kukauka kuanzia Januari hadi Desemba. Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, bado katika maeneo haya imekuwa ni vigumu wananchi kupata huduma zinazohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaizuingumzia Halmashauri ya Kilwa. Katika Halmashauri ya Kilwa, tumepata bahati kwamba kuna wawekezaji na wawekezaji wengine ni wa mibono. Hao wawekezaji wa mibono wametoa zaidi ya milioni 800 katika Halmashauri ya Kilwa. Pesa hizi zimegawanywa kiholela holela, hata ukizungumza kwenye kamati, hakuna maelezo ya kutosha. Cha kusikitisha ni kwamba katika maeneo hayo tuna matatizo mbali mbali, mfano ya walimu hawa watarajali ambao wameletwa tangu mwezi wa saba mwaka jana, wameshindwa kupatiwa huduma zinazostahili. Lakini katika maeneo mengine ya Mikoa, tunasikia wenzetu wakiwasaidia walimu hawa kwa kutumia mifuko yao ya Halmashauri. Sisi, katika Halmashauri ya Kilwa pamoja na kwamba tuna uhaba wa walimu, tunahitaji walimu, pesa hizi zimegawiwa kiholela badala ya kuwasaidia hata hawa walimu pia waweze kupata huduma zinazohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine cha kusikitisha ni kwamba katika fedha hizo milioni 800 ambazo zimeletwa pale, zimetengenezea gari la Mkurugenzi kwa shilingi milioni 21, gari ambalo limetembea kwa muda wa siku tatu limeharibika tena. Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni ubadhilifu wa hali ya juu ambao hatuhitaji kuuona. Mimi kama Mpinzani ninavyoongea kule kwetu, ninaonekana kama ni mnoko. Lakini hivi vitu ninaviona na mara nyingi nimekuwa nikienda kwa Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na kumweleza kwamba sisi katika eneo letu, tunao uwezo wa kujiendesha kwa mambo mengi, lakini ubadhilifu kama huu tutashindwa kuuvumilia na tutaendelea kuuongelea katika majukwaa hata kama tutaonekana vyovyote itakavyokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama Mtanzania, kama mtu wa Kilwa, sikubali kuona wananchi wa Kilwa wanateseka na michango, wakiihudumia Serikali wakati Serikali inatakiwa iwahudumie wao kwa michango hii midogo midogo wakati tunajua kwamba kuna pesa ambazo zingeweza kuwaondolea hizo adha za michango midogo midogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalo lingine la kuzungumza, naomba Halmashauri hizi zitupiwe macho. Kuna wakandarasi, kuna wakusanyaji wa mapato ambao wamekuwa wakidhurumu sana. Wakandarasi hawa au wakusanyaji wa mapato wa Halmashauri, nimeishawahi kuleta barua TAMISEMI ya kuhusu mkusanyaji wa mapato mwenye kampuni iitwayo Nongwa ambayo ameiibia Serikali, Halmashauri. Wakati huo nilishindwa kuongea kwa sababu kesi ilikuwa mahakamani.

Lakini ametolewa kiujanja ujanja. Ameingia Halmashauri na kunyofoa stakabadhi za Serikali na hili nilishalizungumza kwamba hili nalizungumza ni la kweli na wakati huo mimi nilikuwa ni mfanyakazi wa Halmashauri hiyo, ninalifahamu. Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI amelijibia kwa barua, lakini Mkurugenzi ameliwekea, hataki kueleza hali halisi ilivyo kutokana na barua iliyotoka TAMISEMI. *(Makofi)*

Sasa nasema hivi, hawa Wakurugenzi ambao wanakaribia kustaafu, kama ni njia mojawapo ya kuweza kuwaweka katika Halmashauri zetu ili kuwaongezea muda ule wa kustaafu, naomba katika Wilaya zetu wasifike. Na kama ni kuwafadhili, basi kuna nafasi za Mheshimiwa Rais mbili zimebaki za Ubunge wapewe Ubunge. Naomba tafadhali, mambo mengi hayaendi kwa sababu hawa viongozi wengine wamekuwa ni wanasiasa kuliko watendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kero ya ardhi. Kero hii ya ardhi ni ya muda mrefu katika kijiji cha Mnazi Mmoja. Mpaka sasa vijiji hivyo vimekuwa ni Mji Mdogo. Wananchi hawa walitoa maeneo yao kwa Serikali kwa maombi. Ikafanywa tathmini ya kwamba watalipwa. Wananchi hawa wanashindwa kuendeleza maeneo yao kwa sababu maeneo hayo yamekuwa ya Serikali sasa, na kulipwa hawajalipwa na hii ni mara ya pili nakuja kulizungumza hapa. Nimeishafuatilia Halmashauri kuelezea, kwa kawaida napenda kuleta jambo ambalo tayari nimelifuatilia katika Halmashauri yangu.

Lakini pamoja na kufuatilia huko, hakuna majibu ya kueleweka kuhusu eneo hilo la wananchi, hivyo nalazimika kulileta hapa ili nione ufumbuzi wake. Naomba Serikali, Wizara ya ardhi, iwaulize watendaji wa ardhi wa Halmashaur ya Kilwa, nini hatima ya wananchi hawa wa kijiji cha Mnazi Mmoja kuhusu ardhi yao ambayo imeishafanyiwa upembuzi na hawajalipwa chochote na hawana ruhusa ya kufanya chochote katika maeneo hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatangaza utawala bora, tunatangaza ukiukwaji wa haki za binadamu. Suala hili kwa Kilwa limekuwa ni kitu cha kawaida. Ukiukaji wa haki za binadamu umezidi. Serikali ilitoa uboreshaji katika Mkoa wa Lindi hasa Wilaya ya Kilwa na wananchi wamezingatia wanajua nini maana ya uboreshaji. Iweje mtu anapohoji mapato ya na matumizi ya kijiji, anaambiwa kwamba yeye ….

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, uboreshaji wa kitu gani? Unasema uboreshaji, ni nini?

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kuna Idara ya Uboreshaji katika Mkoa wa Lindi yaani ile kuwapa wananchi wa Wilaya na katika Vijiji kujua haki zao na jinsi ya kuhoji mapato na matumizi. Kwa hiyo, hiyo hali imeendeshwa katika Mkoa wa Lindi na Wilaya zake. Kwa misingi hiyo, wananchi wanaelewa nini kinachoendelea, wanajua wanapoibiwa, wanajua kinachoenda sawa. Lakini mtu anapohoji wa Kilwa, mapato na matumizi, huchukuliwa hatua na kusingiziwa kesi ambazo hazistahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ukiukwaji wa haki za binadamu umekuwa ni mkubwa katika Mkoa wa Lindi kwa kusingiziwa kesi mbali mbali iwapo mtu ataonyesha tu kwamba ana mwamko wa kuhoji. Naomba hili liangaliwe kwa sababu ninyi wenyewe ndio mmetoa hayo mafunzo na wananchi wanaelewa. Na hii imekuwa ni kero mpaka wanapandikiziwa maaskari. Askari Polisi wanajua kazi zao za kufanya, lakini kwa sababu ya siasa iliyoingia Kilwa Askari hao wamekuwa wakiendeshwa na Vyama vya siasa. Naomba Viongozi wa Vyama vya kwa mujibu wa sheria kuwa Upinzani umeletwa katika Tanzania hususan Mkoa wa Lindi, waache hizo tabia kwa sababu, nilikuwa harakati za kwenda kwa Waziri Mkuu, CCM katika Mkoa wa Lindi inapoteza mwelekeo na inapoteza watu wake kwa sababu ya unyanyasaji wa kuwanyanyasa wananchi. Wanaponyanyasa wananchi hawatambui kwamba nyuma yao kuna watu wa CCM humo humo wanaishi na kuna watu wa Vyama vya Upinzani wanaishi.

Kwa hiyo, nakuomba Waziri Mkuu, imekuwa ni kero kubwa watu wanawekwa ndani, wanafungwa, wanasingiziwa kesi, bila ya sababu yoyote. Na mimi nasema, hapa nasema mara ya mwisho, sikuweza kufika kwako Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu nilikuwa nasubiri labda hali itabadilika. Lakini naona kadri siku zinavyokwenda hali inazidi kuwa mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maelekezo ya ushirikishwaji, ninyi wenyewe Serikali mmetoa kwamba kila mwananchi katika kijiji anatakiwa kushiriki katika mikutano na kuamua mambo yao wenyewe katika kijiji. Kwa Kilwa imekuwa ni tatizo.

Katika kijiji cha Somanga, wananchi waliomba pesa zao kwa mfadhili, walipata fedha za kujenga ofisi ya kijiji. Mkurugenzi anakatalia kuwapa fedha zao wakati wamekaa kwenye mkutano wa kijiji. Hiyo ni haki? Huu ushirikishwaji uko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, maamuzi ya kijiji sio lazima aamue Mkurugenzi. Pesa zile ni za kwao, wameomba wenyewe, hazikutoka katika ofisi ya Mkurugenzi. Kwa nini anawakatalia baada ya mfadhili kuingiza pesa katika eneo lile, anakatalia kutoa? Naomba hili pia nipate jibu na Mkurugenzi aweze kuwaruhusu wananchi hawa waweze kupata pesa zao kwa ajili ya kijiji kwa sababu ni maamuzi ya wengi, sio maamuzi ya Mkurugenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie hilo hilo la ushirikishwaji. Watu wa mibono wametoa pesa katika kijiji cha Migeregere, pesa ambazo zinatakiwa wanakiji wazipangie wenyewe. Mtu mmoja anatoka kwenda kuwanunulia trekta, halafu anawaambia trekta hili ni milioni 75, wananchi wanakataa wanasema sisi hatukuagiza trekta, tuna vipaumbele vyetu.

Haya ni matatizo ninayotaka kukueleza Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwa sababu haya yako chini yako na hivi vijiji kama Serikali za Mitaa zote ziko kwako wewe.

Maana ya ushirikishwaji kama Mkurugenzi, kama kiongozi yeyote hajui maana yake ni hiyo kwamba watu ambao ameamua kitu chao wakiwa wengi kama ni wanakijiji, basi wakubaliwe kufanya kile wanachokihitaji. Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa fursa hii nami niweze kutoa mchango wangu. Kwanza, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uzima mpaka leo hii. Nami pia natoa maoni kwa niaba ya wananchi wa Namtumbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote walio katika Ofisi yake: Mheshimiwa Celina Kombani, Mheshimiwa Phillip Marmon a Naibu Waziri, Mheshimiwa Aggrey Mwanri kwa kuandaa vizuri hotuba zao na kuhusu mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na Makadirio ya Matumizi ya Fedha Ofisi ya Waziri Mkuu na Bunge mwaka 2009/2010. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kuishukuru Serikali kwa ushirikiano mkubwa ninaoupata kutoka kwa Serikali katika kutimiza majukumu yangu ya kuisimamia na kuishauri Serikali ili kutimiza malengo ya wananchi tuliyojiwekea. Hata vitabu vya dini vinatuelekeza na vinasema kwamba kwanza tumshukuru Mwenyezi Mungu na kumtukuza, halafu tunaomba maombi mengine. Kwa mfano, sisi Waislamu tunasema *"bismillah rahiman rahim"*. Kwa tafsiri isiyokuwa rasmi inasema: "Kwa jina la Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na mwenye kuneemesha neema ndogo na kubwa". Kwa wenzangu *Christians*, *I'm stand to be corrected*. Tunasema: "Baba yetu

uliye Mbinguni, jina lako litukuzwe". Pia tunatoa maombi: "Utupatie mkate wetu wa kila siku".

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nitaenda na mtiririko huo wa kushukuru na kuomba hasa kwa kuwa sisi Waswahili tuna usemi usemao kwamba: "Asiyeshukuru kibaba, hata ukimpa gunia hawezi kushukuru". *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua Serikali ya CCM nia njema iliyo nayo katika suala zima la kukabiliana na umaskini kwa kuunga mkono juhudi za wananchi katika mipango ya Bajeti zetu kupitia mipango ya maendeleo katika Halmashauri zetu. Lakini kutokana na ufinyu na rasilimali tuliyonayo katika nchi yetu wa kuweza kukidhi mahitaji yote kwa wakati mmoja inakuwa ni vigumu. Lakini Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) katika kipindi hiki imeweza kusimamia vizuri utekelezaji wake wa Ilani yake ya Chama cha Mapinduzi hasa kwa wananchi wa Jimbo la Namtumbo, Mkoa wa Ruvuma na wananchi wa Tanzania kwa ujumla. Kwa hiyo, sisi wananchi wa Namtumbo hatuna budi kuishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya 2006, katika mchango wangu wakati nachangia hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu kama hii nilisema kwamba sisi Namtumbo katika Tarafa moja ya Sasawala tuna shida ya maji kweli kweli. Kuna baadhi ya maeneo tunakunywa maji katika vimfereji na wanyama kama tembo, simba na fisi.

Lakini, leo Serikali ya CCM iliweza kutusikiliza na kutuletea miradi mbali mbali hususan wa *quick wins* na wakati huo tulikuwa na visima 360 katika watu tuliopo Namtumbo 225,000. Visima 38 vilikuwa vibovu, 47 vilikuwa havitoi maji vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miradi hiyo Serikali iliyotuletea, tumechimba visima 85, tumekarabati visima 87. Kwa hiyo, hatuna budi tuendelee kuishukuru Serikali. Lakini ni vigumu sana kwa mguu kuushukuru mkono unapoutoa mwiba. Naomba nirudie, ni vigumu sana kwa mguu kuushukuru mkono unapoutoa mwiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mdomo unaweza ukausemea mguu. Kwa hiyo, sisi Wabunge wa Chama cha Mapinduzi hatuna budi kuwa mdomo kuisemea Serikali kwa shukurani zetu kwa kazi nzuri inayotufanyia na kwa hatua kubwa tuliyofikia hadi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, siyo kwamba Namtumbo katika maeneo ya maji ndio basi tumemaliza, bado. Bado tuna maeneo tuna shida kubwa sana ya maji hasa katika Makao Makuu ya Wilaya ambayo ni Mji wa Namtumbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu ya maji iliyowekwa Namtumbo miaka 1927/1928 iliyopita, iliwekwa wakati Namtumbo ikiwa ni kijiji, lakini leo ni Makao Makuu ya Wilaya, watu wameongezeka, nyumba za kisasa zinajengwa kwa kasi ya ajabu. Kwa hiyo, tuna matatizo sana ya maji, miundombinu ile haitoshelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali ituweke katika Mpango wa Maji Mjini. Lakini, naishukuru sana Wizara ya Maji na Umwagiliaji, hasa Mheshimiwa Waziri Mwandosya, amaniambia pembeni kwamba mwaka huu wametuweka, wametupa fedha ya kukarabati Mradi wa Maji wa Namtumbo Mjini. Tunaishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendeleza elimu, Serikali pia tunaishukuru. Kwa kushirikiana na wananchi tumejenga shule za sekondari 19 katika Kata 12 na sasa tuna shule za sekondari 28.

Mwaka jana tumeongeza madarasa 83 katika shule 28 tulizokuwa nazo za Sekondari. Shule za msingi madarasa 55 lakini hata hivyo bado tuna matatizo vile vile katika mikondo mipya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali iendelee kutuunga mkono katika suala hili ili tuendeleze mikondo hii ya shule za msingi kwani tuli-*concetrate* sana na shule za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tunachangamoto katika sekta hii ya elimu, tuna upungufu wa Walimu ,tuna mahitaji ya walimu elfu moja na thelathini na tatu na mwaka huu 2009, tuna Walimu mia saba na kumi na nne, kwa hiyo, tuna upungufu wa Walimu mia tatu kumi na tisa.

Mheshimiwa Naibu Spika katika kipindi hiki cha miaka mitatu, tulipata Walimu themanini na saba na katika hao Walimu kuna Walimu hamsini na saba waliostaafu kwa mujibu wa sheria na kuna wengine wamefariki. Kwa hiyo, utakuta katika ile idadi ya Walimu themanini na saba tuliopata katika kipindi hiki cha miaka mitatu, tuna ongezeko la Walimu thelathini tu. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali katika sekta hii ya elimu, chondechonde, mwaka huu mtupe Walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta ya afya, tunashukuru tena Serikali imetusaidia sana, tumeshirikiana na wananchi, tumejenga zahanati mpya tisa, tumekarabati zahanati saba, vituo vinne vya afya lakini bado tunalia na upatikaji hafifu wa dawa .

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri katika swali langu la tarehe kumi na mbili, *I am ready to be correct,* alisema kwamba Serikali inapitia mapitio ya uongezaji wa dawa kila mwaka, lakini ukitazama mapitio haya katika kipindi hiki cha miaka mitatu, kwa ujumla wake ni shilingi elfu themanini tu ndizo zilizoongezwa kwa zahanati kwa mwezi, kwani 2006 -2007, zilikuwa ni laki tatu na kumi kwa mwezi katika zahanati, mwaka 2007- 2008 ni laki tatu na hamsini elfu na mwaka 2008-2009 ni laki tatu na tisini kwa zahati kwa mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni ongezeko dogo sana ukilinganisha na watu ambao 74.3 % wanaoishi vijijini sawa na watu milioni thelathini, mia mbili arobaini na nane elfu, mia tano na saba. Hawa wote ndio wanaotegemea dawa na kule vijijini

hakuna maduka ya dawa. Kwa hiyo, dawa zinapochelewa kufika au zinapofika zikiwa kiasi kidogo, basi linakuwa ni tatizo sana kwa wananchi wetu dawa zinapokwisha na kwa hasa wale wanaotoa huduma ya afya saa nyingine wanashindwa kukaa katika zahati kwa sasababu wanashindwa jinsi gani ya kumhudumia mtu bila ya kuwa na dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudi katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, *bullet* ya ishirini, alim-*quote* Mheshimiwa Rais kwenye hotuba yake ya tarehe 10 Juni 2009, mjini Dodoma alisema:-

*"Dunia inakabiliwa na msukosuko wa masoko ya fedha ulioanzia huko Marekani na nchi za Ulaya, Asia na kuenea sehemu zingine duniani. Msukosuko huu, umesababisha uchumi wa dunia kuporomoka. Athari kubwa ya msukosuko huo kwa nchi zinazoendelea zinatarajiwa kujitokeza zaidi mwaka 2009"* mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze Serikali kwa hatua nzuri sana iliyochukua ya kuweza ku-*rescue* uchumi wetu pia. Tunaambiwa uchumi wetu mkubwa haujaungana moja kwa moja na uchumi wa dunia lakini athari zake zipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama athari zilizojitokeza katika maeneo ya watani zangu Wasukuma kwenye pamba kule na Wanyamwezi na Serikali ku-*intervene* kuona ni jinsi gani ya kuokoa, hii inasababishwa kama nilivyosema awali, uchumi huu wa dunia angalau hautugusi moja kwa moja lakini huu ni mtambuka. Leo hii Marekani ile *jobless* ime-*raise* kutoka 8.1% mpaka 8.5% toka *recession* ianze, watu waliopoteza kazi Marekani, ni milioni tano na laki moja na kwa kipindi hiki cha miezi mitatu mpaka mitano, watu waliopoteza kazi Marekani ni milioni tatu nukta tatu .

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hawa ndio wanaonunua nguo matokeo yake, kitu cha kwanza wanaahirisha vile vitu visivyo vya msingi kama nguo na nguo, *material* yake ni pamba. Kwa hiyo, tutegemee kabisa kwamba mwaka huu wa 2009 lazima tufunge vibwebwe kwelikweli kuhakikisha kwamba tunaendelea kuwaokoa wakulima hawa wa pamba, bei itaendelea kuwa ya chini kwa sababu ununuzi wa pamba utakuwa mdogo hasa kwa hao wenzetu wanautumia na wanaovaa nguo sana kwa sababu hawana kazi, hawawezi kutumia vitu visivyokuwa vya msingi, watatizama kwanza chakula na vitu vingine .

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumembiwa kuwa Japan vilevile uchumi wao pia umeyumba sana umekuwa *heated* na hii *World Economic Crisis*, tumeambiwa kwamba sasa hivi kuna *data* zina-*speculate* kwamba Wajapan nao wanatafuta *oversies Investment* kwa sababu baadhi ya viwanda vyao vinafungwa kutokana na uchumi kuwa mbaya na wao pia sasa hivi wameshindwa ku-*export, export revenue* ya kwao imeshuka sana na hao ndio wanunuzi wakubwa pia wa pamba. Kwa hiyo, tulione hili katika mtazamo huo na tuishukuru sana Serikali kwa hatua kubwa iliyochukuwa na tuendelee kulitazama kwa karibu sana eneo hili la uchumi katika uchumi wetu Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina mengi zaidi ya kuishukuru Serikali na kuipongeza pia katika utaratibu mpya wa vocha ya mbolea. Kuna wenzangu wamezungumzia vizuri

sana, kuna makosa madogo madogo yaliyotokea lakini jambo lolote jipya haliwezi kukosa makosa. Kwa hiyo, makosa yale yaliyokuwa yametamkwa na Waheshimiwa Wabunge, tunaomba sana Serikali wayaangalie kwa karibu ili tuweze kuyarekebisha. Lakini ni utaratibu mzuri ambao umemhakikishia mkulima kupata mbolea yake kwa gharama nafuu na iliyokusudiwa tofauti na ilivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishukuru Serikali katika miradi yake ya umwagiliaji. Tunachoiomba Serikali katika hii miradi ya umwagiliaji ambayo imewekwa katika majimbo yetu, sasa tuwe na wataalam wa kutosha wa kuwa karibu kusimamia miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi*)

**NAIBU SPIKA**: Ahsante sasa. Sasa namwita Mheshimiwa Grace Kiwelu, atafuatiwa na Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Manyinyi halafu Mheshimiwa Cynthia Ngoye.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kusema machache katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wenzangu, kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Nchi, TAMISEMI, Dada yangu Celina Kombani na Kaka yangu Aggrey Mwanri pamoja na watendaji wote wa ofisi hiyo ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina tatizo na kilichoandikwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tatizo langu liko kwa watendaji ambao watatakiwa kutimiza yale yaliyomo katika kitabu hiki kwa sababu tunapitisha pesa nyingi sana ambazo tunategemea zitakwenda kuleta maendeleo kwa wananchi wetu lakini watendaji wanaopelekewa pesa hizi, wote si waadilifu maana tumekuta matatizo mengi sana ya ubadhirifu wa pesa ambazo tunazipitisha katika bajeti zetu ndani ya Bunge hili. Kwa hiyo, tunawaomba wale ndugu zetu watendaji wakuu watakaosimamaia pesa hizi, waweze kuzisimamia vizuri ili wanachi waweze kupata yale maisha bora waliyoahidiwa. Baada ya kuyasema hayo, naomba sasa niende kwenye tatizo la ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia katika vyombo vya habari na tumeona hata baadhi ya Watanzania wameweza kupoteza maisha yao kutokana na vurugu za kugombea ardhi. Hivi karibuni, tuliona kule Kilosa wafugaji na wakulima wamepigana na wengine kupoteza maisha kwa sababu ya tatizo la ardhi, lakini tatizo hili chanzo kikubwa ni kutokuwa na uadilifu kwa wale viongozi wanaosimamia sehemu hizi. Watendaji hawa wanasababishia wananchi kupoteza maisha yao kwa sababu hawajui wajibu wao katika kazi. Wengi wanafanya kazi zao kwa sababu ya kupata kitu kidogo (rushwa) na ndio maana wananchi wengi maskini wanapoteza haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumeona ametenga maeneo ya wafugaji na wakulima. Tunaomba sasa maeneo haya yaweze kuwekewa miundombinu kwa sababu nchi ya Tanzania wako wakulima, wafugaji na wafanyakazi wote tunategemeana, hatutaki kuona watu wanapoteza maisha, wakulima na wafugaji, tunawahitaji wote. Kwa hiyo, tunaomba maeneo haya yaliyotengewa wafugaji waweze kupata maeneo yao na wakulima wapewe maeneo yao ili wote tuweze kuishi kama Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni, Kamati yetu ya *LAAC* ilifanya ziara katika Manispaa za jiji la Dar es salaam. Katika Manispaa ya Temeke, tulipotembelea Wilaya hiyo, tulikuta matatizo makubwa sana la ardhi katika Jimbo la Kigamboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo lile wameanza kupima viwanja lakini kuna shule moja ya Sekondari ya Kibada ambayo imejengwa kwa nguvu za wananchi, tunajua kabisa jinsi wananachi walivyoshiriki kujenga shule hizi za Kata, mradi huu umekuta shule ile tayari imeshajengwa, cha ajabu wamepima viwanja lakini baadhi ya nusu ya majengo wanaambiwa wabomoe kwa sababu sio kiwanja cha shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaiomba Serikali maana tulikutana na Diwani wa Kata ile pamoja na Mkuu wa Shule ile na baadhi ya uongozi wa shule, wamesema wameshatoa malalamiko kwa Wizara husika ambayo ndio inasimamia mradi huo wa viwanja, tunaomba wasimamie jambo hili tusije tukagombanisha wananchi kwa sababu wametoa nguvu zao kubwa sana na shule ile imejengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine yule atakayepewa kiwanja karibu na shule ile, hatakuwa na amani kuwa watakuwa na mahusiano bora kati ya shule na huyo atakayepewa kiwanja. Tunataka Watanzania wote tuishi kwa amani, tunaomba suala hili Waziri anayehusika afuatilie ili wale wananchi waliojenga shule ile waweze kupata manufaa na watoto wao waweze kusoma, maana sehemu ya kiwanja kilichogawiwa tayari kuna majengo, vyoo na kuna maeneo ya watoto wetu kucheza yaani viwanja vya michezo. Nitashangaa kuona shule ambayo haina viwanja wakati tunasema Serikali imeweka changamoto kubwa sana kwenye michezo. Kwa hiyo, tunaomba sana lisimamiwe vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tatizo hili la ardhi limeendelea zaidi kujitokeza kwa kigezo cha wale matajiri wachache wanaokuja kwa njia ya uwekezaji ambao wanawanyanyasa sana wananchi maskini. Sijawahi kuona hata siku moja tajiri anayenyang'anywa ardhi lakini wale maskini ambao wamekaa katika maeneo hayo zaidi ya miaka ishirini ndio wanaonyag'anywa ardhi! Tunaomba sana wawekezaji hawa wanaokuja kupitia kwa watendaji ambao hawana maadili, wanasababisha wananchi, wanawanyag'anya ardhi yao kwa sababu ya kupewa rushwa, watu hawa wachukuliwe hatua kali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maskini wana haki ya kuishi katika nchi hii kwa sababu hawakupenda kuwa maskini, nao wangependa kuwa matajiri ili nao waweze kuwekeza lakini kutokana na hali ngumu, wamekuwa kwenye hali hiyo. Kwa hiyo,

tunaomba sana Waziri anayehusika na hawa Watendaji ambao wanakiuka taratibu na kuwanyima haki maskini hawa kwa kuwanyang'anya viwanja kwa kuwa yule ni mwekezaji amekuja kuwekeza, tunaomba sana wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine tumelikuta katika Manispaa ya Kinondoni juu ya suala hili la ardhi, wamekuwa wakigawa maeneo ya wazi ambayo watoto wetu wangeweza kucheza! Tunaomba sana suala hili lisimamiwe katika Manispaa ya Kinondoni, watoto wetu wamekuwa wakicheza barabarani na inahatarishia sana maisha yao. Tunaomba Manispaa hasa za Dar es Salaam, wale wahusika wote wa mipango miji, wasimamiwe na wakumbushwe wajibu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende katika tatizo lingine, katika Halmashauri zetu, tumekuta tatizo kubwa sana la Halmashauri zetu kushindwa kesi. Halmashauri zetu zimekuwa zikiingia hasara kubwa sana, aidha kuwalipa wale ambao wamewashtaki waliokuwa wanafanya nao biashara au wafanyakazi ambao waliziibia Halmashauri hizo na kupelekwa Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na kutokuwa na uadilifu mzuri kwa wale Wanasheria ambao wako katika zile Halmashauri. Wamekuwa wakiungana na wale walioshtakiwa na Halmashauri kwa ahadi ya kupewa kitu kidogo na wamekuwa hawaudhurii Mahakamani na matokeo yake Mahakama inatoa hukumu. Halmashauri zetu nyingi zinashindwa na kuliingizia Taifa na wananchi wa Halmashauri ile hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwomba Waziri wa TAMISEMI, afuatilie suala hili na wale Wanasheria wote watakaogundulika wanashirikiana na wale walioshtakiwa na Halmashauri kwa ahadi ya kupewa kitu kidogo, wachukuliwe hatua. Hatutaweza kuvumilia kuona wananchi wetu wanakosa maendeleo kwa sababu ya uzembe wa watu wachache, wanaojali maslahi yao na kuwasahau Watanzania wale ambao ndio wamewezesha kupata nafasi ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza hayo, katika Halmashauri zetu, naomba sasa niende kwenye Daftari la Kudumu la Wapigakura. Tunajua daftari hili lilichukua pesa nyingi sana na tulitegemea lingeweza kuondoa matatizo yale yote ambayo yalitukumba kabla hatujawa na daftari hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tulikuwa na uchaguzi mdogo kule Busanda na mimi nilikuwa kule, nilishuhudia baadhi ya Watanzania ambao walikosa haki yao ya kupiga kura. Wananchi hao walikuwa na shahada lakini majina na picha zao katika daftari hayakuwemo. Ninapenda kujua ni kwa nini majina ya wananchi wale hayakuwemo na kwa nini wananchi hao wanakoseshwa haki ya kupiga kura na kuchagua kiongozi wanayemtaka?

**WABUNGE FULANI:** Wa chama gani?

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kujua walikuwa ni wa chama gani kwa sababu wajibu wangu mimi ni kumsemea kila Mtanzania.

Ninapenda niambiwe ni tatizo gani lilitokea wananchi wakakosa haki yao hiyo ya msingi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakwenda kwenye chaguzi za Serikali za Mitaa, tumeambiwa kwamba wataandikishwa upya. Mimi ninapenda kujua ni kwa nini daftari lile ambalo lilitumia pesa nyingi za walipa kodi wa nchi hii, lisitumike hilo hilo badala ya kuingia tena kwenye zoezi jipya ambalo nina hakika, litatumia tena gharama kubwa kuandikisha tena Watanzania kupiga kura uchaguzi wa Serikali za Mitaa? Ninaomba nipewe ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye huduma za uzazi kwa akina mama na watoto. Tatizo hili bado ni kubwa sana kule vjijini, vijijini kule hatuna vituo vya afya na kama vipo ni vichache, hosptali nazo ni chache, akina mama kule wanapata matatizo sana ya kujifungua, akina mama wanapoteza maisha, watoto wanakufa, tunaomba sana Wizara inayohusika iharakishe kupeleka huduma hizi kule vijijini. Huku mijini tatizo hili limepungua kwa kiasi fulani kwa sababu walioko huku mijini, wana uwezo, wanaweza kwenda hospitali za watu binafsi lakini kule vijijini, kutokana na umasikini walionao, bado kuna tatizo kubwa sana katika uzazi na huduma kwa akina mama wajawazito.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu uwekezaji, nimesoma katika Kitabu cha Hali ya Uchumi, nimeona nchi zilizowekeza katika nchi yetu na ninawapongeza lakini nina tatizo moja na ndugu zetu kutoka China. Naomba nieleweke sio kwamba siwapendi lakini uingiaji wa ndugu zetu hawa kutoka China umekuwa ni mkubwa sana, wamejaa mitaani na biasahara wanazozifanya Watanzania wangewezeshwa, wangeweza kuzifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara wanazofanya, wamefungua migahawa na kuuza maua. Biashara hizi, ninaamini Watanzania wana uwezo wa kuzifanya. Wale waliobahatika kupewa ajira katika migahawa hii ya Wachina, wanapata mateso makubwa, mishahara wanayopewa ni midogo. Tunataka sana wawekezaji katika nchi yetu lakini tunataka wawekezaji watakaokuja kuwekeza kwa kufungua viwanda ili tuweze kuwapatia vijana wetu ajira na tuweze kuongeza pato katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wawekezaji wanaokuja kwa mlango wa nyuma kufanya biashara ambazo vijana wetu wa Kitanzania wangeweza kuzifanya hawa hatutakubaliana nao. Tunaomba kabisa Wizara inayohusika, wafuatilie na wajue wameingia kwa uhalali au lah! Kwa sababu tunajua kabisa iko miradi ambayo wanaruhusiwa kuingia na idadi ya watu (wataalam) wanaoruhusiwa kuingia nao, lakini watu hawa wamejaa mitaani, wamekodisha nyumba na wako wengi sana na tumeona kwenye vyombo vya habari wamefungua viwanda vidogovidogo katika nyumba zao walizopanga na matokeo yake wanatuletea bidhaa ambazo hazina viwango hasa madawa. Tunaomba sana usimamizi katika hili ufuatwe ili tuweze kuhakikisha kwamba katika nchi yetu tunapata wawekezaji wenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee utendaji kazi katika ofisi zetu. Jana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha alijibu hapa kwamba kama tunataka kuondoa

umaskini lazima tubadilike. Napenda kuungana naye kwa sababu katika ofisi zetu za Serikali au katika Halmashauri zetu, wafanyakazi wamefanya ofisi zile kuwa ni vijiwe, wamefanya ni maeneo ya kunywea chai, kusoma magazeti, kuongea mambo yao ambayo hayahusiani na kazi zao za kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli tunataka kuleta maendeleo na kuondoa umaskini, sisi sote tunatakiwa sasa kubadilika tuweze kuleta maendeleo katika nchi yetu. Unaweza kwenda kwenye ofisi ukaambiwa mtu huyo ametoka, ukakaa pale zaidi ya masaa mawili, mtu huyo hajarudi kumbe amekwenda kufanya kazi zake binafsi, utakachokikuta pale ni koti, au pochi zimetundikwa wakitegemea ukiliona, utategemea anatarudi muda mfupi ujao. Tunaomba sana wafanyakazi walioko Serikalini na katika Serikali za Mitaa watimize wajibu wao ili tuweze kuleta maendeleo kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiwelu nakushukuru. Sasa nitamwita Mheshimiwa Shally Raymond, atafuatiwa na Mheshimiwa Manyinyi na Mheshimiwa Cynthia Ngoye ajiandae na Dr Chrisant Mzindakaya na Godfrey Zambi wawe *standbay*.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa fursa hii ya kipekee kabisa. Pia namshukuru Mungu kwa kunipa uhai ili niweze tena kuzungumza hapa kuhusu matatizo yanayotusibu kweli kule kwetu Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba pia kuwashukuru wanawake wa Kilimanjaro kwa kunichagua niweze kuwazungumzia huku Bungeni. Nitakuwa sijaitendea haki nafsi yangu, kama sitawashukuru Wabunge wenzangu walionichagua kwa kura za ndio kuwa katika Baraza la *APRM* wakati nikiwa safarini Ghana. Nawashukuru sana Wabunge wenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo, naomba nitoe pongezi kwa Waziri Mkuu na wote wale ambao wamehusika katika kuiandaa hotuba hii nzuri ambayo kwa hakika, inaonekana inatekelezeka. Kabla sijasahau, niunge mkono hoja hii japo nitakuwa na machache ambayo nitataka ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanzia pale katika ukurasa wa tatu, katika kukwamua uchumi wetu. Badhi ya mambo ambayo tumeelezwa pale ni pamoja na kufanya kilimo sasa kiwe endelevu na cha kisasa ambacho tunaweza kukwamua nchi yetu na uchumi wa wananchi wetu. Mimi mwenyewe naamini kabisa kwamba kilimo hiki kinaweza kuendelezwa katika makundi matatu ambayo ninaweza nikayafafanua kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wale wanaohusika na pembejeo za kilimo na zana za kilimo, wakulima na pia kuna Serikali. Katika wakulima hao, kuna wakulima wakubwa, wakulima wa kati na wale wadogo, wanaoniumiza kichwa mimi ni wale wakulima wadogo ambao ndio hapo tutawakuta wale akinamama wa kijijini, akina

mama wasio na uwezo na akina mama pia ambao kilimo kwao ni kawaida au ni hali ya maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimanjaro kunalimwa kahawa, ndizi, na mazao mengine. Miaka nenda rudi, watu wamekuwa wakipata chakula kwa kulima ndizi na mazao kama ya mahindi lakini zao kuu la kupata fedha ni kahawa na hilo linaitwa zao dume yaani ni zao la baba. Miaka ya hivi karibuni, zao hilo limepauka na pia tumeelezwa kwamba katika mtikisiko huu unaoendelea, soko la zao hilo limeharibika, hivyo basi unakuta baba atamuegemea mama kupata chochote kutoka kwenye ndizi, lakini ndizi hizi zinazolimwa Kilimanjaro katika maeneo kama Siha, Rombo, Moshi vijijini, Same, halijapata soko la uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la ndizi sasa hivi, linaliwa kote na wengi wanapenda ndizi kwa sababu wanga wake ni wa chini hata wale ambao wanasumbuliwa na maradhi ya *diabetes* wanapendelea ndizi. Mkulima wa ndizi pale kijijini, mkungu wake atatuuza kutokana na ambavyo ataambiwa bei pale sokoni kijijini lakini ukifika sokoni Kariakoo mkungu ule unapata bei kubwa sana. Shida yangu ni kwamba ni jinsi gani sasa zao hili la ndizi litapata kipimo kinachoeleweka katika soko la mkulima pale kijijini? Tutokane sasa na kuhesabu vichane, tutokane sasa na kuhesabu ndizi moja moja, tuingie katika kupima ndizi kwa kilo, mkulima ajue kwamba akikuuzia ndizi yake, itapata bei nzuri. Naomba kuuliza je, katika hizi hela ambazo zinaelekezwa kwenye kilimo, wakulima wa ndizi kama wa pale Kilimanjaro, watakuwa wamefikiriwa katika kuboresha namna ya kupima ndizi zao ili waweze kupata bei nzuri popote na pia wawe na uhakika wa kupata fedha kila wanapokuwa na mazao mazuri? Nitaomba wakati hoja hii inahitimishwa, nipatiwe jibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo, nizungumzie sasa maeneo ambayo yamekwenda mbali na kuweza kubuni mradi kama kiwanda. Nichukue fursa hii kumpongeza sana Mbunge wa Same Mashariki, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kwa kubuni, kuelekeza na kujenga kiwanda cha tangawizi. Nilipata nafasi kutembelea kiwanda hicho na kabla sijaendelea nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu alifika kuona na kuweka jiwe la msingi katika kiwanda hicho. Wakulima wa kule Same wanangojea kwa hamu sana na shauku kubwa kujua katika bajeti hii wametengewa kiasi gani ili waweze kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha tangawizi. Wakulima wale wamengoja miaka mingi, wamekuwa wakilima tangawizi kienyeji na tangawizi ni zao zuri, wengi wanapenda kwenye chai na viungo vingine, lakini hawakuweza kupata mtu wa kuwaongoza, ametokea sasa Mbunge wao, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, amefanya ubunifu, kiwanda kimejengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda hicho kimeshafikia hatua kubwa lakini ni jinsi gani sasa kitawezeshwa ili kianze kufanya kazi? Maeneo yote hayo niliyotaja ya Wilaya zote zilizoko Mkoani Kilimanjaro, hawatafaidika sana na matrekta ambayo yamezungumziwa hasa wale wa nyanda za juu. Wale wa tambarare, nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa sababu wanalima mahindi na eneo lile lina ruhusu kupita matrekta na hata hizo *power tillers* lakini wale wa kule Milimani wao daima watalima tu

kwa jembe la mkono kwa sababu ya msongano wa kahawa , ndizi, miti, vyote hivyo viko katika mteremko wa Mlima Kilimanjaro na Milima ya Upareni .

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwa hakika baada ya kipindi kirefu cha mvua na ukiangalia *slope* ya milima hiyo, ardhi ile imechujuka. Ardhi haina rutuba, watu wale hawajazoea wala hawajahi kutumia mbolea za chumvichumnvi na mbole za kisasa kwa sababu siyo aina waliyokuwa nayo, wao wanatumia mbolea ya samadi, tatizo linakuja sasa namna ya kupata samadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ndani, tunapozungumzia ufugaji, mara nyingi inazungumziwa mifugo ile inayofugwa nje ambayo inapelekwa kwenye malisho, lakini eneo hili mifugo yake ni mifugo ya ndani, yaani ni *zero grazing* na mifugo mingi ni ile ambayo sasa imeshakuwa na mbegu ambazo hazitoi tena maziwa kwa wingi, yaani wakipata ndama siyo wale ndama wa kisasa. Naiomba Serikali katika bajeti hii, iangalie namna ya kupata ndama wa kisasa ambao wataendeleza mifugo itakayoweza kuleta tija kwa wakulima hao wa eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba wengi wa wanawake wa Kilimanjaro wanashauku kubwa kuweza kuendeleza kilimo chao lakini elimu yao ni duni, pamoja na nia nzuri ya kuweza kuleta programu tofauti katika maeneo hayo, kabla ya kuleta programu hizo waweze kupatiwa mafunzo. Mara nyingi tatizo limekuwa hawahudhurii vikao vya kuibua miradi na wanadhani labda vikao ni kwa ajili ya akina baba na siyo akina mama. Tuchukue hatua mahsusi kabisa kuwaelimisha watu hawa, Serikali ikishirikiana na Wabunge hususani Wabunge wa Viti Maalum tuweze kutoa elimu kwa wanawake hawa wajue kwamba kuhudhuria vikao ni muhimu ili waweze kuibua miradi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie kuhusu kilimo chetu hapa nchini na pia uwezo wa wale wasomi wetu katika fani hiyo. Tunawasomi wengi sana katika fani ya kilimo lakini nikiangalia ni jinsi gani tunaweza tukapeleka usomi wao katika kilimo, naona kwamba haviendi sambamba. Naomba Serikali wakati wanahitimisha, watuambie, tunao wasomi wangapi katika *level* ya Digrii ama *Masters* na Diploma ambao wanafika mpaka *level* ya kijijini kutoa elimu kwa wakulima? Mara nyingi hapa tumekuwa tukinung'unika na kulalamika kwamba Maofisa Ugani. Sawa Maofisa Ugani watakuwepo na huenda pia hawatoshelezi lakini hawa waliopo juu, wasomi waliobobea, wanasaidiaje kufanya nchi hii ijikwamue katika kilimo hiki duni na hasa kwa kauli mbiu ya KILIMO KWANZA, inapiga hatua na pia inaleta mabadiliko yatakayoonekana wakati huu tunapotaka kuona kwamba tumeweza? Itakuwa ni jambo jema kama tutaweza kutumia wasomi hao na pia tukaweza kuwapa motisha vijana wetu. Vijana wetu wa sasa wameona kwamba kilimo siyo jambo muhimu la kufanya, lakini kama wasomi hao wanaweza wakasaidia, nadhani wote tunaweza tukawa wakulima wazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, amezungumzia kwamba viongozi wote ingefaa wawe wakulima wazuri na waonyeshe mfano, lakini mimi naona ninatatizo kwamba viongozi wetu tulionao siyo wengi ambao

wamefanikiwa au wamebahatika kuwa na mashamba. Wengi wamezaliwa katika maeneo ambayo mashamba ni ya kurithi na labda mashamba hayo sasa hakuna tena kitu zimebakia *plot* za nyumba tu. Naomba Serikali sasa ione kwamba ni muhimu kuchukua hatua mahsusi kutoa maeneo ya mashamba kwa viongozi wao, wakiwemo Wakuu wa Mikoa, Waheshimiwa Wabunge, Madiwani, wote wapate mashamba mahali ambapo wanaweza kufanya kilimo ambacho sasa kitakuwa kilimo cha mfano, kilimo ambacho kitatoa ajira, kilimo ambacho kitawafanya na wao wakati wakifikia ku-*retire*, waweze kuona kuwa waliitumikia Serikali na wakapata mashamba na wakaweza kuonyesha mfano wa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wakati wanapofanya majumuisho, tupate mwanga hata wale ambao hatuna mashamba nikiwemo mimi, nijue labda shamba langu lipo Morogoro, awamu hii ya Wabunge shamba liko wapi. Ninasema Morogoro kwa sababu ni Mkoa mzuri sana na ni karibu na Dodoma, kwa hiyo Mbunge unaweza ukapitia pale ukalima na ukarejea Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa sijawatendea haki wale walionituma kuipongeza Serikali kwa hatua ambayo Mheshimiwa Rais amechukua kuweza kuzikwamua benki ambazo zilikuwa zimetoa mikopo kwa wakulima, ikiwemo *CRDB* ambayo wananchi wengi ni wanahisa hapa Tanzania. Hali ilipobadilika wananchi wengi sana walinyong'onyea na wakaona kwamba hakuna haja ya kuwa na hisa tena lakini baada ya Rais kusema kwamba Benki zilizokuwa zimetoa mikopo kwa wakulima zinaweza sasa kuendelea kutoa mikopo na Serikali itaangalia itakuwaje. Nawapongeza sana wanahisa hao na waendelee kununua hisa *CRDB* na pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa hatua aliyochukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nikushukuru, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Pia nampongeza kwa hotuba yake nzuri pamoja na Waziri wake wa TAMISEMI, Mheshimiwa Celina Kombani na Naibu wake pamoja na Serikali nzima, kwa kazi nzuri wanaooendelea kuifanya.

Mheshimiwa Spika, binafsi napenda kuendela kuipongeza Serikali kwa sababu ninapokumbuka mwaka 2005 wakati tunaomba ridhaa, yapo mambo ya kimsingi ambayo tuliyowaahidi wananchi wetu kupitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi, leo ninayofuraha kusema kwamba asilimia kubwa ya yale mambo ambayo tuliyaahidi, yameendelea kutekelezeka. Tulikuwa na tatizo kubwa la barabara zetu, naishukuru Serikali imeendelea kutupatia fedha japo kidogo kidogo walau barabara zangu za Musoma Mjini zinaendelea kuwa za lami. Tulikuwa na tatizo kubwa upande wa afya, leo Hospitali yetu ya Mkoa inajengwa vizuri sana, lakini na zahanati zetu zinaendelea kujengwa. Kulikuwa na tatizo kubwa upande wa elimu lakini leo kila mtoto wa Musoma anayefaulu anaenda Sekondari. Kwa hiyo, kazi kubwa tuliyonayo ni kuhakikisha tunaendelea kuboresha zile huduma ili ziendelee kuwa nzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalo tatizo kidogo kwenye upande wa maji. Katika Jimbo langu, wapo wananchi wanaishi kilomita moja kutoka mahali yalipo maji ya ziwa Victoria lakini bado wanatatizo hilo! Lakini kwa kuwa Waziri wa Maji, naye ni Kaka yangu na tunazungumza vizuri na kwa ahadi zilizopo, ni imani yangu kwamba kufikia mwaka kesho tatizo hili nalo tutakuwa tumesogea mbele sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, anisaidie tatizo moja kubwa ambalo liko katika Mji wangu wa Musoma na katika Mkoa wa Mara kwa ujumla. Tatizo kubwa la Mkoa wetu wa Mara na hasa Mji wangu wa Musoma, pamoja na watu kufurahia hizi huduma zote zinazopatikana lakini hali ya uchumi si nzuri hata kidogo, hali ya uchumi si nzuri kwa maana watu wengi hawana ajira na hili limechangiwa na tatizo moja kubwa, Musoma tumekuwa tukitegemea sana viwanda vya samaki. Hivi leo ninavyozungumza, nadhani kama kimebaki hai ni kiwanda kimoja kama si viwili ambavyo navyo vinaenda kwa kusuasua na vingine vyote vimefungwa. Licha ya viwanda hivyo vya samaki, kipo kiwanda kikubwa kabisa cha nguo cha *MUTEX*. Kiwanda hiki kimekuwa kikiajiri watumishi wengi na watu wengi wamekuwa wakitegemea kiwanda hiki kwa ajili ya ajira yao binafsi pamoja na familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri Mkuu wakati akijibu, atuambie na awaambie wananchi wa Musoma, atawasaidiaje kuhakikisha kwamba kiwanda hicho cha nguo kinafufuka tena? Kiwanda hicho kiliuzwa kwa mtu mmoja na baada ya kuwa kimeuzwa hakuna kilichoendelea, inawezekana dalili ni kukifunga ili vile viwanda vyake vingine viendele. Kwa hiyo, ninapenda atuambie, atatusaidiaje watu wa Mara na watu wa Musoma katika hili tatizo la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nami nitoe mchango wangu katika sekta ya kilimo. Nami nakubaliana kabisa kwamba sasa hivi wote tunazungumza lugha moja ya kilimo kwanza, lakini lugha hii ya kilimo tumeendelea sasa yapata miaka mingi kwamba siasa ni kilimo, kilimo ni uti wa mgongo na haya yote tumeyazungumza kwa sababu ya kuanza kuangalia ni kwa kiasi gani tunaamini kilimo kinaweza kikatusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakubali kwamba kwa namna jinsi Watanzania tulivyo wengi na kwa namna tulivyo na maeneo mengi, makubwa na mazuri ya kilimo, ninaamini, ni kilimo pekee ndicho kinaweza kutoa ajira kubwa na nyingi katika nchi yetu, lakini ni kilimo vilevile ndicho kinachoweza kuinua kipato cha Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba safari hii fedha za kilimo zitoke kwenye kilimo na kama hilo tutakubaliana yapo mambo ya msingi ambayo ni lazima tuyafanye kuhakikisha kwamba tunaboresha kilimo. Nasema hivi kwa sababu mimi pia ni mkulima mdogo mdogo kwa hiyo ni vitu ambavyo navizungumza kwa sababu nina uzoefu na ninavielewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ukienda kijiji chochote kile, maeneo yapo mengi lakini ni kazi kubwa sana kupata ardhi kwa ajili ya kulima na hii ni kwa sababu tu ya ukiritimba uliopo kule, maeneo yapo lakini hakujawa na mpango mahsusi kwa yule anayehitaji ardhi ili apewe ardhi. Kwa hiyo, ninaomba Serikali isimamie jambo hilo kwamba vijiji vitenge maeneo na kuyatoa kwa wale walioko tayari kulima na wale wanaochukua muda mrefu bila kulima, wanyang'anywe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hatua ya pili ni nini kifanyike baada ya hayo maeneo kutengwa, tuwe na makundi mawili ya wakulima, wawepo wakulima ambao wana mitaji ya kawaida na wale ambao wana uwezo wa kwenda benki, wakakopa pia wawe na kundi lao, lakini wawepo wakulima ambao wao kukitokea na mtikisiko kidogo, ama ukame kidogo, Serikali inabidi igharamie kupeleka kule chakula. Kukiishakuwa na makundi mawili, Serikali ishughulike na hili kundi la hawa wananchi wa kawaida ambao kipato chao ni kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namna ya kushughulika nao ni kwamba tuwe na utaratibu wa aina mbili, utaratibu wa kwanza ni labda ule wa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tarafa mpaka kule chini, wao pamoja na shughuli zao zingine lakini wajikite zaidi katika kusimamia kilimo. Kama watajikita zaidi katika kusimamia kilimo, Manispaa na *Councils* washughulike na huduma za jamii, Kadri watakavyoendelea kujikita kwenye kilimo waainishe maeneo labda mfano Mkoa wa Mara yapo maeneo mazuri kama ya mto Mara, mto Suguti na kule Bugwema, ambayo yanafikia ekari mia tano na kuendelea, wale wananchi wanaozunguka maeneo hayo, wapewe maeneo hayo kama ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inachoweza kufanya ni kitu kidogo tu, badala ya kusubiri wawapelekee wananchi wale chakula, kama ni ekari elfu moja, Serikali ifanye kazi ya kutoa tenda zilimwe, zikishalimwa, kazi zote zitakazofanyika kwa mikono, wale wananchi wa eneo hilo, kupitia ushirika wao, wazifanye ikiwa ni pamoja na kupanda, palizi na kuvuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunadhani kwamba wale watu kadri watakavyounda ule ushirika wao, sisi tutakuwa tumewapelekea ile miundombinu ya kuwalimia kwa mara ya kwanza, lakini mara ya pili tuhakikishe badala ya kusema labda namna ya upelekaji wa maji kule kwa ajili ya umwagiliaji katika kipindi cha muda mfupi, tunachoweza kufanya ni kitu rahisi tu, ni suala la kutangaza nani, kama hawa Wachina ambao kila siku wanakuja humu, wanatafuta shughuli za kufanya, wao wafanye kazi ya kuvuta maji na kumwagilia katika mpango ambao tutakuwa tumewekeana nao wa makubaliano kwamba hizi hekta 1000 mtamwagilia katika kipindi cha miezi sita ya mavuno kwa shilingi ngapi. Kwa hiyo, kati ya wale wananchi kila mmoja akipata hekta moja moja pale utajikuta tumehudumia siyo chini ya kaya mia tano hadi 1000 na watu sasa wataweza kuwa na uhakika wa kuvuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wetu wengi wanalima lakini hawana uhakika wa kuvuna kwa sababu baada ya kipindi kifupi jua linaingia na kile chakula kinapotea. Kwa hiyo, tunadhani kwamba, kwa kuanzia kwa utaratibu huo, hasa kwenye

haya mazao ya chakula maana sisi kule tukilima mpunga na mahindi tayari tatizo letu litakuwa limeisha. Niseme tu kwamba kama ni suala la soko, masoko yako wazi. Leo ukiangalia hizi nchi zote zinazotuzunguka Kenya, Uganda, Kongo, kila leo zinahitaji chakula. Kwa hiyo tukisimamia vizuri hiki kilimo watu wetu wengi na asilimia kubwa ya Watanzania wataweza kupata ajira, lakini vilevile na sisi wenyewe tunaweza kuinua uchumi wa nchi yetu kuliko hivi sasa ambapo tunategemea pamba lakini pamba unakuta gharama za mkulima anatumia shilingi mia sita badala yake anauza pamba kwa shilingi mia tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru sana na tunaipongeza Serikali kwa kazi kubwa na kwa zile fedha zilizotoka kwa ajili ya wajasiriamali. Lakini fedha hizo, kwa kuwa zilitoka kwa mara ya kwanza, zimeshindwa kuwa na *impact* kubwa kwa sababu zifuatazo; Watanzania wengi bado walikuwa hawana elimu ya ujasiriamali, wengi wao hawakuzitumia vizuri na wengi wao wamechukua mikopo lakini hiyo mikopo wameshindwa kuirudisha. Ninaomba Serikali isikate tamaa kwa kuona kwamba zoezi hili halikwenda vizuri. Serikali iendelee kutoa zaidi elimu ya ujasiriamali, iendelee kufufua ofisi zetu za ushirika, elimu ya ushirika itolewe na fedha zaidi zitengwe kwa ajili ya wajasiriamali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa watu kama wa Musoma Mjini ambao leo hawana viwanda na eneo la karibu kwa ajili ya kilimo basi ni fedha hizi za ujasiriamali peke yake ndizo zitakazowawezesha kuzungusha ili waendelee kupata riziki ya siku hadi siku. Kwa hiyo, tunadhani kwa sababu sikuona sana kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ilivyoonesha kwa mwaka jana, kwa hiyo inawezekana Serikali ikasitasita kidogo lakini mimi niombe tu kwamba tunadhani bado Serikali inaweza ikafanya kazi nzuri sana kama itapeleka Maofisa Usharika kule na wakaendelea kutoa elimu nzuri kwa watu wetu. Baada ya kutoa elimu nzuri, basi na usimamizi madhubuti uwepo kuhakikisha kwamba yule ambaye mtaji wake anaweza kufanya biashara ndogo basi asaidiwe kulingana na uwezo wake. Kwa kufanya hivyo, utakuwa umetusaidia sana watu wa Musoma lakini vilevile na katika maeneo mengine ya mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, naomba kuzungumzia barabara ya Musoma – Nata - Mugumu kuelekea Loliondo mpaka Mto wa Mbu. Barabara ile, tulishasema ikipewa tu fedha za kutosha, maana wengine wanaomba fedha kwa ajili ya barabara kwa kiwango cha lami, sisi tunachoomba ni fedha kidogo ili barabara ile iweze kupitika, maana nilishasema hapa Bungeni kwamba barabara ile ni tofauti na tunavyozunguka Singida kuja Mwanza, barabara ile ni kama nusu ya ule mzunguko, kwa hiyo ule mfumuko wa bei ulioko katika Mkoa wa Mara, unasababishwa na barabara ile kuwa ndefu, ndiyo maana tukaomba pamoja na mpango uliopo wa muda mrefu wa kuitengeneza katika kiwango cha lami. Hebu basi tupate fedha za kutosha kwa ajili ya kuiwezesha barabara ile iweze kupitika na tunadhani kwamba ikiweza kupitika, basi itakuwa rahisi zaidi watu wetu kupata bidhaa kutoka Dar es Salaam, Arusha na Tanga ambazo ni pamoja na sementi, sukari, ngano na kusababisha mfumuko wa bei kuliko ambavyo sasa watu wetu wanazunguka umbali mrefu sana na ndiyo sababu za huo mfumuko wa bei kuendelea kuwepo hasa katika Mkoa wetu wa Mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kadri anavyofanya kazi pamoja na ofisi yako pamoja na Serikali yako lakini basi nikuombe uyaangalie baadhi ya haya maeneo ambayo tumeyasema na tunadhani kwamba kwa kufanya hivyo utakuwa umetusaidia sisi wananchi wa Musoma lakini vile vile wananchi wa Mara kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Cynthia Ngoye, atafuatiwa na Mheshimiwa Dokta Chrisant Mzindakaya na Mheshimiwa Godfrey Zambi ajiandaye.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi ambayo umenipa ili na mimi niweze kuchangia machache kuhusu hotuba ya Waziri Mkuu lakini vilevile kuhusu hotuba au maelezo aliyotoa Waziri wa Nchi, TAMISEMI, Mheshimiwa Celina Kombani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda moja kwa moja, kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa asilimia mia. Vile vile, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kazi kubwa anayoifanya katika kutatua kero za wananchi hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono vipaumbele ambavyo vimetolewa na Serikali katika bajeti ya mwaka huu 2009/2010 na elimu ambayo inapewa nafasi ya kwanza, ninakubaliana nayo kwa sababu bila elimu katika nchi zetu zinazoendelea, hatuwezi kwenda mahali popote. Kwa hiyo, suala la elimu halina ubishi, kila mtu anafahamu kwamba elimu ni lazima tuipe nafasi ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa elimu, TAMISEMI imepewa jukumu ya kusimamia elimu ya sekondari lakini vile vile elimu ya msingi, nakubaliana kwa sababu shule nyingi ziko katika maeneo ya Serikali za Mitaa lakini bado Wizara ya Elimu nayo inaendelea kushika nafasi ya kusimamia sera na mambo mengine. Ninaloomba hapa ni mchanganuo au maandishi ambayo yataonesha nini TAMISEMI wanawajibika kufanya na nini Wizara ya Elimu wanawajibika kufanya katika kuendesha elimu ya sekondari na elimu ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalisema hivyo kwa sababu kwa mfano, zoezi lililofanyika la kulipa madeni ya Walimu, utaona katika kuhakiki, Wizara ya Elimu ndiyo iliyohusika lakini ilipofika katika kulipa TAMISEMI, ndio waliohusika. Kwa hiyo, hapo unachanganyikiwa kuona sasa ni nani mwenye wajibu. Kwa hiyo, ni vizuri basi Serikali ikatuandikia sisi Wabunge ili tusiwe tunababaika, kwa sababu wakati mwingine unaenda Wizara ya Elimu, unaeleza tatizo lako, unaambiwa hili halituhusu, linahusu TAMISEMI, hii si kazi kubwa, naomba watusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri inayoendelea hivi sasa katika kuboresha elimu, naona kuna machache ambayo ni lazima tuyaangalie na bado ni changamoto kubwa sana, kwanza ni suala la maabara katika shule za sekondari. Tatizo la upungufu wa maabara katika shule za sekondari, bado ni kubwa sana. Matatizo ya kutokuwa na maabara, yamechangia sana kwa wanafunzi wengi kutopenda masomo ya sayansi, lakini vilevile imechangia sana baadaye kutokuwa na Walimu wa kutosha wa masomo ya sayansi katika shule zetu, hapa tunatoa mzunguko wa elimu ambao hautaweza kutupeleka mbele katika karne hii ya sasa ya sayansi na teknolojia. Naomba tulitazame suala hili la ujenzi wa maabara kwa uzito mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutoa ushauri. Huko Mikoani, kuna maabara ambazo zilijengwa huko nyuma kati ya miaka ya 2000 na 2008, hii ilitokana na uhamasishaji wa Wizara yenyewe ya Elimu kuwataka wazazi waweze kujenga maabara, lakini maabara hizo hazijakamilika. Ukitaka kuliita jengo ni maabara maana yake ni lile jengo lililokamilika, likawekewa na vifaa vyake tayari kwa kutumika lakini siyo *structure* peke yake, kwa hiyo naomba maabara hizo zikamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natoka Mkoa wa Mbeya, katika siku za hivi karibuni, nimeshatembelea shule moja ya Ndalambo Wilaya ya Mbozi, shule ya Kambasegele, Kisiba, Rufilio, hizo zipo Wilaya ya Rungwe. Shule hizi zina maabara za zamani, matokeo yake Walimu kwa kukosa madarasa sasa ndimo wanamopeleka wanafunzi wasomee humo. Ninaomba Serikali itoe maelekezo maalumu kwa Mikoa kuangalia kwanza zile maabara ambazo hazijakamilika, wazikamilishe kwanza. Pili, ninaomba sasa tuongeze chachu katika kuongeza maabara mpya. Mkoa wa Mbeya kwa mwaka huu wa 2009/2010, wanapewa kujenga maabara nne tu kwa Mkoa mzima, sasa tutafika lini? Ninaomba sana hatua ya kuongeza kiwango cha ujenzi wa maabara iongezeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa nizungumzie suala la mikopo ya wanawake. Ari ya wanawake wa Tanzania katika kufanya maendeleo yao, ni kubwa sana na hasa wanawake wa Mkoa wa Mbeya. Mimi nina ushahidi, pamoja na ari kubwa sana ya kujiletea maendeleo yao lakini kikwazo kikubwa sana ni mitaji na mikopo ambayo haipatikani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika fedha ya kuwezesha wananchi ambayo inajulikana kwamba ni Mamilioni ya JK, wote tunaelewa kwamba wanawake wengi sana na hasa wanawake wa vijijini, hawakupewa nafasi ya kupata ile mikopo. Kwa hiyo, bado akina mama wanatuuliza sisi wawakilishi wao kwamba mnafanya nini? Mbona hii mikopo tunaisikia tu hewani iko wapi?

Nilifikiri wakati Serikali inaendelea kuangalia huo utaratibu unaozungumzwa wa kuteua mabenki yanayoweza kufika kwa wananchi kwa urahisi, tuangalie hii *ten percent* ambayo Halmashauri za Wilaya zilipaswa kuchangia, je, kweli Halmashauri zote zinachangia hiyo *ten percent* kwa wanawake na vijana mpaka sasa? Je, Halmashauri ngapi zimechangia na fedha kiasi gani zimechangwa na wanawake wangapi wamefaidika na mikopo hiyo? Napenda kulifahamu hilo kwa sababu linatukwaza hasa tunapokwenda

vijijini tunaulizwa na wanasema mbona Halmashauri yetu ipo hapo lakini hatuoni ambacho tunakipata? Wanaweza wakabajeti hata milioni kumi, milioni ishirini inasaidia nini? Haisaidii kwa kiwango kikubwa cha wanawake tulionao hasa katika Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie suala lingine ambalo ni la upangaji wa miji yetu hapa nchini. Ukuaji wa miji yetu hivi sasa naona kwamba unanipa matatizo. Ni kweli, ni lazima tujenge majengo ya kisasa, lakini majengo hayo ni lazima yaendane na upangaji wa miji hiyo. Nichukue mfano wa Dar es Salaam peke yake. Dar es Salaam hivi sasa, kwa sasa tunaopita Dar es Salaam, kila mtu hapa anapita Dar es Salaam, ndiyo maana nasema nitazungumzia Dar es Salaam kwa sababu ni kwetu sisi wote, wote tunapita Dar es Salaam. Dar es Salaam, umeibuka mtindo wa kujenga magorofa, sawa, magorofa yanajengwa, lakini, nina amini magorofa yale hayana mpangilio hata kidogo. Kwa mfano, chukua Kariakoo, yanajengwa kwenye maeneo ambayo yalipangwa huko nyuma kuwekwa majengo ya kawaida yenye watu wasiozidi 6 au 7, leo yanajengwa magorofa marefu sana ambayo mengi ni mahoteli yanayoweka watu zaidi ya 50 mpaka 100, lakini miundombinu ya maji taka ni ile ile ya zamani. Umeme ni ule ule wa zamani, sasa hapo maana yake nini? Wakati wa mafuriko, hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nenda *Oysterbay*, sehemu ambayo ilipangwa vizuri sana katika nchi hii; ilikuwa ni *Oysterbay* lakini sasa, baada ya nyumba zile kuuzwa, utaona majengo marefu, hapa bar, hapa nyumba ya kuishi, hivi kweli ni mipango miji wameruhusu hali hiyo? Mimi sidhani. Kwa hiyo, ninaomba sana hali hiyo itatupeleka pabaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mango, hili liko pia katika mji wa Dar es Salaam na majiji mengine ya Mwanza na Mbeya, kuna mabango makubwa kabisa ambayo yamewekwa huku na huku, mimi najua kweli ni chanzo cha biashara, nakubaliana nalo, lakini, mabango yale yawekwe kwa utaratibu, sio kuweka barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kuuliza swali hapa siku moja kuhusu mabango hayo hayo. Naibu Waziri akajibu vizuri tu na akatoa maelekezo, kupitia Bunge hili kwamba kuanzia sasa naziagiza Halmashauri zote ziweke utaratibu wa kuweka mabango vizuri. Alipojibu swali lile tangu wakati ule, naona ni kama alihamasisha zaidi, mabango yanawekwa hovyo hovyo kabisa, hasa Dar es Salam. Kwa hiyo, naomba sana suala hili liangaliwe upya. Tunakubaliana kwamba ni chanzo cha mapato, lakini lazima awepo mtu wakusimamia la sivyo Dar es Salaam tutakosa hata hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumze kidogo tu kuhusu majengo ya zamani, ya kihistoria. Mimi naona ni chanzo kizuri sana cha utalii. Maeneo mengi sana hapa duniani wanatumia maeneo yale kama vyanzo vya utalii. Lakini sisi jengo la zamani lolote lile tunaliona kwamba ni uchafu, tunabomoa, jamani! Hasa sisi huku Bara. Nawasifu sana wenzetu Zanzibar, wana sehemu inaitwa Mji Mkongwe. Ule ni mji mzuri kabisa unapofanya ukarabati unapopewa eneo hilo, unakarabati kwa muundo ule ule ili jengo hili liendelee kwa vizazi vijavyo. Watajua hapa waliuzwa watumwa, hapa ilikuwa hivi na kadhalika. Lakini sisi leo tunafikiri maendeleo maana yake ni kubomoa majengo

yote na kuweka majengo mapya. Si sahihi hata kidogo, kwa sababu tumetembea nchi nyingi Ulaya, Marekani, kila mahali majengo ya zamani wameyatunza kwa ajili ya utalii. Watalii wanakuja wanatembelea majengo wanaangalia. Sio wote wanaopenda wanyama. Hata mimi ninapenda niende Zanzibar nitembelee Mji mkongwe. Watalii wengi wanakuja Zanzibar kuona Mji Mkongwe. Kwa hiyo, tujisahihishe katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kabisa, Ofisi ya Waziri ya Mkuu, italizingatia masuala yote niliyoyazungumzia hapa mwisho yanaweza yakatuletea matatizo hapo baadaye na hasa lile la kuzingatia ujenzi ulio na utaratibu. Kwa sababu bila miji yetu kusimamiwa wakati wa masika itafurika, itakuwa uchafu mtupu na hivyo haitaleta sura nzuri ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, naunga mkono hoja hii ya Waziri Mkuu, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hotuba hii ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia wote kuwepo hapa, nina hakika na kutokana na sala zetu, tunawatumikia Watanzania. Natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri, wote tumeshuhudia yeye anavyoshirikiana na sisi Wabunge, ni kiongozi mwenye kujaa hekima na upendo na kujali wenzake, tunamwomba aendelee na moyo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kutumia nafasi hii, kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ni kiongozi ambaye ameijengea nchi yetu heshima kubwa katika jamii ya kimataifa. Wote tunashuhudia alivyo mvumilivu, mtu aliyejaa roho kubwa na upendo kwa wananchi. Muda wote niliopata nafasi ya kukaa na kuzungumza naye, nimeshuhudia jinsi Rais wetu alivyo na *vision* na upendo wa kuongoza nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili, nataka niseme kwamba sisi Rukwa na nasema Rukwa *with confidence*, mimi ndiyo mzee wa Siasa wa Mkoa wa Rukwa, mimi na Wabunge wenzangu Mheshimiwa Kimiti, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, tumekwishamaliza kutembelea Mkoa wote wa Rukwa na kueleza mafanikio ya Ilani ya CCM na haya nitakayosema, tumetumwa na wananchi wa Rukwa. Mwaka 2005, Mkoa wa Rukwa, Rais Kikwete alipata asilimia 92 ya kura, Mkoa wetu ulikuwa miongoni mwa Mikoa mitatu iliyoongoza. Katika Jimbo langu, Rais alipata asilimia 94.30, Jimbo langu lilikuwa la kwanza kwa Majimbo yote ya Mkoa wa Rukwa na kwenye Kata yangu alipata asilimia 99 na mimi 98. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge wenye upendo na nawajua wote ni wenye upendo wa nchi yao na Wapinzani pia, kwamba kwa Mkoa wa Rukwa, kura za Rais Kikwete hazitashuka mwaka kesho. Nimetumwa nije niseme rasmi kwamba tunaomba agombee mwaka kesho na tutampa kura nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Wabunge hasa wa CCM tumekuja Bungeni kwa Ilani, kwa hiyo mtu akisema Serikali yetu haina *vision*, haina mwelekeo hajui, maana tumekuja kwa Ilani hii hapa na haiwezekani Rais au Waziri fulani akazuka na *vision* yake na mwelekeo wake, sisi tuna Ilani yetu na tuna *vision* ya 2025, hiyo ndiyo tunayoifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hayo, nafurahi kusema nimeshuhudia na hata kwa maelezo hapa, mimi nimefurahi sana Waheshimiwa Wabunge, tuliingia kwa mafiga matatu, Rais, Mbunge na Diwani, sasa hapa tulipo tushangilie mafanikio. Sisi tumefanya kazi nzuri na Serikali yetu na kabla kipindi hiki cha Bunge hakijaisha, Waheshimiwa nawaahidini mimi nitafanya utafiti wa mafanikio yote mliyofanya ili nije niyaseme tena hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimekuwa Mbunge muda mrefu lakini nikitazama kwa dhati kabisa Wabunge wa kipindi hiki cha Awamu ya Nne, mmefanya kazi kubwa kuliko miaka yote na lazima mjivune kwa kufanya kazi nzuri. Nimeshuhudia jinsi Wabunge mnavyoeleza, mama Kilango alikuwa anasema jana, Mheshimiwa Kawawa amesema, Mheshimiwa Beatrice alikuwa anasema jinsi alivyofanikiwa katika jimbo, sasa wananchi wangependa kusikia hayo, nafurahi na Wapinzani kwa sababu hata Mheshimiwa Dr. Slaa yale aliyoeleza kwamba amefanikiwa kule kwake, huo wote ni utekelezaji wa Ilani ya CCM maana yeye hana Serikali. Kwa hiyo, tunapongezana wote pamoja na Wapinzani kama Mheshimiwa Dr. Slaa, kusaidia kutekeleza Ilani ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina majirani hapa, Mheshimiwa Ndugai ana kata 14 wamejenga sekondari 26, asilimia zaidi ya 100, nina kijana hapa George, ana kata 9 amejenga sekondari 12 na Wabunge wengi hapa mmefanya kazi kubwa. Wabunge wa Viti Maalum wamefanya kazi nzuri ya historia, wametuunga mkono sisi Wabunge wa Majimbo kuleta ufanisi. Kwa hiyo, CCM ina haki ya kurudi tena madarakani, kwa sababu Wabunge wake wametekeleza Ilani vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baada ya hayo, ninapenda kusema yafuatayo, kwanza, niseme ya Rukwa kidogo na Jimbo langu, nisije nikasahau. Jimboni kwangu tuna kata kumi na tatu, tumejenga sekondari 17. Tulipoingia wakati ule watoto waliokuwa wanaingia sekondari walikuwa 1521 sasa tuna wanafunzi 4700, ongezeko ni kubwa sana. Jimboni kwangu, tulikuwa na vituo vya afya 3, sasa tunavyo 6. Jimbo langu lina vijiji 96, asilimia 90 vina zahanati na vijiji vyote vina shule za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwa upande wa elimu kitaifa, tumesikia wote hapa, Rais wetu alipoingia madarakani alisema kwamba tutajitahidi elimu. Elimu kwanza na kweli imepewa kipaombele na wote tumeona katika bajeti. Tumepata taarifa hapa kwamba tulikuwa na *university* 8, sasa tunazo 11 za Serikali na katika hizo Waheshimiwa Wabunge, *university* ya Dodoma, itakuwa miongoni mwa *university* za kujivunia Afrika na hatutamsahau Rais wetu na chama chetu katika jambo hili. Haya ni mambo makubwa ya kujivunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaambieni mimi ni Mwanasaikolojia, digri yangu ya heshima ni ya *Humanities*. Binaadamu ana kasoro moja; hata kwa watu wa dini wanayo kasoro hii, ukimfanyia mema 10, ukimkosea 1, anafuta yote 9. Sasa mtu anapokuja hapa, akaning'inia na jambo la chuki, anasahau mengine mema, huyo naye anakuwa hana dini. Kwa mfano, Mudhihir alisema jana hapa na mimi ngoja nikusomeeni Biblia inasema nini. Tuangalie hekima za Yoshua, Yoshua 5:15 inasema:-

*"Usiwe fisadi, katika jambo kubwa wala dogo, wala usipate kuwa adui badala ya rafiki".*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, watu wanakuja hapa wanapima ufisadi kwa pesa, hawapimi ufisadi kwa roho zao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inaendelea inasema hivi, Yoshua 6:4 inasema:-

"roho ya ufisadi, itamuaribu yeye aliye nayo, hata kumfanya mzaha kwa adui zake".

Kwa hiyo, wewe kama unakuja hapa, siasa umeikuta, kazi yako ni kuandama wenzako wakati na wewe ni fisadi, huna roho ya utu na kwa nini wewe umezaliwa na roho ya kuandama watu wengine tu? Hivi wewe ukichunguzwa si fisadi hata kwa maisha yako mwenyewe? Unataka tuseme, maana wote kila siku tunasoma dini ati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona tuwekane sawa hapa. Rukwa, mimi nilikuwa ndio mwenye shida, Rukwa, Jimbo langu lina watu wengi na ndio tunatoa chakula kingi zaidi katika Mkoa wa Rukwa, kwenye Jimbo langu naishukuru Serikali, kwamba imetumia zaidi ya biloni 4 kutengeneza barabara, ambayo ilikuwa ikitusumbua kwa miaka yote ya kutoka Kijiamatundu, naungana na Mheshimiwa Mbunge wa Mbozi na sasa barabara imefungiliwa na wananchi wamenituma kuja kuishukuru Serikali. Sasa tutaungana na wenzetu wa Mbozi maana ilikuwa wakati wa msimu, miaka mitano iliyopita, gunia moja la mpunga shilingi elfu tano leo hivi natoka Jimboni kuwashukuru wananchi na kuwasomea utekelezaji wa Ilani, gunia limefika 35,000, kwa sababu ya uzuri wa barabara. Kwa hiyo, tuna haki ya kuipongeza Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Rukwa katika kipindi hiki cha Awamu hii ya Nne, ulitengewa shilingi bilioni 14 za kutengeneza barabara za Mkoa wa Rukwa. Wabunge wote tunaishukulu Serikali yetu na nina furahi sasa Waheshimiwa, kutoa taarifa hapa, kwamba Mkoa wa Rukwa utatengenezewa kuanzia mwaka huu na mwaka kesho, barabara za lami zifuatazo:-

Kwanza, kutoka Tunduma mpaka Sumbawanga, inaanza Disemba na Januari.

Pili, kutoka Sumbawanga kwenda Mpanda, kilomita 150 inaanza Agosti mwaka huu, barabara ya lami.

Tatu, kutoka Sumbawanga kwenda Matai Kasanga na tutakuwa na Bandari kubwa ya kufanya biashara nchini, inaanza Agosti mwaka huu. Serikali nzuri itoke wapi? Kwa Mungu?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo!

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Si ndio ilikotoka hii? Hii ni Serikali ya Mungu, inajali watu wake. Kwa hiyo, nimeona niseme hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo, wote mnajua mimi ugonjwa wangu ni kilimo. Nataka niipongeze Serikali kwamba sasa imeipa kipaumbele kilimo. Nina ushauri ufuatao, labda kabla sijatoa ushauri huo, nataka niwajulishe Waheshimiwa Wabunge, kwamba Mkoa wa Rukwa kwa mwaka huu, tutavuna tani 1,600,000 za chakula na tutakuwa na ziada, kwa sababu sisi wenyewe tutaitaji kutumia tani laki tatu tu mpaka laki nne. Kwa hiyo, tutakuwa na ziada ya chakula, mahindi, mpunga na maharage; tani 1,200,000, utakuwa ni mchango kwa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana, kama Rais alivyokuwa akisema, sisi hivi sasa, karibu zaidi ya tani 40,000 zinatolewa Sumbawanga kupelekwa katika Mikoa mingine yenye njaa, juhudi hii, tumeifanya sisi wenyewe bila msaada wa Serikali kwa sababu ukitanguliza ombaomba, unaondokewa akili ya kujitegemea. Tulipopata Mkoa, niliwaambia wenzangu hatuna mjomba, hata Serikalini hakuna mjomba, Mjomba ni raia wako aliyekuchagua na kukupa uongozi. Kwa hiyo, tulijipanga wenyewe viongozi wa Rukwa, tukaamua tuanze na kilimo na leo tuna sifa ya kweli. Katika hili, Waheshimiwa, mbaya kujivuna lakini niseme kweli tu, mimi mwaka jana nilichangia gunia za mahindi na ngano, 5000 na mwaka huu, nitachangia gunia 6000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mmoja ya wakulima bora katika Mkoa ule, wala silimi kwa kubabaisha na hii ni sifa yangu tu; lazima mtu uwe na cha kujivunia kimoja katika maisha yako. Mimi ninajivuna kuwa mkulima mzuri, wala sihitaji mtu kunisifu maana ndivyo ilivyo. Ndiyo, sihitaji, maana kuna watu wana roho mbaya, ukifanya vizuri tabu, ukifanya hovyo tabu na hawa wanatoka katika kundi la watu wasio thubutu, kutokuthubutu kunakufanya usipate lawama. Wewe ni mzuri kila siku, hata lawama hizi anazopata Rais Mkapa, ni za kishetani tu; zinatokana na ushetani sio utu. Hivi kweli Mkapa miaka 10 alikaa anacheza tu?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengelee ya pili.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Aah ni ya pili?

**NAIBU SPIKA:** Ndio!

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Ni ya kwanza Mheshimiwa!

**NAIBU SPIKA:** Ni ya pili**.**

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Aaaah! Naunga mkono hoja kama ni ya pili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mambo ya kishetani na ya kinyama, anajua Mungu. Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Godfrey Zambi na Mheshimiwa Mwanne Mchemba ajiandae.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu ambayo aliwasilisha jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba, ukizungumza baada ya wazee wetu kama Mheshimiwa Mzindakaya, unaweza ukakuta huna cha kuzungumza sana. Lakini na mimi naomba nianze kwa kuishukuru sana Serikali, kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na timu yake kwa jinsi ambavyo wamesimamia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa umahiri mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri na lazima tukiri kwamba yale mengi tuliyoahidi kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, yametekelezwa kwa kiwango kikubwa sana. Mzee wangu, mzee Mzindakaya hapa ametoa takwimu nyingi kwa Mkoa wa Rukwa, lakini mimi naomba tu niseme kwamba kwa Wilaya ya Mbozi, tumetekeleza mengi tuliyoahidi kwa zaidi ya asilimia 80 mpaka sasa. Nina hakika mpaka tunakwenda kwenye uchaguzi mwaka kesho, tutakuwa na mengi sana ya kujivunia na hakika mengine tutakuwa tumeyapita kwa zaidi ya asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia, mafanikio haya yametokana na mshikamano mkubwa kati ya uwongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, pamoja na wananchi wenyewe wa Wilaya ya Mbozi ambao wamekuwa wakiiunga sana mkono Serikali yao katika maendeleo katika sekta mbalimbali. Mimi naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza sana sana wananchi wa Wilaya Mbozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunapopongeza maendeleo yanayoendelea katika nchi hii, wapo wasomi wanaotubeza kwamba kwa sababu tumeona uchaguzi, ndiyo sababu tunapongeza yanayoendelea katika nchi hii, si kweli. Nadhani na wasomi katika nchi hii na wenyewe wana upungufu sana kwa sababu, kila lililo jema, wao wanabeza, kila lililo jema wanabeza, hatuwezi kwenda hivyo! Yale mazuri, lazima tuseme haya mazuri, yale yenye upungufu, lazima tuseme pia haya yana upungufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze na suala zima la kilimo, Mheshimiwa Mzee Mzindakaya amesema ni mzee wa kilimo, mimi natoka kwenye familia ya kikulima na mimi najifunzafunza kulima. Inawezekana pia nikaja kuwa mkulima kama Mzee Mzindakaya huko mbele, Mungu akinijalia kuwa hai. Mwalimu Nyerere amewahi kusema hivi, naomba nimnukuu:-

*“kwa sababu ya umuhimu wa kilimo katika maendeleo yetu, ungeweza kudhani kwamba kilimo pamoja na mahitaji yake kingekuwa na rejea katika mipango yetu yote badala yake kilimo hakijapewa msukumo unao stahili, kimechukuliwa kama jambo lingine lolote. Katika nchi, hatujaweka umuhimu unaostahili katika kilimo, kilimo kimepuuzwa, kama kila sekta inafanya inavyotaka katika kilimo, basi wakati sasa umefika wa kukomesha tabia hii ya kukipuuza kilimo, lazima sasa tukipe msukumo na nafasi inayostahili kwenye mipango yetu yote ya maendeleo, kwani kilimo, ndio msingi wa maendeleo yetu wote”. Mwisho wa kunukuu.*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yalikuwa ni maeneo makali, lakini yenye busara sana yaliyotolewa na Mwasisi wa Taifa hili, Mheshimiwa Mwalimu Nyerere na Mungu ailaze roho yake mahali pema alipolala.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kilimo, ili kiwe kilimo cha kimapinduzi; aliyekuwa kiongozi wa Taifa la India kipindi fulani, Pindit Jawal Nehu, Waziri Mkuu wa India, aliwahi kusema maneno haya, naomba ninukuu: -

*“Everything else can wait but not agriculture”.*

Mheshimiwa Naibu Spika, anasema mambo mengine yote yanaweza kusubiri lakini sio kilimo. Leo tuna kilimo kwanza, hapa tunahitaji utashi mkubwa sana wa kisiasa ili kilimo kiwe kilimo kwanza. Nimepitia bajeti sana, bado hatujaweka msukumo wa kutosha katika kilimo. Bado, tunahitaji tuweke msukumo wa kutosha na mkubwa sana ili kilimo hiki kiweze kutusaidia. Kwenye Ilani yetu, tumewahi kusema maneno haya na Wakuu wetu wa nchi za Kiafrika wamewahi kukubaliana na haya maneno pia nimewahi kuyarejea huko nyuma. Naomba ninukuu kwa ruhusa yako, yanasema:-

*“CCM itazitaka Serikali kuhakikisha kuwa sekta ya kilimo inatengewa si chini ya asilimia kumi ya uwekezaji unaofanywa na Serikali, sambamba na lengo la Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi Kusini mwa Afrika yaani SADEC”.*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado hatujafika asilimia kumi ya pato la taifa kwa tunavyowekeza kwenye kilimo. Mimi namuomnba Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye katika kipindi chake kifupi, amelivali njuga sana suala la kilimo, aendele kulisukuma ili kilimo kipate nafasi katika uchumi wa nchi hii na wananchi ambao zaidi ya asilimia 80 ni wakulima waweze kufaidika na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kilimo kinapewa mbolea kidogo sana, Mbozi tuna kaya zaidi ya 120,000; lakini ni kaya karibu 50,000 tu ambazo zilifaidika na mbolea mwaka jana. Hiki ni kiwango kidogo sana. Namshukuru Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu wametuambia kwamba kilimo kitapewa zaidi ya TShs.90bn, kwa maana ya mbegu pamoja na mbolea. Kama hili litafanyika, basi utakuwa mwanzo mzuri katika kutekeleza ile kauli mbiu ya kilimo kwanza na hapo wanachi wanaweza wakaona sasa Serikali yao imeanza kuwajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumze suala la mbolea ya Minjingu. Nilichangia wakati tunazungumzia Muswada wa Mbolea, kwamba suala la mbolea ya Minjingu kwa Mbozi ni tatizo na wengi wakaona kama nakosea Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nireje kusema sikukosea na wala sijakosea. Wananchi wa Mbozi wamenituma, kwa mujibu wa Katiba yetu kwamba sisi ndio wawakilishi wa wananchi na hapa nawasemea wananchi wa Wilaya ya Mbozi, nilipotoka Bungeni, nimepita karibu Kata zote 15, nimekutana na Halmashauri Kuu za Kata, nimekutana na *WDC* zote, wananchi wamesisitiza kwamba mbolea ya Minjingu hawaitaki na hii ni kauli ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema kama Serikali au viongozi wana wasiwasi na ninayosema, jamani Mbozi si ipo? Waziri wa Kilimo, karibu Mbozi, Waziri Mkuu karibu Mbozi na bahati mbaya hujafika toka umekuwa Waziri, nina hakika ulizoea kupita pale Mbozi ukitoka Rukwa, wakati ule ulikuwa Waziri wa TAMISEMI, sasa Waziri Mkuu, mzee unaruka juu yao, tunaomba siku moja uje, wale wananchi wana hamu, lakini pia ukasikilize matatizo yao. Namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Kilimo jana nilikutana naye, alisema safari hii wananchi hawatalazimishwa kununua mbolea ya Minjingu, kwa sababu ataleta *voucher*. Kwa hiyo, mwananchi atalazimika mwenyewe *either* anunue Minjingu au aina nyingine ya mbolea. Hilo litakuwa ni jambo jema zaidi kwa sababu wananchi wa Mbozi walikuwa wanasema afadhali tupandia samadi, kuliko kupandia Minjingu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kusema hapa, jamani Mbozi tumekuwa tunatumia mbolea miaka nenda rudi, sio wanafunzi wa matumizi ya mbolea, kwa hiyo, hatukosei kuhusu matumizi ya mbolea. Ninaomba Serikali iichukulie kwamba hii ni kauli ya wananchi wa Wilaya ya Mbozi na msilete mbolea ya Mijingu kwa sababu hata mkiileta wananchi wamekata tamaa, iliyoletwa mwaka jana, bado ipo kwenye maghala haijatumika. Kwa hiyo, tusije tukawapa mzigo wale wanaouza mbolea kwa sababu itakaa kwenye maghala na wala haitaweza kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, tulipokuwa tunapitisha *Finance Bill* hapa, kulikuwa na wazo la kutoza *VAT* kwenye kahawa na chai. Mazao ya kilimo yana kodi zaidi ya 15 katika nchi hiii. Sasa tunataka tuweke tena *VAT* katika kahawa na chai, tutawaua hawa wananchi ndugu zangu! Mheshimiwa Waziri Mkuu, wananchi hawa wanachangia sana kwenye maendeleo ya nchi, leo tunataka tena tuendele kuwaongezea kodi, ambazo hapo nyuma tuliziondoa. Mimi naomba, pamoja na kwenda huko *East Africa*, Jumuiya ya Afrika Mashariki sio kila jambo lazima tusukumwe. Mambo mengine tuangalie yenye maslahi kwa wananchi wetu na tuwape wananchi nafasi ili waweze kuzalisha vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimkumbushe au nimuombe tena Mheshimiwa Waziri Mkuu, shamba la Mbozi la *NAFCO*, zaidi ya ekari 12,000 limekaa tangu mwaka 1996, limekuwa *specified* mpaka leo hakuna kilichofanyika. Naiomba sana Serikali iweze kuchukua hatua kwa kuwapa wananchi au basi kama hatuwezi kuwapa

wananchi, tuuze lakini hamna kinachoendelea. Wakati fulani niliwahi kuuliza swali nikaambiwa *land pressure* Mbozi sio kubwa, hii sio sawa Mheshimiwa Waziri Mkuu, *land pressure* kwa Mbozi ni kubwa na wananchi wanahitaji maeneo, tunaomba Serikali ichukue uamuzi unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Kamati ya Mahesabu ya Mashirika ya Umma, ilitembelea Mbozi na imetoa ushauri huo huo kwa Serikali kwamba wapeni wananchi haya mashamba, Serikali inaona kigugumizi gani Mheshimiwa Waziri Mkuu? Lakini kuna shamba la Sasanda Mbozi, lina ekari zaidi ya 800, limekaa *idle*, liko chini ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, halijafanyiwa kazi yoyote, tukiomba wananchi watumie, bado wanasema tutalitumia, tunaangalia miaka 50 sijui 100 ijayo, nadhani tunahitaji wananchi waweze kuyatumia haya maeneo kikamilifu sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumzie kidogo suala la uwanja wa ndege Songwe ambao umetengewa bilioni karibu 32.6 lakini pesa hizi, bilioni karibu 18 ni za hapa nchini na bilioni 14.6 ni za nje, zinatolewa na *BADEA*. Tumeambiwa sasa hii ni *phase* ya mwisho ya ujenzi wa ule uwanja, lakini tatizo ambalo tulikuwa tunalipata na ambalo Waziri wa Miundombinu amekuwa anatueleza ni kwamba mara kadha Hazina wameshindwa kutoa pesa za ndani na *condition* mojawapo ya *BADEA* kutoa pesa, lazima waone ninyi mnatoa pesa yenu kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, nataka nikuombe ulitilie maanani hili, tutoe pesa kadri zilivyo kwenye bajeti, tusije tukafika mahali pesa hazipo tena, kwa maana hiyo tumeshindwa kuendelea kujenga kile kiwanja cha Songwe pale Mbeya ambacho nadhani kitakuwa na manufaa sana kwa watu wa Mbeya lakini pia na watu wengine ambao pia wangependa kwenda kuona maendeleo ya Mkoa wa Mbeya na wale ambao wangependa kwenda kuwekeza katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kwa kifupi sana suala la *TICTS.* Mimi niliwahi kuwasilisha hapa Bungeni hoja ya *TICTS* mwaka jana mwezi wa nne mwaka 2008. Naomba nidiriki kusema kwamba bado mpaka leo Serikali haitaki kutoa majibu yanayoeleweka. Suala hili sasa limechukuliwa ni la kisiasa, Zambi anaposimama hapa kulizungumza anaonekana kwamba haipendi *TICTS*, sina sababu ya kuipenda *TICTS*, tunaenda kwa *facts* kwamba hivi *TICTS* inachangia namna gani katika kuzorotesha au kukuza uchumi wa nchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ulio wazi kwamba mambo ambayo *TICTS* walizungumza au waliahidi kwamba watayatekeleza mpaka leo hayajafanywa. Naomba niseme niko Kamati ya Bunge ya Miundombinu, kwa maana nyingine naweza kusema kwamba ninaifahamu *TICTS* kwa sababu pia hata bandarini nimeenda, kuna mambo mengi ambayo si sawa. Leo tunaanza kuiondolea *TICTS* lawama tunaipeleka kwa *TRA*, kwamba *TRA* ndio tatizo. Tunajua ni kweli kuna mambo mengi yanayochangia utendaji mbovu bandarini lakini mambo mengi yanachangiwa na *TICTS* Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali mchukue hatua. Hivi ni utawala gani bora jambo la mwaka mzima, kuna mambo tumeleta hapa Bungeni mwaka mzima na bado tunazungumza utawala bora; nadhani ni pamoja na kuyafanya mambo haraka yakatafutiwa ufumbuzi haraka ili wananchi wajue kwamba mambo yamekwisha lakini mnapoweka mambo mwaka mzima, mwaka na nusu, nadhani wananchi wanafika mahali wanaweza wakawa na wasiwasi na Serikali yetu nzuri ya Chama cha Mapinduzi ambayo mimi nina hakika inafanya mambo mema sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, jamani, naomba suala la *TAZARA* mlipe kipaumbele. Wafanyakazi wa *TAZARA* ambao wamestaafu wanapata taabu sana. Nimekuwa nazungumza sana na Waziri wa Miundombinu kwamba jamani shughulikieni, hangaikieni suala hili wananchi wanapata tabu, watu wamestaafu tangu mwaka 2005 mpaka leo hawajalipwa haki zao! Mbona tuna mifuko mingi? Tuna *LAPF*, *NSSF*, *PPF*, haya mashirika ya umma yanakopesha pesa kwenye taasisi nyingine; tunaona tabu gani tukaikopea *TAZARA* pesa ili wale wananchi waliotumikia vizuri wakaweza kupata haki zao na kwa maana hiyo wahudumie familia zao bila matatizo yoyote. Hili na lenyewe limekuwa tatizo, tunasema kwamba Wachina watatupa msaada lakini mpaka lini? Mimi naomba sana Serikali ijaribu kuliangalia suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninaomba Serikali ijaribu kulipa madeni ya *TTCL* ili *TTCL* iweze kufanya kazi zake. Leo *TTCL* wanaidai Serikali bilioni 2.1 kwa ajili ya mauzo yaliyotokana na uuzwaji wa Chuo cha Watumishi, Kijitonyama, lakini mpaka leo Serikali haijatoa hela na hili ni agizo la Mheshimiwa Rais. Hivi, Mheshimiwa Rais akiagiza, ni nani tena anaweka tatizo katika utekelezaji? Mheshimiwa Waziri Mkuu, wewe ni msimamizi wa shughuli za Serikali hapa Bungeni, tunaomba lifuatilie hili suala ili *TTCL* waweze kupata hela zao ili waweze kufanya shughuli zao mbalimbali za maendeleo lakini pia *TTCL* wanadai bilioni 9, zilizotokana na malimbikizo ya bili za kupiga simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja lakini nikiomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, basi ayatolee ufumbuzi masuala haya niliyozungumza, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hotuba iliyoko mbele yetu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Moja kwa moja nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri yenye mwelekeo mzuri na yenye kueleweka. Lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza dada yangu, ndugu yangu, mama Celina Kombani, Waziri wa *TAMISEMI* na Mheshimiwa Naibu Waziri, Kaka yangu Mwanri, kwa kazi nzuri pamoja na wataalamu wote kwa hotuba ambayo wameisaidia sana Wizara hii, Ofisi ya Waziri Mkuu kufanya vizuri. Pamoja na pongezi hizi, nichukue nafasi ya pekee kumpongeza kaka yangu Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kazi nzuri anayoifanya na pia utekelezaji wake wa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti iliyopita, Mheshimiwa Waziri Mkuu, alizungumzia jinsi ya kuondoa matatizo yaliyokuwepo ya barabara ya Manyoni – Itigi –

Tabora lakini kabla sijaanza hapo katika utekelezaji huo, naomba niingize kipengele kidogo tu kwa tatizo kubwa tulilokuwanalo la utekelezaji na usumamizi wa majukumu yetu. Mwaka jana kwenye barabara iendayo Urambo inayotoka Tabora Manispaa katikati yenye kilometa tatu, barabara hii alipata mkandarasi. Mkandarasi huyo alitakiwa kufanya kazi hiyo tangu Aprili mwaka 2008 mpaka 2009 Aprili awe ameikabidhi barabara hiyo, ya kilometa tatu tu. Kabla sijaenda kwenye Miundombinu kwa ndani, Mkandarasi huyo aliteuliwa kutoka Musoma kwa kilometa tatu. Gharama ya usafirishaji wa vifaa vya ujenzi ni kubwa ukilinganisha na gharama ya ujenzi wa barabara yenyewe lakini kilichotokea, Mkandarasi huyu kutwa yuko Musoma, Mkandarasi huyu hana vifaa kwenye *site* vya kutosha, Mkandarasi huyu hajatekeleza ile barabara mpaka hivi leo kamwaga matuta kwa kilometa tatu, hivi Serikali inasema nini Kilometa tatu anajenga kwa mwaka mzima! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Tabora wako Wakandarasi ambao wangeweza kufanya kazi hiyo kwa muda mfupi; kuna barabara kwa bahati nzuri au bahati mbaya wengi hawaifahamu lakini wenyeji wa Tabora wanaifahamu, ya Madaraka ambayo inapita uwanja wa Ali Hassan Mwinyi. Barabara ile kwa muda mfupi tu kapewa yule mzawa, imekamilika. Ni kigezo gani walichokitumia kumchukua Mkandarasi kutoka Musoma kwa kilometa tatu? Naomba majibu niyapate na hatua anazochukuliwa Mkandarasi huyo kuanzia sasa, ni nini kinachotaka kutokea? Amemwaga moramu tu, watu wanapata tabu, kupita tabu, wananchi wa pale wafanyabiashara wanafanya biashara kwa tabu, hakuna anayesogea pale, utapitaje? Kwa hiyo, ninaomba hilo, Mheshimiwa nimeona niliingize kwanza kabla sijaanza kuchangia hotuba yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu kama nilivyosema awali alitoa bilioni 10 kwa barabara hiyo baada ya hotuba yake ya mwaka jana lakini zile pesa hazikutolewa zote, matokeo haya ni kwa sababu tuliomba angalau barabara hii ipitike kwa kipindi cha masika na kiangazi, haikupitika, yalipita magari ya sisi wakubwa tu wadogo hamna, wadogo ni wale wanaopanda mabasi. Kwa hiyo, tunapotetea barabara ya kutoka Manyoni au ya kutoka Dodoma kwenda Kigoma, maana yake ni kupitia na wale wengine ambao ni wafanyabiashara wadogo wadogo, lakini haikukamilika kwenye sehemu korofi. Lakini asilimia kubwa kazi inayofanyika katika makadirio ya fedha za matumizi za Serikali, ni upembuzi yakinifu, miaka sita upembuzi yakinifu; hii barabara haina upembuzi yakinifu, ulishafanywa, hizi pesa zimekwenda wapi? Naomba majibu ni kwa nini hazikukamilika zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala lingine, naishukuru sana Serikali ndio maana nimesema tangu awali ninaipongeza, barabara hii angalau kwa mwaka huu imetengewa fedha milioni 6.7 kama 10 hazikutosha hizi je? Pamoja na shida tulizokuwa nazo na matatizo lakini mimi tegemeo langu ni kwamba kwa sasa zamu iliyobaki ya kufungua *corridors* zote ni ya Tabora, kuanzia Dodoma – Tabora – Kigoma, ndio *corridor* iliyobaki, kwa sababu *corridor* zingine za Kusini tayari. Hivi tumlete nani Mheshimiwa Waziri Mkuu, barabara ya Tabora unaijua, wewe ndugu yangu unapita huko, hebu fikiria tabu tunazozipata sisi wakazi wa Mkoa wa Tabora na Kigoma ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hayo kuna barabara iliyotengewa fedha kama bilioni 5 ya kutoka Tabora kwenda Nzega. Barabara hii Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha anaijua alishapita na ilimkerembesha. Nilitegemea safari hii kwa sababu alipata tabu basi angeiwekea kifua mbele, kwa sababu sisi kule hatuna Wanyamwezi ambao wako kwenye *Cabinet* hizo, hatuna wataalamu kwenye nafasi hizo za kusema atasema nilipita jana, sasa yeye ndio shahidi na yeye yuko kule. Hivi alishindwa nini kuona umuhimu wa barabara kipande kidogo, kilomita 110, kutoka Tabora anglau iweze kuunganishwa ile barabara ifike Nzega, Nzega inaunganishwa kwenda Mwanza na Dodoma, hizi barabara hazipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine kuna barabara ya kutoka Tabora kwenda Sikonge, Ipole kwenda Inyonga kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, nayo fedha yake imetengwa kidogo, lakini imetengewa kuanzia Inyonga kuja huku. Mimi ninaomba nayo iangaliwe ili angalau na Mkoa wa Tabora iwepo barabara ya lami inayofungua nyenzo zote. Mheshimiwa Waziri Mkuu, hebu lipe kipaumbele suala hili angalau basi kutengwe fedha, hakuna fedha. Tungetengewa fedha ya kutoka Tabora kwenda Ipole na hatimaye twende Inyonga. Mimi nadhani hii ingekuwa imeunganisha tayari kwenda Sumbawanga kwa watani zetu. Tungeunganishwa, Mheshimiwa Waziri Mkuu, mimi nilipita wakati natoka Kigoma barabara ya Jimboni kwako, una Jimbo bovu halina barabara; sasa umekalia hata hicho kiti ndugu yangu inakuwaje? Mimi nikuombe, Mawaziri husika, afundwapo mtoto wa tajiri na wa masikini humo humo ataenda kuosha vyombo. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakutizame wewe kwa jicho la huruma na sisi tutapatiepo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa niende kwenye ukorofi mkubwa, nilikuwa nimeomba kwamba ikiwezekana Wizara ya Miundombinu au Ofisi ya Waziri Mkuu, tungepewa hata siku nane. Niliomba hilo kwa sababu tuna tatizo kubwa la reli, Tabora – Kigoma, reli hii mbovu. Hawa watu tangu wameichukua hawajali huduma za abiria. Juzi tu hapa ajali iliyotokea Godegode hapo, ajali ile ilisababisha vifo vingi vya abiria kutokana na uzembe. Mabehewa yaliyoletwa yamewekwa nondo, huwezi kuepuka ajali, hata ikiyumba kidogo kusema utaweza kuruka hakuna, yamezibwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabehewa hayo wanayosema *express* ya kwenda Kigoma, hakuna hata *buffet* wanasema *take away; take away* mimi Mwanne naijua wapi? Leo hakuna hata mahali pa kuchemsha hata maji kwamba unaweza kumpa mtoto ambaye anasafiri, hakuna! Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakuomba utoe amri hapa Waziri wa Miundombinu apande treni ile kuanzia Dar-es-Salaam mpaka Kigoma, aone madhara yake. *CCM* tunaipenda sana, kura itapata sana na Tabora na Kigoma itapata kura zote hasa ukizinganita jana Mheshimiwa Rais alikuwa anomba msaada wa barabara hii, na yeye ninampongeza sana, lakini kabla kengele haijalia, nina mengi nitakwenda kuongea kwenye Wizara husika lakini ninataka niongee hili lifutalo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu usije ukalipokea kwenye *Cabinet* hili ninalosema. Ninasikia, sina uhakika, Chuo Cha Ardhi Tabora kinategemea kuhamishwa; bwana isije ikaleta *songombingo* humu ndani, ninaomba Chuo hiki kisihamishwe. Mimi ninasema kwa kweli nitaleta hoja binafsi kama Chuo cha Ardhi,

kitahamishwa Tabora. Lakini nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara hii tulilia kurudisha Chuo Cha Nyuki, nawashukuru wamekirudisha na sasa kinaendelea na kozi ndogo ndogo ambazo ni za muda mfupi za uvunaji wa asali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la tumbaku. Mheshimiwa Waziri Mkuu, sera yako ni nzuri lakini tumbaku imeachwa pembeni hata juzi nimeuliza, mazao mengine yana-*STABEX*, ni kama ruzuku; hivi kuna tatizo gani Mheshimiwa Waziri Mkuu, suala la tumbaku likapewa ruzuku, pembejeo za ruzuku, kuna tatizo gani nchi hii? Kwa wale wanaopata mbolea kwa ajili ya chakula na uzalishaji wapate tumbaku. Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumbaku haizungumzwi, kuna tatizo gani wakati inaipatia Serikali kipato kikubwa na fedha za kigeni? Wakulima wa tumbaku wamenyanyasika sana, wameadhiriwa sana, naomba waangaliwe sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho, ndio maana nilisema mengine nitazungumza kwenye Wizara husika, maji. Maji Manispaa ya Tabora hakuna, bwawa lile limejengwa kabla ya mimi sijazaliwa mpaka hivi leo hakuna chanzo kingine. Mambomba yale tangu wakati Hayati Baba wa Taifa, namrehemu saa hizi, alipokuwepo anasoma pale, kutoka Igombe kwenda Kazehiri, ndio yalitengenezwa, hayajafanyiwa ukarabati. *TUWASA* haiwezi, lakini wananchi wanapelekewa bili kwa sababu hawana jinsi ya kufanya kutokana na *EWURA,* lakini hakuna chochote Mheshimiwa. Maji yananuka, maji machafu, maji tope, kwa sababu kina chake ni kifupi. Tunaomba Waziri wa Maji atakapokuja aseme ni lini atatoa tope kwenye bwawa la Igombe na Kazima na kutoa yale magugu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda cha nyuzi. Kiwanda cha nyuzi ni tatizo, pamoja na kwamba wawekezaji tunawahitaji lakini ni tatizo; wafanyakazi wanateseka, hawapati haki zao, mengine nitaongea huko. Naomba niunge mkono, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Napenda kutamka kwamba naunga hoja mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, kwa michango yao iliyowezesha Waziri Mkuu kuandaa hotuba hii nzuri yenye mwelekeo na mipango mikakati ya kuboresha maisha ya wananchi wa Tanzania na kuimarisha uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Rorya, wanampongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa kutekeleza ahadi yake aliyoitoa mwaka 2005 wakati wa kampeni kwamba atawapatia Wilaya. Wanataka kumuhakikishia kwamba watakuwa watiifu kwake na kwa viongozi, wataendelea kulinda mpaka wa nchi yetu, wataendelea kulinda amani, uhuru na mshikamano wa taifa letu. Wananchi wa Rorya ni wapenda amani na wapenda maendeleo, hususan elimu, sio wagomvi na wanalaani sana mauaji ya Albino.

Lakini pamoja na hayo hawapendi vurugu wala hawapendi kuchokoza mtu lakini hawapendi kuchokozwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa naibu Spika, si kweli kwamba wananchi wa Rorya kwa kupitia Madiwani wao wameshindwa kufikia uamuzi mahali pa kujenga Makao Makuu, si kweli kabisa. Huu ni upotoshaji wa hali ya juu unaofanywa na baadhi ya watu wachache wakiongozwa na Diwani mmoja ambaye hataki kukubali matokeo na maamuzi. Kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa, Sheria Namba 7 na 8 ya mwaka 1982 na kwa mujibu wa tangazo la Serikali namba 241, Ibara ya 26 (1) inasema:-

*"Maamuzi yote yataamuliwa na Baraza la Madiwani na kupata baraka kutoka kwa Kamati ya Ushauri ya Mkoa."*

Mheshimiwa Naibu Spika, vikao vinne vilishafanywa na wananchi na wajumbe kwa 99% walishaamua mahali pa kujenga Makao Makuu. Ni diwani huyo huyo na genge leke na watu wake ndio wameendelea kupinga. Mheshimiwa Rais, kwa mamlaka aliyonayo na kwa busara zake ameamua kutangaza eneo jipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbele ya Mkuu wa Mkoa kwenye Mkutano, ni Diwani huyo huyo ndiye alileta vurugu kwa kumtishia Mwenyekiti wa Wilaya kwa bastola. Sasa tunajiuliza kulikoni huyu Diwani anaendekezwa? Kama ameshindwa kuishi Rorya ahame! Wananchi wa Rorya wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais na wanampongeza kwa kutangaza Makao Makuu katika kijiji cha Ingrijuu, Kata ya Mirare, Tarafa ya Giranga. Wanaomba na wanashukuru Mheshimiwa Rais kuwapatia Mkuu wa Wilaya. Wanamuunga mkono Mkuu wa Wilaya, Luteni Kitange. Ni mchapakazi, muadilifu, ana nidhamu ya hali ya juu; ninaposema ni kanali mnanielewa. Lakini hiyo haitoshi, juzi tumempata Kanali mwingine, Mkuu wa Mkoa. Sasa wanaomba tuwaachie wafanye kazi, awashughulikie hawa watu, wasiwe wanakimbiakimbia mara wamepiga simu kwa Rais, mara wamepeleka barua kwa nani, nchi haiwezi kuendeshwa hivi. Hawa ndio wamemegewa sehemu ya nchi kuwa Rais, hawa ndio walinda amani, utulivu, mshikamano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri Mkuu, atoe baraka zake kwa viongozi hawa. Wananchi wa Rorya wana imani sana na Mkuu wao wa Wilaya, ni kijana mzuri sana. Sasa kama kawaida yetu, mnajua kama mnampenda mtu, kimila zetu sitaki kusema; lakini mmenielewa, lakini ninachotaka kusema ni kwamba wasimamie mambo yote ambayo yameshaamuliwa kwa vikao halali na Rais akawavumilia, akasema basi naamua iende pale, bado wanapinga! Ninavyozungumza leo huyo mtu mmoja, Diwani mmoja na watu wake ameandika barua sijui Wizara ya Ardhi, sijui wapi, eboh! *(KIcheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa ujenzi wa Makao Makuu umeshaanza na ninaomba usimamiwe na Mkuu wa Wilaya na ninaomba wananchi wa Rorya wasomi, wafanyabiashara ambao wanaishi Tanzania na nje ya Tanzania warudi wawekeze katika Wilaya yetu. Wanachi wa Rorya kuanzia mwaka 2000 wameshajenga sekondari 31 kabla ya hapo tulikuwa na sekondari 8, mchakato wa kujenga Chuo Kikuu umeanza na

tutajenga. Tuna Maprofesa wengi sana, ndani na nje ya nchi, sisi tunapenda elimu; na huwezi kwenda katika mji usimpate mtu ambaye amehitimu elimu ya juu au sekondari.

Sasa naomba warudi tujenge Wilaya yetu na tunashukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kutuunga mkono. Tunamshukuru Waziri Mkuu, wewe ni mwana Rorya, ninaposema wewe ni mwana Rorya ni kwa sababu sehemu ya familia yako iko Rorya, tunakukaribisha uje tukupe uraia wa Rorya na tutakupa ardhi ya kuishi. Tunampongeza sana Mheshimiwa Kombani, wamenidharaulisha sana hawa genge la wahuni, lakini vumulia hiyo sio picha ya wananchi wa Rorya, wananchi wa Rorya ni wakarimu sana. Unaweza kurudi wakati wowote, una marafiki wengi na wewe ni shemeji yetu, hakuna atakayekugusa. Baada ya maelezo hayo, ninaamini sasa suala linaloandikwa kwenye magazeti kila wakati limefikia tamati. Tuachane nayo tumuunge mkono Mkuu wa Mkoa yuko pale, ninamfahamu sana ni Mwanajeshi, tumuunge mkono Mkuu wa Wilaya Mwanajeshi, Rorya ijengwe kijeshi na iendeshwe kijeshi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naomba ruhusa yako nichangie maeneo machache. Kwanza, kutokana na fani yangu mimi nitachangia eneo la afya. Wilaya mpya ya Rorya haina Hospitali, tulikuwa na Hospitali tukichangia na Tarime lakini najua kwamba tutachukua muda mrefu kujenga hospitali, kwa hiyo, tunaomba vituo vya afya vya Kinesi, Changuge na Utegi, vipatiwe watumishi wa kutosha na madawa ya kutosha viweze kufanya kazi ambazo zinafanywa na Hospitali; hilo ni ombi maalum. Vile vile tupatiwe magari kwa kila kituo, hatuna hospitali. Lakini wakati huo huo tunaomba mchakato ulioanza wa uboreshaji wa vituo vya afya, kwa kuwa Rorya ni Wilaya mpya ipewe kipaumbele zaidi, vituo vyetu vya afya vilivyopo vifanyiwe ukarabati wa haraka. Kuna upungufu mkubwa wa watumishi wa sekta ya afya wapatao 150. Naomba Wizara, watumishi wa kada mbalimbali wafanye mpango maalum wa kutupatia watumishi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakati inabidi mimi nifanye kazi ya Udaktari nikienda nyumbani, wagonjwa wanakuja nyumbani kwangu kwa sababu mimi bado ni Daktari, leseni yangu haijafutwa, hata wakati huu naweza kufanya kazi ya Udaktari. Kwa hiyo, tunaomba vituo hivi vifanyiwe ukarabati wa haraka ili tuweze kunusuru maisha ya wananchi wetu hususan mama na mototo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba ujenzi wa Makao Makuu, utakapoanza uende sambamba na ujenzi wa Mahakama zetu za Tarafa na Kata. Kadhalika ujenzi wa Ofisi za Serikali za Kata na Vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, narudia kusisitiza tena kwamba wananchi wa Rorya wamepokea kwa furaha na shangwe uamuzi wa Rais kutangaza Ingrijuu ambayo ni sehemu ya Kati ya Mirare, Tarafa ya Kirango kuwa Makao Makuu; wanampongeza sana na sisi tunamuhakikishia tutailinda nchi yetu na tutatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa vitendo. Nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Sarungi, isipokuwa kwamba Wilaya ile iendeshwe kijeshi, ndio sina uhakika. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge naomba tukumbushane baadhi ya mambo ambayo tunapaswa kuyazingatia. Kwanza kabisa, jana jioni Mheshimiwa Spika, aliwaeleza kwamba tulikuwa na orodha kuubwa sana ya wachangiaji na kwa utaratibu na siku ambazo zimebaki kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, tukifika 60 itakuwa ni bahati. Kwa hiyo, akaagiza kwamba majina yapangwe upya kwa sababu ilionekana kwamba labda kuna msururu wa watu wa aina moja dhidi ya wengine kwa hiyo wakapanga upya. Kwa hiyo, wengi wameandika barua wakiuliza kwa nini nimebadilishwa, kwa nini nimebadilishwa; hili lilikuwa limeagizwa jana kwa mujibu wa Kanuni ya 60(6). Kwa hiyo ukiona jina lako limepanguka panguka basi usiandike hapa kwamba mutanieleza tu imekuwaje? Ni kwa mujibu wa Kanuni ya 60(6) ambayo inasema tutakuwa tunatoa nafasi ya kuchangia kwa kutazama maeneo, kwa kutazama jinsia, kwa kutazama itikadi na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, naomba msiniandikie tena barua kuniuliza juu ya hilo maana nimejibu nyingi sana ni kwa nini, sasa naomba msiniulize tena.

Lakini la pili, katika orodha hii tumegundua kuna wengine walishachangia Wizara ya Fedha, kwa hiyo, wale waliochangia Wizara ya Fedha majina yao yataondoka. Tunayo majina kadhaa hapa ya ambao walichangia katika Wizara ya Fedha, kwa hiyo, wakiona majina yao hayapo ni kwa sababu hiyo. *(Makofi)*

Tatu, ninaomba tuzingatie Kanuni ya 66(3)(a), ambayo inasema tukiwa humu ndani ni lazima kuzima simu ya mkononi na kwa namna yoyote ile kutotumia simu. Wapo ambao simu zao zinasikika pamoja na kwamba tuna mtambo wa kuweza kuzuia simu zisisikike, inaelekea kuna simu nyingine za kisasa zaidi hazikutwi na ule mtambo, kwa hiyo, Kanuni yetu hii inatumika. Kama unapenda kutumia simu, toka nje ukafanye hiyo shughuli halafu urudi. Kwa hiyo, tunaomba hiyo izingatiwe kwa sababu, Bunge kama la Malawi, nimeona mwenyewe kwa macho yangu simu ilipoita *Serjeant-Art-Arms* amekuja kumchukua Mbunge na kumtoa nje na anakaa huko wiki tatu. Kwa hiyo, naomba sana hii Kanuni yetu tuizingatie. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tuzingatie baadhi ya haya mambo na ninaomba nisitishe shughuli za Serikali mpaka saa 11:00 jioni. Tutakaporudi, Waheshimiwa wafuatao wajiandae; Mheshimiwa Haroub Masoud, Mheshimiwa Sevelina Mwijage, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa John Malecela na wengine watakaotajwa baadaye. Waheshimiwa, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11:00 jioni.

*(Saa 07:00 mchana, Bunge lilifungwa saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunasitisha shughuli za Bunge mchana, nilikuwa nimemwita Mheshimiwa Haroub Masoud, Mheshimiwa Sevelina Mwijage, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya,

Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa John Malecela. Sasa tunaanza na Mheshimiwa Masoud.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya mwanzo jioni hii ili na mimi nichangie hotuba ya Waziri Mkuu, mimi kwanza nitamke tu kwanza nimeikubali na ninaiunga mkono asilimia mia moja. *(Makofi)*

Lakini vilevile nimpongeze yeye mwenyewe binafsi Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Waziri wa TAMISEMI na Naibu Waziri. Kweli labda nimwambie tu Mheshimiwa Waziri Mkuu umepata Waziri TAMISEMI aliyefuata unyayo wako na vilevile Naibu wako ni miongoni mwa Manaibu Waziri wazuri sana kwa sababu naamini Manaibu wapo wengi lakini na yeye yupo miongoni mwa wale *top ten* katika utendaji kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwa kupitia kwako, nampongeza sana Waziri wa TAMISEMI, kipindi kilichopita hapa niliuliza swali la nyongeza kwa ajili ya kupeleka Jimboni kwangu fedha za kumalizia ujenzi wa ofisi ya Bunge. Fedha zile zimefika mwezi wa Mei, wiki ya mwanzo, namshukuru sana na *Inshallah,* Mwenyezi Mungu atamjalia kila baraka na heri katika kazi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Wabunge akina mama walinivutia sana wiki iliyopita Mheshimiwa Lucy na leo Mheshimiwa Shellukindo, wamezungumzia vyema kabisa kuhusu watendaji wakuu Serikalini na bahati nzuri nimefurahi sana kwamba hawakuwaingiza Mawaziri kwa sababu Mawaziri ni wanasiasa katika kazi za Serikali za kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama utakumbuka ulikuwepo katika Bunge la mwaka 2005 pamoja na Mheshimiwa Marmo ananiangalia pale, nilipokuwa nachangia hotuba ya Waziri Mkuu nilikuja na kitabu ya Albadili, ubani na chetezo na nikamwambia Mheshimiwa Sumaye kwamba nitasoma Albadili, kuhakikisha kwamba wale wabadhirifu ndani ya Mawaziri wanapukutika kama senene. Sasa matokeo tunayaona kwa hivyo nawapa pole Mawaziri wetu, wawaogope sana watendaji wa aina hiyo, mimi sisemi kama ni wote lakini hali ni mbaya na lazima wadhibitiwe kwa hali zote zile. Kwa uwezo wako Mheshimiwa Waziri Mkuu, kazi hiyo utaweza mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakuja la pili, kama unavyelewa *TBC* imebadilika kweli kweli miaka mitano nyuma ilikuwa kwa kupewa *marks* ilikuwa ni asilimia 25 sasa hivi wamefikia asilimia 99. Lakini *TBC* imewekwa kama mtoto wa kambo, mtoto wa kambo siku zote anasukumwa huku, nguo hanunuliwi, tulikwenda kutembelea Mheshimiwa Waziri na Kamati pamoja na Mwenyekiti wangu Mheshimiwa Mhagama, tulisikitishwa na nimewahi kuisema mara moja hapa, tulisikitishwa na bahati mbaya ilikuwa siku za mvua, tukakuta katika chumba kimoja cha habari kuna ndoo ya moja iko katikati, sasa mimi nikauliza mnaoga humu ndani, wakasema hapana Mheshimiwa, si hivyo, jengo hili linavuja. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ni kubwa zaidi, miaka kumi iliyopita paliwekwa jiwe la msingi pale na majengo yale makubwa yapo pale, mpaka leo Mheshimiwa Waziri Mkuu hayajakumbukwa, Wizara ya Fedha haijaweka fedha, hakuna lolote lililotendeka pale, sisi kwa juhudi zetu Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kama ulivyofanya mwaka jana, mwaka jana ni mambo yangu matatu niliyazungumza kwako na ninashukuru siku ile ile yamechukuliwa hatua kwa sababu uliwaandikia Mawaziri wanaohusika siku ile, sasa huu ndiyo utendaji wa Serikali, sio unamuandikia Waziri au unamwandikia Katibu Mkuu mwaka mzima barua hajibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa majengo yale tukaona tutumie busara mimi na Mwenyekiti wangu na Kamati yetu, tukawaita watu wa hifadhi, *NSSF* tukazungumza nao na wao wenyewe watu wa *TBC* tukazungumza na watu wa habari, tukakaa nao jamani tuokoe fedha za Serikali hizi kama kweli mna uchungu na Serikali, kama kweli mnaipenda Serikali, kama kweli mnakipenda chama chenu, majengo yale yamalizwe yamekaa bure, *billions and billions* za pesa zimepotea bure pale, majengo yamekaa wanalala paka ndani, kwanza kunanuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hatua tuliyochukua Kamati Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kubwa sana *DG*, Dr. Dau alikubaliana moja kwa moja kwamba yeye akipata *guarantee* ya Wizara ya Fedha, majumba yale yatamalizwa haraka sana. Taratibu zote Mheshimiwa Waziri Mkuu zinazohusiana na kupata *guarantee* zote wamezikamilisha, imebakia Wizara ya Fedha mpaka sasa hivi hatujapata jibu lolote hakuna lililofanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa zile fedha ni mkopo na Mkurugenzi Mkuu wa *TBC* yeye mwenyewe ameahidi kuzirejesha fedha zile kwa miaka ambayo ametakiwa na *NSSF*, wala haitaji fedha za Serikali anasema ana uwezo sasa hivi zamani nikitambaa sasa hivi nina chupa juu. Sasa mtu katolewa alikotolewa, kawekwa pale, hebu tumpe raha yule mtu, tumpeni raha ndugu zangu, hebu tuwaonyeshe watu kwamba uwezo wake ni mkubwa, anaweza kufanya kitu cha maana. Lakini mpaka leo imelala Wizara ya Fedha, hatujui sababu gani *guarantee only*. Mheshimiwa, naomba hili uliingilie kwa sababu utakapoliingilia hili umeokoa taifa zima. Mawaziri sisi tunakuja pale tunahoji hawana lolote la kusema kwa sababu hawana uwezo ule hata sisi Kamati basi hatupewi heshima yetu, haipewi heshima Serikali, tunaomba Waziri Mkuu hilo nina hakika utalichukulia hatua kama ulivyochukulia hatua mwaka jana suala la *NIP*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine hili ni rai, liangalieni katika *cabinet* na tumeliona wakati tunapitia taarifa za Wizara ya Kazi na nyinginezo, Serikali inaonyesha inapoteza fedha nyingi sana kwa ajili ya pango la ofisi zao, Serikali inapoteza fedha nyingi sana kwa ajili ya pango za nyumba za maafisa na nyumba za Mawaziri hapa Dodoma. Mheshimiwa tutumie hii mifuko, hebu kila mwaka tuweke *target* yetu safari hii tunajenga ofisi tano za Mawaziri na safari hii tunajenga angalau *rest house* 20 za Mawaziri. Mtu anakodi nyumba laki saba, hivi kweli tuko na raha zetu na mifuko iko tele hii iunganishwe, hakuna lisilowezekana Waziri Mkuu hata moja tuangalie Chuo Kikuu kile pale. Kama mtu alipita miaka mitatu nyuma, ukamleta kwa helkopta ukamshusha

pale atasema sio Dodoma, lakini mifuko yetu wenyewe kwa mikopo, *guarantee* ikishatoa Wizara ya Fedha hakuna lisilowezekana hata moja. Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakuomba sana, chonde chonde ulisimamie ili tuendelee mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia habari za ajira za nje, Mheshimiwa Waziri Mkuu nchi nyingi sana zinataka wafanyakazi kutoka Tanzania, wa kila aina mpaka madereva, lakini Balozi zetu hazitusaidii kututafutia ajira hizo. Libya wanataka, isipokuwa mimi niwapongeza watu wa Wizara ya Kazi kwa juhudi zao wanatumia ma-*agent* tofauti wa kiraia, hivi karibuni wamepeleka watu 200 sijui na zaidi nje kwa mikataba maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama kazi ile inaweza kufanywa na watu hapa hapa sisi wenyewe, Mabalozi tunao wenyewe tele nchi za nje, hebu wachangamke, watu wetu maskini angalau waondoke, wakipata mshahara kule wanakuja kulisha watu wao hapa nchini tunapata kodi sisi hapa. Mheshimiwa Waziri Mkuu, hilo nalo tungeomba sana ukalisimamia kikamilifu, nakwenda mbio mbio, hilo ni ajira za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nakuja lingine, Mheshimiwa Waziri Mkuu, sasa hivi utamaduni wetu umeharibika, tulizungumza tukiwa na watu wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, nyimbo zetu Mheshimiwa Waziri Mkuu chafu sana, nyimbo zetu tena wala si kizazi kipya, kizazi kipya nawapongeza sana sijasikia nyimbo hata moja za kizazi kipya ambayo ina matusi lakini taarabu hizi, *modern* taarabu hizi ndugu zangu huwezi kusikiliza nyimbo za *modern* taarabu mbele ya Chilolo, labda mtu mwingine, mimi ni mtu wa haya Mheshimiwa, ni mtu wa haya, nakimbia. Mfano wa nyimbo asilia moja tu nitakupeni ubeti mmoja unasema:-

*"Nanasi utamu wake, linapumbaza moyoni,*
*Naipenda radha yake, ulitiapo kinywani,*

Mheshimiwa Naibu Spika, hujui kakusudia nini huyu, ni fumbo, anasema nanasi kwa nini liliwekwa nanasi, lakini sasa hivi mambo yako wazi wazi, naona haya wala sitaji nyimbo moja chafu lakini ziko tele, hawajui kutunga mashairi, wao kazi yao kusukuma sukuma tu, tunaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani liliulizwa swali hivi karibuni hapa sijui na Mheshimiwa Dr. Mwita au nani, juu ya Chuo cha Marine Sayansi Ugunja. Chuo kile tangu kilipoasisiwa kijengwe kina miaka 20 mpaka Zanzibar ikaundwa Kamati ya kusimamia chuo kile kufuatilia pamoja na Benki Kuu. Bahati nzuri Mwenyekiti nilikuwa mimi, akina Mheshimiwa Kidawa walikuwepo hapa bado Wabunge, akina Dr. Mwita walikuwepo, tukafuatilia mpaka kiwanja tukakipata cha Benki Kuu. Leo ukiitembelea Zanzibar, hebu kaiangalie Benki Kuu utazania uko Nairobi, Benki Kuu nzuri, ya kisasa, yale ndiyo matunda ya Tanzania, leo Marine Sayansi walichagua wenyewe kiwanja Mkokotoni, wakakaa wakakifelisha, tukawapatia Buyu, juzi nimeambiwa inasuasua ujenzi fedha sijui hakuna sijui kuna kitu gani. Hii ni aibu kwa nchi unapoanza ujenzi halafu unasimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja hii ni kama nilivyokupongeza kabla kwamba suala la kiwanja cha *NIP* ulisaidia siku ile ile na siku ile ile Mheshimiwa Chiligati, mtoto wa kazi aliandika barua akamuandikia Waziri wa Elimu, fedha zile zimetolewa. Lakini cha kusikitisha kwa Wizara ya Ardhi, Mheshimiwa Waziri hebu pekecha pekecha kuna nini Wizara ya Ardhi, wale wamenyang'anywa, *NIP* ni taasisi ya Serikali lakini hawa *IMTU,* hawa watu binafsi tangu wamepewa sasa hivi ni miaka minane kama sikosei au saba, hawajaendeleza, hawajajenga, hawajafanya chochote. Sasa ikiwa Serikali imenyang'anywa wale wanaogopwa nini? Wizara ya Ardhi kuna maneno, lakini bahati nzuri nimefurahi sasa hivi mwenyewe mtoto wa kazi yuko pale Mheshimiwa Chiligati atafuatilia, atamuuliza Mheshimiwa Katibu wake, watu wa aina hii ndiyo wale aliowasema Mheshimiwa Lucy na Mheshimiwa Shellukindo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine haraka haraka na ni kubwa zaidi ni kwamba lazima kwa njia yoyote wale wanaoisengenya Serikali kwamba hakuna kitu chochote, ukikifuatilia kitafanikiwa, Mashehe wale, Mapadri, Maaskofu, waliambiwa msizungumze na maredio na magazeti nendeni kwa viongozi wa juu, bahati nzuri nakupongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, walikuja kwako ukatoa maamuzi ya haraka sana, uongozi ndiyo wa aina hii, uongozi unasikiliza wananchi wako, unasikiliza malalamiko yao, unaliangalia lipi nzuri lipi mbaya, umeona kweli ni bora kwa sababu ya *NGO's*, taasisi za dini hizi zinachangia Serikali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sipendelei kugongewe kengele na *inshallah,* nitatafuta kwenye Wizara nyingine nichangie. Lakini nimechangia ofisi yako makusudi najua unasikiliza, unafuatilia na maamuzi unatoa haraka, ahsante sana, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. SAVELINA M. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia, naomba nianzie kwenye ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesema hapa kilimo kwanza, tunakubali na mipango mizuri sana iliyomo kwenye kitabu hiki cha bajeti, lakini tunaomba utendaji na wenyewe uwepo, isiwe mikakati ya kuandika kwenye vitabu tukashindwa kutenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wetu ni mkubwa sana una ardhi nyingi sana, mikakati hii ya kilimo ikiwezekana kuwezesha kilimo cha umwagiliaji, mapori tunalinayo ya kuficha majambazi yatashughulikiwa, tutashukuru sana. Tuna migogoro mingi hasa sehemu za Kiakuka, nitamuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba unisikilize uweze kutusaidia, hii migogoro imekuwa kero kwa siku nyingi, tangia nimeingia Bunge hili nachangia sana hii migogoro. Migogoro ya Bubale na migogoro ya Kitengule ranchi, kila navyosimama hapa lazima niliseme hili sasa nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu wewe ndiyo utakayemaliza haya yote. Kwa sababu ranchi ya Kitengule mwaka 2002 Serikali iliwagawia wawekezaji 10, lakini kati ya wawekezaji 10 wawekezaji tisa ndiyo ambao wanaoendeleza ardhi hiyo na walipewa ardhi ndogo sana kila mmoja alipewa ardhi, eka 2000.

Lakini mwekezaji mmoja huyu wa Kagera Sugar yeye alipewa ardhi 30,600 yeye mwenyewe amechukua ardhi ameishika, haifanyii kazi anajidai yeye ni mfugaj,i ni ranchi ana ng'ombe 300 na anawanyanyasa wananchi walioko karibu pale mpakani, mbuzi wake asihame kutoka kwake sehemu za Kianga na sehemu za jirani pale kuingia sehemu ile na ardhi waliyompa haifanyi kazi na ile sehemu walisema aliomba kwamba anataka kulima miwa na miwa yenyewe pale si rahisi kustawi kwa sababu ni milima na mabonde. Wakazi wa pale hawaruhusiwi kwenda kukata majani hata ya kuezeka, hawaruhusiwi hata kukanyaga mle kutafuta kuni.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, chonde nakuomba sana utusaidie, uweze kufika pale, uweze kuwasaidia wananchi wa pale, yeye kama hawezi, awagawie wananchi walioko pale majirani ambao ni watu wa Karagwe waweze kuitumia na sasa hivi ndiyo tunasema kilimo kwanza. Kama ni kulima walime, kama ni kufuga wafuge.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakwenda Bubale, wananchi wa pale wamekaa kwa miaka mingi sana pale na ile sehemu ilikuwa ni ya kwao kabisa lakini wakaleta mwekezaji pale na yule mwekezaji hana faida yoyote anayoingiza kazi yao ni kuwanyanyasa wakazi, kiongozi yoyote akiondoka kwenda kule anaruhusiwa afike kule mpaka anarudia pale pale kwenye kiwanda cha miwa. Hafiki kule ili kuona matatizo waliyonayo, wanafukuzwa kutoka pale toka mwekezaji amekuja basi wawatafutie sehemu nyingi waende wakalime, mtu wanamwambia kwamba ondoka pale halafu wanamchangisha pesa za maendeleo za ujenzi wa shule pamoja na zahanati, kweli huo sio unyanyasaji, sehemu ya Kaishundo, wako karibu na sehemu ya mamlaka ya chai, wale watu wamefungwa hawana hata sehemu ya kupita kupeleka ng'ombe zao kwenye malisho, hawana hata sehemu ya viwanja vya watoto kwenda kuchezea mpira, yule mwekezaji amechukua zile sehemu mpaka sasa hivi watu wanaleta malalamiko kila siku kesi zimeshakuwa kesi. Msipomaliza hiyo migogoro ya ardhi kwenye Mkoa hata kilimo hakitafanyika kwa sababu ardhi zote zimetekwa na wawekezaji na hawazifanyii kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, hizi chaguzi zilizofanyika ni maajabu hilo daftari, unakuta mtu mmoja ana majina matatu mle mle kwenye datfari. Ukifuatilia kwenye Tume na wewe unafahamu ikiwa uchaguzi huwezi ukasema wewe mpinzani kaa chini kwa sababu ukilalamika unamwambia huyu mtu mbona ameandikisha mara mbili wanakwambia watashughulikia wakati kupiga kura unaona amepanga mstari anakwenda kituo hiki. Nilikuwa naomba hili daftari liweze kurekebishwa na lifuatiliwe mpaka mwisho na jina lake moja na sehemu yake moja sio madaftari matatu na yeye yumo kila daftari inakuwa kero katika kipindi cha uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naingia kwenye sehemu ya watendaji wa kijiji, kwa kweli safari, nashukuru sana kwa sababu hotuba ya Waziri Mkuu ameshukuru sana wananchi wanapochangia maendeleo na kweli walikuwa wanatuuliza mara kwa mara wanasema shule imejengwa na Serikali mbona sisi wananchi hatusemwi kwamba wananchi Fulani, kijiji fulani wamechangia, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri

Mkuu kwa suala hili watu wote wamesikia na wakapiga simu wakashukuru kwa kuona thamani yao ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hao watendaji wa vijiji, wamekuwa miungu mtu kwa wananchi, kuchangia watu wanakubali, lakini tatizo mtu anatuma mgambo pale, anamkamata, anampiga viboko, anamweka ndani, anakaa siku mbili tatu, anamwachia, sasa kuliko kumfanya hivyo, unampiga viboko kwa nini usimchukulie hatua angalau ukampeleka Mahakamani, ni unyanyasaji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda kwenye afya, wafanyakazi wa afya katika Mkoa wa Kagera, hospitali ya Mkoa, kuna Madaktari wanalalamika kila siku, nimeshaomba kuuliza swali hilo lakini kwa vile nimepata muda huu, Serikali yote iko hapa watawasikiliza na kuwasaidia. Kuna Manesi walienda kutibiwa wakatumia pesa yao, wakapewa *appointment* ya kurudi, mpaka sasa hivi wananyanyasika kweli, kila mara wananipigia simu tuulizie basi huko. Sasa kwa kuwa Serikali iko hapa, itaweza kulifanyia kazi na hao watu kuweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda kwenye ajira, naomba sana Serikali kilimo kwanza na MKUKUTA, unakuza uchumi, sasa Mheshimiwa Serikali hii isipojiangalia sana kukuza viwanda angalau tukawa tunatengeneza matunda kwenye nchi yetu kuliko kutegemea matunda yanatoka Tanzania kwenda Kenya yanarudi makopo hapa na matunda yametoka Tanzania, kwa nini tusiwe na mikakati yetu tukawa kwanza tunaandaa kidogo angalau safari hii bajeti hii tukatengeneza hiki kikaisha vijana wetu wakaweza kupata ajira kuliko kuteseka? Wanaendesha baiskeli wanapigwa, wanaendesha pikipiki wanapigwa kwa sababu mtaji wa maskini ni nguvu zake mwenyewe na huku anapigwa lakini viwanda vikiwa vingi wakapata kazi, hiki kilimo cha umwagiliaji kikija ni rahisi sana kuweza kupata ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye *SACCOS*, *SACCOS* imekuwa kero, hizi pesa za JK wengine wanajipangia inakuwa kampeni ya siasa kwa sababu mtu anafuata pale pesa anajiandikisha, kufika pale wanamwambia leta kadi ya CCM, hizo pesa sio za siasa, watu wameshanyanyasika kweli na ni wengi wanaunda vikundi, kama nadanganya naomba mfuatilie muone matatizo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naenda kwenye uwanja wa ndege, nimesoma hapa kwenye hotuba, nikakuta wamechanganya na uwanja wa Mpanda sasa wa Bukoba sijui umetengewa shilingi ngapi ili kuweza kuongeza zile wakaweza kumaliza uwanja ule tukaacha kuwa tunapelekwa vindege vya kutupeleka, kufika bahati nasibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naingia kwenye barabara ya Muleba hadi Rusunga, tunashukuru sana lakini hatujajua ni lini itatengenezwa ili wananchi waweze kuwa na imani, kwa sababu ile barabara imekuwa kero. Ni kero kubwa kwa sababu ile barabara magari yakiingia mle hayafiki Biharamulo na majambazi wanawateka kwa sababu barabara ni mbovu ikiwa imetengenezwa vizuri hakuna matatizo, ni rahisi wananchi kuweza kupata vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda kwa Polisi, naomba niwasemee Maaskari hawa, Maaskari wapo barabarani wanafanya kazi kwa mfano Maaskari wa Gairo, kituo chao kilipo ni mbali sana na sisi hii barabara tunaitumia mara kwa mara ni barabara ambayo wale Maaskari wanatusaidia sana kwa kweli, kituo kilipo kule ni mbali sana hata mimi pale kuna gari yangu ile iliyopata ajali niliitafuta mpaka nikachoka. Ukipata tatizo pale barabarani kuja kuwapata ni shida, wewe unasema Maaskari hawakufikii ni kwa sababu wako mbali walinionyesha kwamba walishapewa kiwanja pale pale, Serikali wakati inapanga bajeti na wenyewe angalau nawasemea kwa sababu wanatusaidia sana, hiyo barabara ni yetu sisi waweze kuwa karibu na barabara hata ukiwa na shida nao ni rahisi kuwapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, naenda moja kwa moja kwenye Serikali za Mitaa. Serikali za Mitaa sasa hivi tunaelewana, tunapanga mikakati sheria inafanya kazi, lakini tukishafika kwenye chaguzi, vurugu inaanza, tunaanza kuvurugwa, mara muweke pingamizi, mara muweke ndani, mara fanya nini, hapa tunaongea vizuri kuna sheria lakini tukifika wakati huo wa kuanza kugombea inakuwa vurugu. Naomba sheria ichukue mkondo wake kila mmoja atakayekuwa anatoa taarifa awe anasikilizwa sio kusikiliza chama tawala peke yake kwa sababu ingekuwa hivyo vyama visingesajiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda moja kwa moja kwenye kilimo, narudi kwenye kilimo cha kahawa nimesahau hapo, sisi watu wa Kagera, sana sana kilimo chetu ni kahawa na majani ya chai, sasa mimi nasikitika, nimetembea Kilimanjaro huko kote nimekuta kahawa zao ni nzuri sana, halafu wao bei yao ni tofauti na sisi kwetu Kagera. Halafu watu wa Kagera, watu wanauza kahawa Uganda wanapata pesa nzuri sana tu.

Naomba Serikali hawa watu wanauza kahawa zao bei nzuri Uganda ni kwa nini wasiwaruhusu wakauza kule, ni tatizo gani kwa sababu yeye ukija kumchangisha hapa mwananchi wa mkoa wa Kagera, hana pesa, kipato chake kidogo lakini akiwa na kahawa, majani ya chai mpaka sasa hivi yamekuwa kuni, lakini wakipata maelekezo mazuri, bei ikatoka nzuri na kiwanda kikatengenezwa vizuri hiki ambacho kiko pale Bukoba *Tea Estate*, wanaweza wakapata hata uchumi wao mzuri bila hata kufika saa ya kuombaomba au kusema kwamba sisi ni maskini, sisi sio maskini kila kitu kipo isipokuwa mipangilio ya Serikali. Tunaomba sana mipango ya Serikali iende vizuri kama ilivyoandikwa kwenye kitabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisipigiwe kengele ya pili, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Naibu wake, Watendaji wote kwa kazi nzuri ya kuandaa hotuba na hatimaye wakatengeneza bajeti ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameweza kuisoma kweli. Kwa kweli nina kila sababu ya kumpongeza.

Lakini pia nichukue nafasi hii, kumpongeza Mkuu wangu wa Mkoa, Brg. Dk. Balele, jinsi anavyosimamia shughuli za maendeleo na jinsi anavyojitahidi kuhakikisha kwamba Shinyanga tunatoka kwenye zero kwenda hatua mbele. Mungu ambariki na aendelee kuchapa kazi, huyo ni Kamanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongeza hizo, ninataka nitoe shukrani zangu pia kwa Serikali, kwa mambo ambayo tumeyafanya katika Wilaya ya Bukombe hasa tulipokuwa tunaingia wakati wa kunadi Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Nina kila sababu ya kupongeza na kutoa shukrani zangu, kwa sababu nisipofanya hivyo hata wananchi wakati mwingine wanaweza wasinielewe, kwa sababu wakati tunaingia hatukuwa na hospitali ya Wilaya, leo Bukombe tuna hospitali ya Wilaya nzuri ya kisasa, upungufu uliopo, Mheshimiwa Waziri wa Wizara husika tumewasiliana, tatizo la *X-ray*, haifajafikishwa pale lakini nashukuru kwa sababu amenijibu kwa maandishi kwamba ni lini itafika pale, ninaomba muipeleke ili tuhakikishe kwamba wananchi wetu wanahudumiwa vizuri, tumepata Mahakama ya Wilaya ambayo inaendelea ilikuwa ni tatizo sana katika Wilaya yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nipongeza kwa ajili ya kufungua barabara, tumefungua barabara katika Wilaya zaidi ya kilomita 300 na kitu, kwa hiyo hali ni nzuri lakini shida katika eneo hili ambalo nilitaka niseme na niishauri Serikali mfuatilie, ni utendaji wa barabara zinazotengenezwa.

Tuangalie sana, ikiwezekana Kamati ya LAAC inayoshughulika na Serikali za Mitaa, ipitie na iangalie *value for money*. Pesa nyingi inakwenda kwenye barabara, chukua mfano wa barabara mojawapo, kila mwaka labda inapelekewa milioni 30 mwaka, unaofuata milioni 30, baada ya miezi kadhaa ukifika pale barabara ile haipo. Tunatengeneza kwa utaratibu gani? Ninafikiri labda Wataalamu wa Wizara, wajaribu kubuni utaratibu, barabara ambayo ipo kwenye matengenezo ya kila mwaka, ina kilomita labda 12; kwa nini pesa tunazozitoa mwaka mmoja tusiende kuboresha kuweka moramu hata kilomita nne na mwaka unaofuata tukaweka pia kilomita 40 na hatimaye mwaka mwingine unapofika ile pesa itaonekana ilipofanya kazi? Tunapeleka milioni 30 mwaka mmoja, inakwanguliwa na greda inapita mpaka mwisho, miezi mitatu baadaye barabara haipo.

Chukua mfano wa Barabara ya kutoka Buntubili kwenda Buleba, ukiangalia kila mwaka pesa zinazokwenda pale, lakini pia barabara zinaendelea kuwa finyu kadiri mwaka unavyokwenda. Kwa hiyo, tunashukuru tunafungua barabara, lakini naomba usimamizi wa barabara zake uimarishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa Elimu, ndiyo maana nimempongeza pia Dr. Baleli. Mimi binafsi, katika Wilaya ya Bukombe, tumeingia madarakani pamoja, kwa sababu mimi nakuwa Mbunge yeye anakuwa Mkuu wa Mkoa. Tulikuwa na Sekondari tano, leo tuna sekondari 25 na katika sekondari 25, sekondari 23 tumejenga maabara ingawa hazijakamilika.

Ombi langu katika sehemu hii, mwaka jana tulipitisha bajeti ya kujenga maabara katika Mikoa katika sekondari zetu. Wilaya ya Bukombe, kwa taarifa nilizonazo, labda ambazo sizifahamu, hatujapata pesa ya kujenga maabara katika Wilaya ya Bukombe. Tumetumia pesa zetu zote za *Local Capital (LCGD)*, tulipozipata zote tulisema hazifanyi shughuli nyingine tunazielekeza kwenye maabara na hosteli. Naibu Waziri wa TAMISEMI anafahamu, alifika kule, naamini atakuwa shahidi.

Kwa hiyo, tunaomba mwaka huu mpeleke pesa za maabara, tukakamilishe maabara zetu. Kuna mchangiaji mmoja alisema asubuhi kwamba, tunapokuwa na yale majengo hayajakamilika, vile vifaa vyake siyo maabara. Tunayo majengo pale tunataka tuyakamilishe, kwa hiyo, ninaomba Serikali mtusaidie ili tuhakikishe kwamba, tunakwenda.

Naishukuru sana Wizara ya Fedha, mlitusaidia sana, benki ilikuwa kilio; Walimu wangu na Wafanyakazi wa Wilaya ya Bukombe, walikuwa wanatembea kwenda na kurudi kilomita 200 kufuata mishahara. Wanalala kule, wakirudi mshahara wote umekwisha, lakini sasa Benki ya NMB iko pale, tuwaombe na benki nyingine mje pale Bukombe; ni nzuri ina raslimali zake, ina machimbo wachimbaji wadogowadogo wengi na ina misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nipongeze hayo, lakini pia ninaomba sasa kuzungumzia matatizo mbalimbali, ambayo Wananchi wa Bukombe wamenituma. Mara nyingi huwa nasema, nina wananachi zaidi ya laki tano na kitu na hawa ninapozungumza ni sauti yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ni mara ya nne, ninasimama katika Bunge lako Tukufu, nikiongelea na kuomba umeme katika Wilaya ya Bukombe. Inawezekana leo Serikali ikisimama, wanapeleka umeme Bukombe. Katika Kitabu cha Mipango ya Maendeleo ya Mwaka 2009/2010, ukurasa wa 45, mpango wa mwaka 2009/2010 naomba ninukuu: "Kumalizia miradi ya kuweka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya zilizobaki hata katika Mikoa ya Kigoma, Rukwa, Mtwara na Lindi." Shinyanga haipo, kwa maana hiyo Bukombe pia haipo.

Mara nyingi tukiuliza Serikali wanasema mipango inaendelea, aidha, anatafutwa mkandarasi mshauri; huyu mkandarasi mshauri anakaa wapi? Bajeti ya Mwaka 2006/2007, mlisema pesa imepatikana na wafadhili wa SIDA wanakuja kuukamilisha mradi ule; mwaka 2007/2008 mkasema maneno yale yale; 2008/2009 hadithi zilezile; huyu mkandarasi anatafutwa kwa muda gani? Hapa ndipo tunapofika sehemu unaweza ukasababisha watu waanze kukosa imani.

Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Yussuf Makamba, alifika pale akawaambia Wananchi wa Bukombe, umeme utawaka. Naibu Waziri, alikuja pale akasema umeme Bukombe utafika na utawaka, ilikuwa ni mwaka jana, lakini mpaka leo tunapouliza tunaambiwa mkandarasi mshauri anatafutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili, Serikali ninaona kama vile inawadanganya Wananchi wa Bukombe; na tunapowadanganya Wananchi, hata katika maandiko Mungu

hapendezwi na hilo. Tunapotoa udanganyifu ndipo ghadhabu ya Mungu inashuka. Kwa nini tunalazimisha maneno haya katika Wilaya yetu ya Bukombe? Chama cha Mapinduzi, hakina jibu leo pale, mimi Mbunge sina jibu na Mkuu wa Wilaya hana jibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu na ushauri; tunashukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mwadilifu sana na hii ni kwa sababu ya hofu ya Mwenyezi Mungu; na kwa sababu hiyo bado hujaja Bukombe. Mimi nikuombe, kwa sababu unayo ile hofu uje uwaambie ni mojawapo ya kufanya ziara. Najua umeambiwa kila sehemu nenda, ukiona huwezi kupata nafasi ya kuja basi wape jibu tu Wananchi wa Bukombe Siku ya Alhamisi kwamba, umeme utawaka Bukombe au laah! Tunaamini majibu utakayoyatoa, wataelewa na kwa sababu tuna imani kubwa sana na wewe, tunaamini huwezi kusema umeme Bukombe utawaka wakati hauwaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ulikuwa ni ushauri wa kwanza. Ushauri wa pili, kwa sababu unasema pesa za ADB zipo, naomba mzipeleke kwenye account ya Brg. Dr. Balele, tutabanana kwenye RCC atapeleka mkandarasi haraka sana, kwa sababu labda Wizara hazifanyi kazi vizuri au mzipeleke wilayani kwa Mkurugenzi wangu.

**NAIBU SPIKA:** Inabidi apeleke Mkoani siyo kwa Dokta haitaeleweka!

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Sawa! Basi zipelekwe huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunisahihisha, lakini ninafikiri wamenielewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kilimo; Kilimo Kwanza na ndio kitawakomboa Watanzania. Ninaomba sana, tuboreshe kilimo kwa kuboresha maeneo husika; kwa mfano, Wananchi wa Wilaya ya Bukombe hawakopesheki, vijiji vyao vimepimwa havina vyeti, hawana hati miliki na wala hawana chochote; leo watapataje pembejeo? Tunaomba tuangalie uwezekano.

Naomba nimshukuru Mheshimiwa Wasira, alikuja pale akaona SACCOS ya Vijana Masumbwe. Wasaidie vijana wale, uwakopeshe pembejeo, kwa sababu unaweza ukawadhamini wewe au Wizara yako ili waweze kuwasaidia wakulima wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la wafugaji; tunaomba wafugaji watengewe maeneo. Katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi hili limeeleezwa, silitoi kichwani mwangu. Tunaomba Wafugaji wa Bukombe watengewe maeneo na nataka nieleze ni wapi walipotengewa eneo, yapo maeneo ambayo mara nyingi nimekuwa nikiyaainisha. Lipo eneo la Nyashinge kwenda Nyalugusu kwenye Jimbo la Busanda, lile litasaidia wafugaji wengi. Lipo eneo la Kerezia kwenda Bunzewe, hawa wafugaji wanapata shida, wananchi wanatekwa kila wakati pale. Nimeomba mpeleke Jeshi la Wananchi hamtaki, tengeni lile eneo liwe la wafugaji ili majambazi wasiingie pale. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee masuala mengine ya jumla. Watumishi wa Serikali hasa *Local Government*, ambao nakaa nao karibu, tofauti ya mshahara kati ya

Mkuu wa Idara na Wasaidizi wake ni kubwa mno, tunaomba mliangalie hili ili muwasaidie hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kengele imegonga, nakwenda haraka. Suala la ubambikizaji wa kesi; nimpongeze sana Mheshimiwa Lawrence Masha, Waziri wa Mambo ya Ndani, wamekuja pale walitusaidia zile hela tumemalizia kile kituo chetu kimejengwa vizuri sana na kinaendelea, nakuomba uende pale wakati wa ufunguzi tukakukabidhi ukione na utukabidhi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba, kuna wananchi wangu wamebambikizwa kesi na ninapoongea hapa ni kwamba, mimi nina ushahidi kwamba wamebambikizwa kesi. Nimemwandikia Mwanasheria Mkuu wa Serikali anasema, Ofisi ya RCO, haijamaliza upepelezi. Wao wanapeleleza kwa muda gani? Kesi za mauaji zinaonekana ni 67, walioua kweli wahukumiwe, lakini ambao hawajaua wameonewa. Wapo vijana pale Masumbwe, Chama cha Mapinduzi Tawi na Serikali ya Kijiji, imeniandikia barua inawatetea vijana, lakini kesi haziendi. Siku moja niliomba hapa nikasema, undeni Tume ikasaidie upelelezi mbona hamuundi mnatutakia nini sisi wanasiasa wenzenu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana hilo tulifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa Polisi, wako Mapolisi na wananchi katika Wilaya ya Bukombe wamefanya kazi nzuri sana katika zoezi la Maalbino, sijasikia hata siku moja wamepongezwa. Nilimwona RPC wa Kigoma akiwapongeza Maaskari wake, naomba muwapongeze Maaskari hawa waliofanya kazi nzuri. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ni ya Utawala wa Sheria, tena ni nchi ambayo tumelelewa vizuri sana na Baba wa Taifa. Tunaonekana nchi yetu sasa tunaipeleka mahali ambapo sipo, suala ambalo linasemwa wakati mwingine; mara sijui Rais Mstaafu Benjamin Mkapa ashtakiwe, mimi ninaona tunaipeleka nchi pengine sana. Rais huyo amefanya kazi kubwa sana katika nchi hii, simjui lakini namjua kama Rais wangu Mstaafu, lazima tulinde heshima yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la Bandari; mizigo inajazana pale Bandarini, kungekuwa na mfumo wa kutengeneza Bandari Kavu; kwa nini hatutengenezi ? Nilikuwa naomba niyaseme haya, lakini zaidi kuiomba sana Serikali, wakati Waziri Mkuu akihimitisha awaambie Wananchi wa Bukombe umeme utawaka lini ? Awaambie wafugaji kama wana maeneo yao pale Wilaya ya Bukombe 60% ni msitu, 40% ndiyo makazi, mifugo na kilimo …

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili hiyo Mheshimiwa.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, unajua unapojadili hoja hii, unaiambia Serikali, sasa kwa mfano Mheshimiwa Luhahula amesema kwamba, Mheshimiwa Wasira alikuja kule; alikuja kama Wasira au alikuja kama Waziri wa Kilimo ? Kama alikuja kama Waziri wa Kilimo, unamtaja kwa wadhifa wake, kwa mujibu wa Kanuni ya 60(16) na kuna faida ya kumtaja kwa wadhifa, hata akiondoka Waziri bado Waziri wa Kilimo alifika pale. Kwa hiyo, ndiyo umuhimu wake.

Tunaendelea na sasa nitamwita Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya na Mheshimiwa Richard Ndassa ajiandae na Mheshimiwa Malecela naye ajiandae.

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ningependa kumpongeza na timu yake yote, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuleta maendeleo katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naanza moja kwa moja, kwa kusoma ukurasa wa 56 Ulinzi na Usalama, kipengele cha 79.

Kinasema hivi, naomba kunukuu: "Kwa mwaka 2009/2010, Serikali itaendelea kulinda mipaka ya nchi yetu, pamoja na kuimarisha amani na utulivu nchini."

Mheshimiwa Naibu Spika, haya maneno ni mazuri sana, kwa Watanzania wanaopenda amani na utulivu na kujiletea maendeleo katika nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeyasema hayo, kwa makusudi kabisa; katika siku za hivi karibuni kumeanza kusikika maneno ya ajabu ajabu; watu wanaanza kuzungumza udini, watu wanaanza kutembea kifua mbele eti kwa sababu yeye ni Mkristu au yeye ni Muislam.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo siyo utamaduni wa Mtanzania hata kidogo na huko mnakotupeleka siko hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tungeiendesha nchi yetu kwa kutumia misingi ya dini, tusingepata uhuru hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako, naomba nikusomee majina ya watu ambao waliianzisha TANU katika nchi yetu na ninyi wenyewe mtajua kama kulikuwa na Waislam peke yake au kulikuwa na Wakristo peke yake na ndiyo walioleta uhuru katika nchi hii. Tarehe 07/07/1954, wazee hawa walikutana Dar es Salaam wakaamua kwamba, wanataka kuanzisha chama cha kisiasa cha kuikomboa nchi hii. *(Makofi)*

Moja; Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, ambaye alikuwa Rais wa TAA na baadaye TANU, Geremano Pacha, Joseph Kimalando, Japhet Kirilo, C. O. Milinga, Abubakar Langa, L. B. Makaranga, Saadan A. Kandoro, Suleiman M. Kitwana, Kisunju

Tagabara, Tewa Said Tewa, Dosa A. Aziz, Abdul Sykes, Patric Kunambi, Joseph K. Bantu, Ali Sykes na John Rupia. *(Makofi*)

Hawa ndiyo wazee waliokaa wakasema tunataka kudai uhuru katika nchi yetu na ninyi mmeyasikia majina haya; ndani yake kuna Waislam na kuna Wakristu. Mwalimu Nyerere, akaikubali hali hii akafanya nao, tarehe 9 Desemba tukapata uhuru wa nchi yetu. Ninyi leo ndiyo mtupeleke katika Ukristu au Uislam? Mnatoka wapi; mnatoka katika nchi hii ya Tanzania au mnatoka nchi nyingine? Nasema hivi; kama wewe ni mmojawapo unayezungumzia udini, ujue kwamba, huna chochote na wala hatukusifu kwa hilo, unataka kuiangamiza nchi hii. Hatutaki udini wala ukabila na hatutaki tofauti ya rangi, msitupeleke mahali pabaya ambako siyo kwetu; nawaomba sana. *(Makofi*)

Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, alikwenda Afrika ya Kusini, akakaa katika meza ambayo wao walifikiri hakutarajiwa kukaa pale kwa sababu tu ni Mhindi, akawaambia mimi ni Mtanzania na huko Bombay sikujui, wakamwacha hapo hapo. Maana yake nini? Maana yake ni kwamba, wale kule wanapimana kwa rangi, udini na ukabila, lakini sisi hatupimani kwa hilo. Hivi mifano hatuioni?

Lebanon wamepigana miaka 15, Muislam na Mkristu, hakupatikana mshindi hata mmoja. Walifika mahali wakatazama kama kuku, wakajiuliza hivi sisi tunafanya kitu gani cha ajabu hiki? Sote sisi ni Waarabu, tuache kupigana bila sababu, hizi ni imani tu, nani aliyethibitisha kama Mungu yupo hapa? Ni imani ya roho tu, kila mmoja amwache mwenzake na imani yake. Leo Lebanon wanapata tabu ya kujenga nchi yao, mnataka na sisi tufike huko? Eti unatembea barabarani unasema mimi ni Mkristu au mimi ni Muislam utaniona; kitu gani?

Rwanda hapa wamepigana kisa ukabila tu ! Mnyarwanda na Mtutsi wana tofauti ndogo tu; mmoja ana pua pana na mwingine ana pua ndefu, basi wote ni binadamu; ndiyo mnataka kutupeleka wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema acheni mara moja, mpimeni mtu kwa tabia yake na siyo kwa udini, ukabila wala rangi. Hatutaki kuiangamiza nchi yetu hata kidogo katika hilo. Utaratibu wa kuzungumzia matatizo yetu tunaujua upo, tunaogopa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba sana wale wenzetu ambao wanaanza kuchomoza vichwa kwa kutumia ukabila, udini na rangi, waache kuanzia leo hii. Tutakuja kuwajua tu, hata kama mtajificha tutawajua na tutawaambia ninyi mnataka kuiharibu nchi yetu hamtakwepa hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, na mimi ningependa kuzungumzia maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuipongeza Serikali kwa uamuzi wa makusudi kabisa wa kuondoa Stevedoring katika Bandari ya Mtwara. Kitendo hiki ni kizuri sana, kwa maana ya kwamba, Bandari ya Mtwara itachangia katika maendeleo ya nchi yetu. Tulikuwa tunajichelewesha makusudi, ninachoomba kuanzia sasa waambie

Mashirika ya Meli kwamba, sasa mnaweza mkapeleka bidhaa zenu moja kwa moja mpaka Mtwara na katika hili, hata matatizo ya Bandari ya Dar es Salaam, ambayo sasa tunayo yataondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuna bandari nyingi sana katika Tanzania; tuna Mtwara, Lindi, Dar es Salaam, Bagamoyo, Tanga na Zanzibar ni matajiri sana. Leo wenzetu Kenya wameligundua hili, wameanza kujenga Bandari ya Lamu ili wachukue bidhaa zote za Rwanda, Burundi, Congo na Zambia, lakini sisi hapa tayari Bandari hizi tunazo.

Ule mpango ambao upo Serikalini wa kutaka kufufua bandari zetu, naomba sana ule mpango uharakishwe usichelewe. Kama ni wewe mwenyewe Mheshimiwa Waziri Mkuu au kama atakuja Waziri anayehusika, aje kutueleza hapa ule mpango umefikia wapi? Wakati ni huu tusichelewe, watatuacha na watatucheka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi hapa nimekuwa nikizungumza ama nikiikumbusha Serikali kuhusu matatizo ya maji katika Jimbo langu la Lulindi. Katika maeneo ya Chingutwa, Luatala na Namombwe, wana matatizo makubwa kabisa ya maji. Miaka miwili au mitatu iliyopita, Serikali iliahidi kuvifufua vyanzo vya maji na kwa kutoa gharma ya pesa, lakini mpaka hivi sasa ninavyozungumza, bado hakujafanyika kitu chochote. Mara nyingi hapa nikisimama kuuliza swali la nyongeza, huwa hunipi nafasi, sijui unajua kwamba nataka kuuliza maswali ya maji?

Chanzo cha Maji cha Mkululu, Chiwambo na Lupaso, Serikali iliahidi kufufua na pesa mlizitenga, lakini mpaka leo hii hakuna kilichofanyika. Mmefanya kazi nzuri, tumejenga shule nyingi sana katika Jimbo la Lulindi katika Kata zote 14. Kuna shule ya sekondari, tunajenga zahanati na wananchi wako tayari kujitolea, lakini hili la maji bado linatusumbua sana.

Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, wewe ni mchapakazi, ninakufahamu sana, kama walivyozungumza wengine, hili suala litakwisha kabla hatujaingia katika uchaguzi. Mheshimiwa Waziri Mkuu na mimi nataka kurudi Bungeni hapa, ndiyo maana ya kusema ukweli lisije likaniletea matatizo. Naomba suala hili litimizwe kwa sababu tu Serikali iliahidi kwamba, watapeleka pesa hizi tangu wakati wa Waziri Mheshimiwa Mwangunga. Kwa hiyo, naomba sana ahadi ile itimizwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kuipongeza Serikali kwa kazi yake nzuri ya kuleta maendeleo katika nchi hii na mimi nataka kuungana na Mheshimiwa Rais wetu Jakaya Kikwete aliposema, Shinyanga wala msiwe na wasiwasi jamani 2010 tutapeta tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na sasa nitamwita Mheshimiwa Richard Ndassa, atafuatiwa na Mheshimiwa John Malecela na Mheshimiwa James Lembeli ajiandae.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi jioni hii na mimi nichangie hoja iliyopo mbele yetu.

Kama ilivyo kawaida, naomba na mimi nitamke kwamba, naiunga mkono Hotuba ya Waziri Mkuu kwa asilimia zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kama ifuatavyo: Niwaombe sana wenzangu au wenzetu walioko ndani na hata waliopo nje, haipendezi sana, Viongozi wa Tanzania tunaposimama tunaanza kutoa kejeli kwa Marais wetu Wastaafu. Kwa wale tulioingia Bungeni mwaka 1995, tuliingia na Rais Benjamin William Mkapa, nchi yetu haikuwa hivi hata kidogo. Kama huna shukuran, basi wewe bora unyamaze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1995, nchi yetu ya Tanzania haikuwa hivi hata kidogo, nawashangaa wale wanaosahau. Mnyama mwenye tabia ya kusahau ni Ngiri peke yake; Ngiri hana kumbukumbu hata kidogo, anakwenda shambani anamkuta mwindaji anamkosakosa bunduki, atakapotoka hapo *speed* yake kilomita 100 kwa saa, lakini akisimama anatikisa kichwa anajiuliza; ilikuwa jana au juzi? Ndugu zangu, nawasihi sana tena sana, sisi Watanzania tabia yetu siyo kama ya Ngiri kusahau. Tumwache Rais Mstaafu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa huko alipo na nimwambie kwa sababu inawezekana anasikia huko aliko, tulia kunywa whisky yako taratibu na kwa amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirejee kwenye mada yangu sasa, huo ulikuwa utangulizi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, wewe ni mtoto wa mkulima na ndivyo tunavyokujua. Mimi natoka Mkoa wa Mwanza; Mkoa wa Mwanza ni Mkoa wa Wakulima, samaki wamekuja baadaye. Nimetumwa nikuombe na niiombe Serikali, tuwatendee haki Wakulima wa Zao za Pamba wa Mkoa wa Mwanza na Wilaya nyingine zote 42, kwa sababu zipo Wilaya 42 zinazolima Zao la Pamba katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukubali tusikubali, kwa bei ya shilingi 360 kwa kilo moja kwa mkulima huyu aliyelima kuanzia Desemba au Oktoba mpaka leo mwezi wa sita shilingi 360 kwa kilo, mkulima huyu hawezi kunenepa hata siku moja, ataendelea kukondeana kila siku, lakini ile tija ambayo alikuwa anaitafuta hawezi kuipata.

Naiomba sana Serikali, iangalie kwa makini suala hilo. Katika zile trilioni 1.7, ichukue shilingi bilioni 20 ijazie ili badala ya kilo moja ya pamba kuuzwa shilingi 360, iwe shilingi 440. Serikali iongezee senti 80 na kwa bajeti tuliyopewa sasa hivi ni kwamba, kwa mwaka huu tani 250,000 zitapatikana. Kwa maana hiyo, tukizidisha tani 250,000 mara senti 80, tutapata shilingi bilioni 10. Serikali kuchukua shilingi bilioni 20 kuwapa wakulima wa Wilaya 42 katika nchi hii wala sio hasara, tutakuwa tumewasaidia angalau na watasema Serikali yao inawajali. Tumewajali hawa wanunuzi wa pamba, waliokwenda kukopa fedha zao Benki, basi na wakulima nao tuwajali. Tukifanya hivyo, tutakuwa tumejijengea heshima kwa nchi yetu. Bahati nzuri kwa sababu mwakani ni uchaguzi, tusipofanya hivyo, hawatakuwa na imani na Serikali yao. Baya zaidi, inawezekana wakulima hawa mwakani wasilime tena pamba, kwa sababu ya bei ambayo ipo chini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshauri Mheshimiwa Waziri Mkuu; wewe kama mkulima nikuombe sana, Serikali ilitazame hili kwa haraka na liwe la dharura kwa sababu msimu umeanza jana, si vibaya Serikali ikaingilia. Bahati nzuri na Waziri wa Fedha yuko hapa, Waziri Mkuu yuko hapa na Serikali yote iko hapa, hii ni kwa sababu ya dharura. Jana wameanza kuuza pamba, endapo itaendelea hivi basi wataleta matatizo kwa wakulima wetu. Watoke kwenye shilingi 360 kwa kilo moja waende shilingi 440, angalau itasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango wa ugawaji matrekta kwenye vituo vyetu tulivyoviona hivi, sijui labda *criteria* mliyotumia ya kugawa matrekta; Kanda ya Ziwa kwa maana ya Mara, Shinyanga, Mwanza na Kagera, hata trekta moja hakuna kati ya matrekta 55. Matrekta yameenda sehemu nyingine; Mara, Mwanza, Shinyanga na Kagera hakuna. Pamoja na uchache wa hayo matrekta, hivi kweli Mwaza hata trekta moja hakuna; kweli inawezekana? Mnatupa tu *power tillers,* hizi *power tillers* mpaka ule ushibe ndiyo uziendeshe, bila kushiba huwezi, kwa sababu zinatumia nguvu nyingi zaidi na tukimuuliza Mheshimiwa Profesa Mwakyusa hapa, wale wanaotumia hizi *power tillers* ukiwapa miaka mitano sijui. *(Kicheko*)

Nashauri Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunapopanga mambo haya, pengine hatupendi sana kulalamika, lakini inapotokea namna hii mnajiuliza; hivi kweli Kanda ya Ziwa hata trekta moja hakuna?

Ukitazama humu, hata zile *power tillers* maskini ya Mungu, mikoa mingine imepewa nyingi kweli kweli. Sasa tunajiuliza; hata tunaposema hii keki yetu ni ya upande mmoja au ya upande gani? Sitaki kuwa mbaguzi lakini ni vizuri zaidi tunapofika pale tunapogawa hii keki yetu, lazima tuigawe kama inavyotakiwa kila Mtanzania apate haki yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, nimwombe Waziri wa Viwanda; kwa sababu ununuzi wa pamba umeanza jana; na watu wetu wanaibiwa mbegu na pia wanapunjwa kwenye kupima pamba, naomba sana mizani ambayo iko kule, Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara, iihakiki mizani hiyo ili angalau wakulima wetu wasipunjwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala zima la kilimo cha umwagiliaji. Naomba sana Serikali ifanye utaratibu wa makusudi na iamue, huwezi ukazungumzia umwagiliaji kwa kutegemea mabonde. Wenzetu mlioko mbele mnasafiri sana, ukiwa angani kule unaona kuna mabwawa na malambo. Ukikaribia kwenye mji unaona mabwawa na malambo. Yale malambo ni kwa ajili ya umwagiliaji, sasa sisi tunazungumzia tu mabonde, kilimo cha umwagiliaji hakiko namna hiyo.

Sambamba na hilo, bila kupanda miti, hatuwezi kupata mvua za kutosha. Tunaiomba serikali ilete sheria kama haipo. Unapopanda mti, unaukataje huo mti baada ya siku mbili au tatu? Nchi nyingine wanafanyaje? Maana yake lazima tuige yale mazuri, ukipanda mti ndio wa kwako, lakini ukishanza kukua sio wa kwako. Ndio maana maeneo mengine, kwa takwimu za sasa ambazo sio rasmi, upandaji wa miti na ukataji ni mkubwa zaidi kuliko miti inayopandwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapa, lakini niiombe sana Serikali kuhusu suala zima la pamba; mimi ni mdau wa pamba kama ulivyo wewe Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mfugaji mzuri na ni mkulima mzuri. Wananchi wa Jimbo la Sumve, Wilaya ya Kwimba, Mkoa wa Mwanza, zao lao kubwa wanalolitegemea ni pamba. Bei ndiyo hiyo, naomba hii iwe dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nataka kuchukua nafasi hii, kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa jinsi ulivyoanza na *speed* nzuri na kazi yako, tunasema ukiendelea namna hii, utakwenda kwenye rekodi ya watumishi bora wa Tanzania. *(Makofi)*

Nakupongeza sana wewe, nampongeza Mheshimiwa Celina Kombani na Mheshimiwa Mwanri kwamba, mmeifanya Ofisi ya Waziri Mkuu kuwa, ofisi ambayo inafanya kazi, ofisi ambayo ni sikivu kwa matatizo ya watu na ofisi ambayo watendaji wake wako kwenye *field* kila wakati. Nasema endeleeni na moyo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ningependa kuchukua nafasi hii, kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Nne. Mimi kama mtu ambaye ninatoka Dodoma, nataka nichukue nafasi hii, kwa niaba ya Wananchi wenzangu wa Dodoma, tumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais Kikwete, kwa kuamua Chuo Kikuu cha Dodoma kijengwe Dodoma. *(Makofi)*

Tunawashukuru Watanzania wenzetu kwamba, hakuna mtu yeyote katika nyumba hii au nje, ambaye amewahi kulalamika kwa nini Chuo hiki kijengwe Dodoma. Tunasema kwenu wote, ahsanteni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi kwa Rais; tunasema katika ulimwengu huu, watu hawakumbukwi kwa miaka waliyoishi, wanakumbukwa kwa maamuzi au vitendo ambavyo vimebadili hali ya nchi. Kwa sisi wa Dodoma, tunamwombea Mheshimiwa Kikwete, maisha marefu, lakini tunasema kwa kitendo chake cha kuamua Chuo hiki Kikuu kiwe Dodoma, atakumbukwa daima. Labda niseme kwa lugha ya kigeni; *He will be remembered as long as the University of Dodoma is where it is*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuongezea kwamba, kwa wale Watanzania wenzagu ambao walifika Dodoma labda miaka minne, mitano iliyopita, wakija Dodoma mahali pa kwanza pa kwenda kuona Serikali ya CCM imefanya nini, waende kwenye Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa sasa niende kwenye suala la Kilimo Kwanza. Kweli ninakubali Kilimo Kwanza, narudia Kilimo Kwanza, lakini kwa Tanzania, bado kilimo kinategemea mvua. Ukiangalia katika Jimbo la Mtera au katika

Wilaya ya Chamwino, watu tangu walipopanda mbegu mwezi Novemba, 2008, bado mashimo yako vilevile, mwaka huu hatutahitaji kuchimba mengine, tutatia mbegu kwenye yale tuliyochimba mwaka jana. Sasa hapa ukisema Kilimo Kwanza, maana yake nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna mahali ambapo Serikali ingeangalia kwa makini, kilimo cha umwagiliaji basi kiwe Mkoa wa Dodoma, la sivyo, kila siku mtakuwa mnafikiria kutuletea chakula cha njaa; jambo ambalo ni la aibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa sasa nitoe mapendekezo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, kwa Mkoa wa Dodoma ni lazima mjitayarishe kutuletea chakula. Mimi ningependa nibadili hili jina la kusema Chakula cha Njaa; ni la aibu. Tuleteeni Chakula cha Kazi; mtu akifanya kazi apewe chakula.

Hata kwenye Biblia inasema, asiyefanya kazi na asile. Sasa mmeleta mtindo ambao unaleta matatizo nchini kwamba, eti muwape Watendaji wa Vijiji wakauze kwa bei nafuu. Unamuuzia mtu, kama Dodoma hapa mwaka huu mvua haikunyesha kabisa, huyo utakayemuuzia bei nafuu hela atazipata wapi? Kinachotokea sasa hivi, Watendaji wanachukua chakula wanawauzia matajiri, wanakata hela ambazo wanatakiwa kurudisha, wanarudisha nyingine wanatia mfukoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema tukitaka haki, tupate Chakula cha Kazi. Tuangalie miaka ya nyuma, tunayo mabwawa mengi, ambayo yamejengwa kwa Chakula cha Kazi, tunazo shule nyingi ambazo zimejengwa kwa Chakula cha Kazi na sasa hivi tunao Watendaji wengi ambao wako Mahakamani, kwa sababu wamekula hela za chakula cha bei nafuu. Kwa hiyo, badala ya chakula cha bei nafuu, mimi ningesema walete Chakula cha Kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, ningependa niende moja kwa moja kijijini. Hebu niliulize Bunge hili, tangu Baba wa Taifa atuachie vijiji, tumebadili kitu gani? Hakuna wala hatujawahi kufikiria hivyo. Tutengeneze kitu gani cha kuleta mabadiliko ya haraka? Kama ni Serikali ya watu 25, kama ni Mtendaji wa Kijiji bado ni yule yule, halafu huyu Mtendaji wa Kijiji ndiyo tunamtazamia aangalie kazi zote pamoja na mahesabu ili awasomee Wanakijiji, amekusanya hela ngapi na ametumia kiasi gani. Kwa kweli mimi ninasema, hili ndilo linalofanya vijiji vyetu visiendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Waziri Mkuu, kwanza tufikirie watu wawili ambao pengine tungeweza kuwaongeza katika kijiji. Kwanza, mjuzi wa fedha, ambaye kazi yake itakuwa kushughulikia mapato na matumizi ya Kijiji tu. Sasa huyu hata mambo ya mahesabu na kila kitu, tukimwambia atoe itakuwa ni haki kuliko sasa hivi; Mtendaji wa Kijiji kumpa kazi zote hizo ambazo anashindwa kuzitimiza.

Mtu wa pili ambaye anahitajika kwenye Kijiji ni mtu wa Mipango. Tupeleke mtu anayeijua fani ya Mipango. Sasa hivi tunawaambia wanavijiji ibueni miradi, sasa wataibuaje kama hawana mtaalamu wa kuwasaidia katika kuibua miradi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakwenda kwenye jambo lingine; twende kwenye Serikali za Mitaa. Katika Kwenye Serikali Kuu, ukusanyaji wa fedha tumekwishaubadili, tuna TRA na TRA ni sehemu ya Serikali Kuu, lakini kwenye Serikali za Mitaa, tunakwenda tunawaambia nendeni mkatafute mawakala na mahali pengine, mawakala tunawaambia tulipeni kwanza milioni 10 halafu nendeni mkazitafute huko. Hivi hii *system* ya kutangaza mawakala binafsi wakusanye hela za Serikali mmeipata wapi?

Mimi ningeomba; kama tumeweza kuunda TRA kwa ajili ya Serikali Kuu, Serikali za Mitaa nazo tuzifikirie, tuunde chombo kamili, ambacho kitazisaidia kukusanya fedha. Tusipofanya hivyo, kila wakati tutakuwa tunawalaumu kwamba, hawakusanyi fedha za kutosha na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa niliseme ni la utendaji katika Halmashauri zetu. Utendaji katika Halmashauri zetu, unategemeana na mafunzo ambayo watendaji wetu wameyapata. Kwa hiyo, ningependa niseme kwamba, sio kana kwamba, Serikali haifanyi; ni kweli Serikali inafanya, lakini ningependa niombe zaidi, Serikali iwafundishe watumishi zaidi wa Serikali za Mitaa, ili Serikali zetu ziweze kuwatumikia wananchi wetu kama inavyostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingependa kengele ya pili inililie tena; nataka nirudie kwamba, wakati umefika, sisi Watanzania ikiwezekana hata tuunde Tume, iende ikaangalie Vijiji vyetu, tufanye nini ili viweze kupata mabadiliko ya haraka. La sivyo, tunafika mahali tunasema aah Ujamaa huu, Vijiji vya Ujamaa vilileta kugawana umaskini, hapana. Vijiji vya Ujamaa katika Afrika nzima, sisi Watanzania ndio watu tu tunaoweza kuleta maendeleo ya haraka kwa watu wetu wote kwa sababu wanaishi mahali pamoja. Ningependa niseme kwamba, tutengeneze sheria mpya. Kwa mfano, sasa hivi wanasema ooh, Mtanzania yeyote anaweza kuishi mahali popote. Ndiyo, lakini mtu anakuja kuishi popote kwenye vijiji; sio kuishi popote, mtu anakwenda kujichopeka katikati ya pori, halafu anasema yeye ana uhuru wa kuishi mahali popote. Sasa haya hayawezi kufanyika mpaka Sheria mpya itungwe. Kwa hiyo, mimi ningeomba, Sheria ya Vijiji iangaliwe upya, tuitunge upya ili baadhi ya haya mambo ambayo yanatupunguzia kasi ya maendeleo, yaweze kutuletea maendeleo ya haraka katika vijiji vyetu, tupate neema na tuweze kusema sasa maisha bora kwa kila Mtanzania yanawezekana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakupongeza tena kwa kazi unayoifanya na napenda kurudia tena kwamba, naunga hoja mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii jioni ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze mchango wangu, kwa moyo wa dhati kabisa, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kahama, kuishukuru Serikali ya Awamu ya Nne, kwa kutekeleza ahadi yake ambayo aliitoa Mheshimiwa Rais, wakati wa kampeni

kwamba, Serikali ya Awamu ya Nne, itajitahidi kuhakikisha kwamba, Wananchi wa Mji wa Kahama, wanapata maji kabla ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maji Kahama sasa yanatiririka. Tatizo la maji ambalo Wananchi wa Kahama na maeneo ambako bomba limepita kutoka Ziwa Victoria, sasa litabaki kuwa historia. Naishukuru sana Serikali ya Awamu ya Nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi zangu nyingine nyingi za dhati ziende kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati akizindua Mradi wa Maji pale Kahama, alitoa fursa ya miezi mitatu mingine kwa Wananchi wa Mji wa Kahama, kuweza kuunganisha mabomba katika nyumba zao kwa bei nafuu ambayo ilikuwa imetolewa na Serikali. Wananchi wa Mji wa Kahama, wanamshukuru Rais na wanamwomba aendelee kuwa na moyo kama huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niipongeze tena Serikali, kwa uamuzi wake wa busara iliouchukua wiki iliyopita wa kuondoa ile hoja ya kodi kwa Taasisi za Dini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inadhihirisha wazi kuwa, Serikali ya CCM, Serikali ya Awamu ya Nne; ni Serikali sikivu. Baada ya Wabunge wengi kulalamikia hoja hiyo, Wananchi na Viongozi wa Dini, Serikali ilichukua uamuzi ambao mimi kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kahama, ninaupongeza kwa moyo wa dhati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi, sasa nakuja kwenye hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mkoa wa Shinyanga na Mikoa yote ya Kanda ya Ziwa, ambako madini yanapatikana, madini ni siasa. Mimi kama Mbunge, madini ni kero na ni kichefuchefu kwa wananchi ambao madini yanapatikana kwao. Madini ni majonzi, yanaendeleza huzuni miongoni mwa wananchi na ni balaa. Usiombe eneo lako wewe kama Mbunge, yapatikane madini halafu wawekezaji waje pale kuchimba hayo madini, ni balaa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mkosi kwa sababu jambo hili limeleta mahangaiko makubwa na mengi kwa wananchi hasa wa Kata ya Mwendakulima katika Jimbo langu la Kahama. Napenda nianze kwa kunukuu maneno ya Rais wa zamani wa Czechoslovakia ya zamani, ambaye alikuwa anaitwa Haver kwa jina moja; yeye anasema hivi: “Siasa hasa siasa zinazostahili kuitwa siasa, siasa pekee ambayo niko tayari kuitumikia ni suala la kuwahudumia wananchi wanaonizunguka, kuihudumia jamii na kuwahudumia wale watakaokuja baada yetu, mizizi yake ni uadilifu kwa sababu ni wajibu unaoelezwa kupitia vitendo kwa ajili ya wote.”

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeamua kunukuu maneno haya kwa sababu mtu huyu alikuwa mkweli, mwadilifu na mzalendo kwa nchi yake. Nami napenda niseme ndani ya ukumbi huu kwamba, mimi ni mkweli na naipenda nchi yangu, lakini kwa

sababu hii ni awamu yangu ya kwanza kuwa Mbunge, nilichogundua ukiwa mkweli utapata matatizo makubwa. *(Makofi)*

Kwa hili nataka niseme Mgodi ule wa Buzwagi, pamoja na nia njema ya Serikali, umeleta mahangaiko na matatizo makubwa sana kwa wananchi wale. Wapo wananchi ambao wana madai ya kweli na dhati, nathubutu kusema Serikali haiwasikii. Mwaka jana ndani ya Bunge hili, nilipiga kelele baada ya wananchi waliokuwa wakidai haki zao kukamatwa, wakawekwa ndani na kwa hekima ya Waziri Mkuu, walitolewa ndani. *(Makofi)*

Waziri Mkuu, aliagiza Waziri wa Nishati na Madini, aende kushughulikia suala hilo. Alifika mwezi Mei na baadae Naibu Waziri akaja mwezi Agosti, akatoa ahadi nyingi kwa wananchi na kwa sababu ya uzalendo wao na kuipenda nchi yao, walimsikiliza Naibu Waziri. Tangu Naibu Waziri ameondoka mwaka jana mpaka hii leo, hakuna kitu; wananchi wale wanaishi kwa matumaini sasa sijui Serikali inangoja tena wananchi wale waende wakakate uzio halafu ndiyo iwasikilize!

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna madai ya msingi; Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi wa Kata ya Mwendakulima ni mfano mmoja. Huyu alitakiwa kulipwa shilingi milioni 51, amesaini *payment vocher* shilingi milioni 51, CRDB Benki amekuta shilingi milioni 18. Naibu Waziri wa Nishati na Madini analijua hili, alipowauliza Buzwagi wakasema hata wao wanashangaa. Mpaka leo huyu mzee hajaweza kupatiwa haki yake ya shilingi milioni 33 walizopora.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema madini kwa Kahama, nina hakika kwa Geita pia ni siasa. Kama serikali imeshindwa kuwasikiliza na kuwasaidia hawa wananchi waweze kupata haki zao, wanategemea nini mwaka 2010? Buzwagi ni kilomita saba kutoka Kahama Mjini.

Nikiondoka hapa kwenda jimboni kwangu napita Buzwagi, mara nyingi napita usiku, kwa sababu sipendi kuona wananchi wakiwa wamekaa pale na nyuso za huzuni. Mheshimiwa Waziri Mkuu, vijana wako uliowatuma kule hawajafanya kazi na mimi nitakuwa wa kwanza kusema kwamba, nasita kuiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja kama wananchi wale hawatapewa majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu sio wastaarabu, wanapoomba mradi au wanataka kuwekeza, wanakuja na kila aina ya kuonesha kwamba ni wastaarabu. Juzi Rais amekuja pale Kahama Mjini, barabara za Kahama Mjini zinaharibiwa na hawa watu. Asilimia 95 ya uharibifu wa barabara za Kahama Mjini, unafanywa na malori au magari ya Buzwagi na watumishi wa Buzwagi. Barabara ni mbovu, Halmashauri haina uwezo wa kuzitengeneza hizo, tumewaomba tengenezeni walau barabara moja atakayopita Mheshimiwa Rais wamekataa. Hawa ni watu wa namna gani; lakini wana vi-*offers* mbalimbali na vyote hivi vya kuwajaza viongozi wanawavisha miwani ili waweze kuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, wanasema nitachangia hoja yangu hii ya madini tu basi. Wanasema viongozi wote wa Kanda ya Ziwa, Kahama, Shinyanga, mkitaka kwenda kwenye majimbo yenu, mnapanda ndege bure. Kuna kindege pale kutoka Dar es Salaam kinafika Kahama kila siku. Mimi nasema nimepanda mara mbili na hiyo ndiyo ilikuwa mara ya mwisho mpaka nitamaliza Ubunge wangu sikai kwenye hiyo ndege. Wanakupa viti halafu *at the end of the year*, ukitazama kwenye huduma za jamii, wanaweka pale shilingi 20,000,000; ukiwauliza nini hii, wanasema Mbunge alikaa kwenye ndege kwenda kwenye jimbolake! Hili ni tatizo kubwa. Ukipita barabarani utajisikia furaha, lakini mahangaiko ya wananchi huko chini ni balaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Zao la Pamba ndio uti wa mgongo wa uchumi wa Wananchi wa Jimbo la Kahama, Wilaya ya Kahama na Kanda ya Ziwa. Bei ya pamba iliyotangazwa juzi ya shilingi 360 haikidhi. Ni jambo jema kwa Serikali, kuwafidia wafanyabiashara kwa hasara waliyoipata kwa kununua pamba mwaka uliopita. Wananchi hao hao ambao mwaka jana waliuza kwa shilingi 400, walilima pamba kwa kutegemea kwamba, bei itakuwa shilingi 400 au 500. Leo bei ya pamba imeteremka mpaka shilingi 360 na ninavyozungumza, wananchi wale wameshakata tamaa wanafidiwa na nani. Tunasema Tanzania ni nchi ya wakulima na wafanyakazi; kwenye hili la fidia aliyeangaliwa zaidi ni mfanyabiashara. Hili si jambo jema, naomba suala hili mliangalie kwa macho mawili, vinginevyo mwaka ujao tutapata matatizo makubwa sana, sisi tunaotoka Kanda ya Ziwa ambako pamba inalimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani, mtu amewekeza kwenye mbolea na sisi wenyewe tunapita kuwahamasisha walime pamba. Bei ya pamba inavyoteremka, tunakaa kimya! Nikienda jimboni kwangu nikiulizwa wewe Mheshimiwa Mbunge mwaka jana ulipita hapa ukahimiza tulime pamba, tumelima hii pamba yetu ndiyo thamani yake shilingi 360, jibu hakuna. Ukiwa mkweli utaeleza na ukieleza ukweli huitakii mema CCM. Mimi naiomba Serikali isikie kilio hiki cha wananchi, bei ya pamba walau ifikie shilingi 400 itatusaidia, lakini pia itawapa motisha wananchi hawa mwaka huu walime tena pamba. Mimi naamini pamba itaendelea kulimwa duniani mpaka mwisho wa dunia. Kwa sababu vazi lililotengenezwa kwa pamba, asilimia mia moja ni vazi safi na wanaovaa vazi hilo ni watu waadilifu. Sasa ninaomba sana nimalizie kwa kusema, matatizo yanayowakabili Wananchi wa Kata ya Mwendakulima pale Buzwagi, naomba sana yazingatiwe, wapewe haki yao wasinyanyaswe tena. Majuzi wananchi katika tafrani ya wizi wameua askari wa mgodi, wakakamatwa wako ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu na Waziri wa Serikali za Mitaa. Kabla sijasema lolote, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambao kwa namna nyingine wamekuwa ni Jimbo langu la Uchaguzi katika Bunge la Afrika, naomba niwashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitawashukuru tena tutakaporudi mwaka 2010, kwa sababu Ubunge wangu wa Bunge la Afrika unaendelea mpaka 2010. Kipindi cha miaka mitano kimekwisha salama na timu yetu ya watu watano, tuliokuwa tukiiongoza mimi na Makamu wanne kutoka katika Kanda nyingine za Afrika, tumekabidhi madaraka kidemokrasia kwa wale ambao wamechukua nafasi yetu. Rais wa sasa anaitwa Idriss Mussa kutoka Chad, ambaye nimeshaanza kufanya naye kazi kwa karibu na tumerudi hivi karibuni kutoka kwa Mwenyekiti wa Afrika, mimi na Mwenyekiti mpya, kumkabidhi kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika. Nataka niwahakikishie, Watanzania waliopo katika Bunge lile pamoja na mimi, tumejitahidi kwa uwezo wote tuliokuwa nao, kulijenga Bunge lile kuwa ni Bunge la Demokrasia, Bunge linalofuata sheria na utaratibu na sasa wenzetu tumewakabidhi wafike hatua katika kutatua matatizo mengi yanayoikabili Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme kwa haraka haya yafuatayo:-

Kwanza, naomba niwasilishe kwa Waziri Mkuu, maombi niliyokabidhiwa tarehe 15 nilipokuwa jimboni, nilipopokelewa kwa umati mkubwa wa wanajimbo ambao walifurahi sana kwamba, mimi nimepata sasa muda wa ziada kuwatumikia. Mwalimu Msiba wa Nansio, Kata ya Kagera, alisema Mama pensheni haitoshi. Waziri Mkuu umejibu, ahsante sana. Haijawahi kutokea pensheni ikaenda mara mbili, tunaomba tukushukuru sana na ambao hawakusikia hotuba yako, tunaomba wairejee tena hasa humu humu Bungeni kuona kwamba, Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi, inafanya kazi kwa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Ukerewe pia wameomba nifikishe salamu na shukrani za umeme. Sasa hivi umeme hauwaki katika Mji wa Nansio tu, lakini unawaka katika vijiji karibu vyote katika Kisiwa cha Ukerewe. Kwa maamuzi ya kuangalia maeneo yenye mazingira magumu, tumepata matumaini tena ya kwamba, shule zetu za sekondari, zahanati zetu zilizoko katika visiwa vingine kama vile Burubi, Irugwa, Ukala, Nakokote, Ghana, Zeru; nikivitaja ni vingi zaidi ya 28, wamepata matumaini makubwa. Waziri Mkuu, naomba nifikishie salamu hizo ambazo nimepigiwa simu za matumaini kwa Wananchi wa Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkuu, pamoja na timu yake, wametoa hotuba ambayo sisi ambao ni walimu, tunapaswa tuiandikie *scheme of work* na *lesson plan*. Maana yake NI kwamba; si hotuba ya kujadili hapa na kuiacha hapa; ni hotuba ya kwenda kusema haya katika *topic* ya Kilimo Kwanza ni nini kinafanyika, tarehe ngapi kwa kutumia vielelezo vipi na mbinu zipi za kufanyia kazi. Nadhani hiyo ni kazi ambayo bado iko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kilimo Kwanza, ningeomba niulize; hivi nishani zimekwisha? Kwa nini Kigoma wasipewe nishani? Kwa nini Mkuu wa Mkoa anasifiwa kwa maneno; hivi nishani za utumishi uliotukuka zimekwisha?

Mimi naishia hapo. Kama zipo wapeni watu walioitumikia nchi hii, wakaonyesha njia, lakini ningeomba pia vyombo vya habari vitusaidie. Wakati wa Siasa ni Kilimo kila mtu alijua vijiji bora katika nchi hii, kwa sababu vyombo vya habari vilikuwa vikitangaza. Siku hizi tunasikia malolosololoso tu kwenye vyombo vya habari; kwa nini msiitangaze Kigoma?

Tulikuwa tunakijua Kijiji cha Nzihi, Iringa, kilichokuwa kijiji bora, wanalima vizuri kikiendeshwa na Mwenyekiti mwanamke. Tulikuwa tunajua Kwamsisi, tulikuwa tunajua Isansa Mbeya, tulikuwa tunajua vijiji vyote hivi kwa sababu vyombo vya habari vilitusaidia kuelekeza mawazo ya Watanzania katika kilimo kilicho bora. Kwa hiyo, tulikuwa tukisikia kazi zinazofanywa zaidi ya maneno mengine mengine, ambayo sasa tunayasikia na kila mtu alipokuwa anasikia haya alikuwa anajaribu kujitahidi kufanya kilimo bora. Mimi ningeshauri, Ofisi ya Waziri Mkuu itafute tena mkakati wa kueneza habari, kama vyombo vilivyopo havina pesa za kutosha hebu unda vyombo ambavyo vitafikisha habari kwa wananchi wetu ili waweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa katika Kilimo Kwanza tuseme Wanawake Kwanza. Kilimo cha nchi hii, tusipokubali kwamba wanaolima na wanaoshiriki kwa nguvu zao zote ni wanawake, tukahakikisha wanafikiwa na rasilimali zilizotengwa katika bajeti hii, tukakubali kupunguza muda wao wa kazi nyingine kama kuchota maji na kufanya shughuli nyingine, kuwasogezea maji karibu ili waweze kushiriki vizuri, itakuwa ni wimbo kama tulivyoimba siku zote. Kwa hiyo, nasema Kilimo Kwanza na Wanawake Kwanza. Natoa pia pendekezo, kama Waziri Mkuu akikubali kwamba, ajitahidi ikiwezekana ahakikishe watoto wetu wale waliomaliza Kidato cha Nne, kama tulivyofanya Elimu ya Watu Wazima, hivi kweli kupanda kwa msitari unahitaji mtu aliyemaliza Chuo Kikuu, kwa nini hawa wasipewe kozi fupifupi katika vijiji wakaweza kuelekeza watu kwa karibu zaidi? Ningependa pia niseme, sikuona mkazo wa mbegu katika suala hili. Sisi katika Wilaya ya Ukerewe, tumeathirika kulima; tumelima mihogo inaoza na wengine walishaathirika katika maeneo ya migomba, wanalima mihogo inaathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, amani katika nchi hii; kwa kukaa kwangu katika Bunge la Afrika nimejifunza mambo mengi. Msione Burundi, Rwanda, Liberia, DRC, Somalia, chokochoko kubwa wamekuwa wakitumia vyombo vya habari kuvuruga akili za wananchi, chuki inapandikizwa, ikishapandikizwa watoto wadogo na watu wazima, wanaimeza ile chuki wanauana. Tafadhali sana, nawasihi Waandishi wa Habari, nchi hii wazee wetu akina Malecela na wengine, wameihangaikia mno na sisi tumeihangaikia tangu vijana. Msihongwe mkatumia fedha za hongo watu wakamwaga damu, kwa sababu ya kupandikiza chuki. Aliye na chuki aje ayazungumze humu ndani ya Bunge, lakini sio kupandikiza watu ambao wanavuruga nchi hii na kumaliza amani. Sisi Watanzania leo hapa kukitokea vurugu kwa sababu watu wamejaa chuki na jazba, tutakuwa wageni wa nani? Utakwenda Kenya, Uganda, Mozambique au utakwenda wapi, hatukuzoea?

Tafadhalini sana, vyombo vya habari saidieni kujenga nchi, kuelekeza nguvu katika Kilimo Kwanza, kuelekeza nguvu katika elimu na mambo mengine au sivyo

tutajikuta katika hali ngumu kabisa ambayo wenzetu wameipitia. Wengine walianzisha viredio vidogo tu Rwanda, vilivyomaliza watu 3,000,000 kwa siku mbili tu. Kilikuwa ni kiredio tu kinapandikiza chuki na watu wakachukiana bila sababu. Tunaomba tujitazame upya, kila mmoja wetu aweke nguvu katika kujenga maadili ya nchi hii, katika kujenga utu wa nchi hii na kuheshimu watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niwashukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Celina Kombani na Makatibu Wakuu na wote walioshiriki katika Taasisi mbalimbali katika Wizara hii. Nawashukuru sana na tuko pamoja na mpokee shukrani za Wananchi wa Jimbo langu, kwa kazi nzuri inayofanyika. Ahsanteni sana na naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie kwenye Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ambapo naanza kwa kuunga mkono hoja. Mambo ya msingi ni kama yafuatayo:-

La kwanza, naipongeza sana Serikali kwa kitendo kikubwa sana, ambacho kitadumu katika uhai wa dunia hii kwa Wananchi wa Shinyanga hususan Shinyanga Mjini, kwa vyovyote vile pamoja na Kahama, kwa mradi mkubwa wa maji wa kutoka Ziwa Victoria. Hata kama kuna upinzani wowote kutoka kwa mtu mwingine yeyote haitawezekana, kwa sababu Mwenyezi Mungu, alipoiumba dunia hii, maji yale aliyaweka Ziwa Victoria; kwa nini watu wa Shinyanga wasiyatumie hayo maji? Tanzania itaendelea kuyatumia na kufaidika na maji hayo. Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuja kuzindua huo mradi ili kuonesha kuwa, Watanzania hususan Serikali yake, inajali watu wake. Wananchi wa Shinyanga, watafaidika kwa namna mbalimbali na maji haya ya kutoka Ziwa Victoria, ambapo yanatoka saa 24. Ni miji michache sana au sehemu chache sana hapa Tanzania, ambazo zinapata maji ya kutosha kwa muda wa saa 24. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, niishukuru sana Serikali, pamoja na Wananchi wa Jimbo langu la Shinyanga na Mkoa wa Shinyanga katika suala la ujenzi wa shule za sekondari. Kwa miaka 44 ya uhuru mpaka mwaka 2005, Mkoa wa Shinyanga ulikuwa ni kati ya mikoa mitano ya mwisho yenye idadi ndogo ya shule za sekondari zilizokuwa za Serikali 55 tu. Serikali kwa kushirikiana na Wananchi wa Mkoa wa Shinyanga, wamefanya kazi kubwa; wamejenga kwa miaka mitatu shule mpya 200 na sasa ni mkoa wa kwanza kwa kuwa na shule nyingi za Serikali za Sekondari. *(Makofi)*

Nimpongeze sana Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Mheshimiwa Brigadia Jenerali Johannes Balele, kwa sababu ndiye aliyeongoza mapambano haya ya kushughulikia suala la elimu hususan elimu ya sekondari kwa Mkoa wa Shinyanga. Mkuu wa Mkoa huyu, atabaki katika historia hata pale atakapostaafu katika nafasi yake hiyo, kwa kufanya kazi kubwa sana ya kuongoza Mkoa wa Shinyanga, akizingatia aliyotumwa na Mheshimiwa

Rais kwamba, kasimamie pamoja na mambo mengine; kwanza, elimu Shinyanga ameifanya hiyo kazi, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, katika pongezi ni ujenzi wa barabara za lami mjini. Tumeandaa mpango wetu wa ujenzi wa barabara tukauwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu. Naamini wanautumia huu wanapotugawia fedha, ingawa hawajatugawia fedha nyingi, lakini *Inshallah* naamini siku moja watatugawia na nadhani katika bajeti hii, wametugawia nyingi kidogo kuliko huko nyuma ili Mji wa Shinyanga uwe na barabara bora na za lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi za Mheshimiwa Rais. Alama kuu katika Taifa lolote lile na hususan Tanzania, kwanza ni Rais wa nchi ile na sisi kwa Awamu ya Nne ni Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais, anapokuwa anaongea lazima kila anachokiongea kichukuliwe kwa uzito unaostahili. Kwa hiyo, akiahidi wananchi wake ni lazima iendane na kuingiza kwenye mipango ya kazi za Serikali, kuwatumikia wananchi wake. Zifuatazo zilikuwa ni ahadi za Mheshimiwa Rais, ambazo amezirudia hata juzi wakati anazindua Mradi wa Maji pale Mjini Shinyanga na ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga.

Katika uhai wa Taifa hili, Mkoa wa Shinyanga hauna Hospitali ya Mkoa na mwaka jana Serikali ilikiri hili. Pale panapotumika kama Hospitali ya Mkoa, ilikuwa Kambi ya Manamba (*Labour Camp*), ambapo kwa sasa haizidi ekari mbili tu. Kwa vyovyote vile, hata ukiamua kuipanua na kufanya ukarabati wowote ule, haitawezekana kufikia kiwango cha kusema hii ni Hospitali ya Mkoa, lakini kimipango mtu akiangalia anaweza akashangaa sana, kwa sababu kwa mujibu wa takwimu za hii Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Mkoa wa Shinyanga ni wa kwanza kwa kuwa na idadi kubwa ya watu imeandikwa hapa; sio mimi. Watu 3,400,000 wapo ukifuatia na Mwanza, Dar es Salaam, Mbeya, Kagera na Tabora.

Kwa hiyo, katika mipango huwezi ukawa unaukwepa Mkoa wa Shinyanga, kuujengea Hospitali inayostahili ya Mkoa. Hebu jaribu kuangalia, moja ya matatizo yaliyoko Mkoa wa Shinyanga ni wananchi wengi kwenda kwa waganga wa kienyeji. Sababu zake ziko mbili tu; moja elimu. Kama wakiwa na elimu ndogo, lazima utatarajia hayo wayafanye. Pili, wakiwa na huduma hafifu na hazitoshi wakimbilie wapi, lazima waende kwa waganga wa kienyeji. Ndiyo maana nasema, Mheshimiwa Rais, tulipomweleza ndio nimesimama kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Shinyanga Mjini na katika hili nilikuwa nawakilisha Wananchi wa Mkoa wa Shinyanga; nikamwambia pale pale kweli Mheshimiwa Rais alisema Serikali itajenga Hospitali ya Mkoa. Bahati nzuri katika jimbo langu, ndiko lazima ijengwe pale, kwa sababu ni Makao Makuu ya Mkoa na tumetenga ekari 100 kwa ajili ya ujenzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika bajeti ya mwaka kesho, tutatarajia kuona Mkoa wa Shinyanga unatengewa fedha za ujenzi wa Hospitali ya Mkoa ili tunaposherehekea Miaka 50 ya Uhuru wetu na Shinyanga iwe katika mikoa ambayo ina Hospitali ya Mkoa inayostahili kuwahudumia watu wengi kuliko mikoa mingine yoyote hapa Tanzania. Mkoa wa Shinyanga kama mnavyoufahamu, asilimia 65 ya pamba

inatoka kule.  Madini mengi yako kule, mifugo mingi iko kule, idadi kubwa hii ya rasilimali watu ni nguvu kazi, lazima ipelekewe huduma ya afya ili rasilimali watu hii iweze kutumika katika kuchangia kujenga uchumi mkubwa wa Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi ya pili ya Mheshimiwa Rais, ilikuwa ni soko la kisasa pale Mjini.  Amekuwa akielezwa mara kwa mara akienda Shinyanga na juzi alipokuwa kule tulimweleza akasema Serikali itajenga.  Hapa ndipo mahali pake pa kusemea; kwa hiyo, nitatarajia katika bajeti ijayo au kwa kutumia utaratibu mwingine ule mimi naufahamu na Serikali inaufahamu, tuwe na soko la kisasa.  Kuna madaraja mawili pale Mjini ya Ngokoro na Ndala.  Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), anayafahamu na alishakubali, sasa bahati nzuri ile ajenda imepanda juu zaidi ya yeye imekwenda kwa Mheshimiwa Rais, kwa hiyo, mambo yatakuwa barabara ili iharakishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi za Wakuu wa Wilaya, moja kati ya Wilaya ambazo hazina Ofisi stahili za Wakuu wa Wilaya ni pamoja na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Shinyanga.  Mimi nazifahamu Ofisi nyingi tu za kisasa, zinazojengwa sasa na zilizokwishajengwa, lakini Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, haina hadhi kwa hali ya sasa na miaka ijayo kuendelea kuwa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya; naomba ishughulikiwe hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la umeme kwa sababu sijapata fursa ya kuzungumza, nizungumze kwa kifupi sana.  Mimi kule nyumbani, ninaweza nikakaa kwangu mjini au kijijini ambako ndiko asili yangu kule Kizumbi, kwa sasa nakaa Kizumbi, lakini pamoja na kuomba umeme hadi leo hii sijaupata.  Kwa hiyo, huwa nikienda nyumbani sikai mjini kule kwenye umeme, nakaa huku na wananchi wangu ambao tunalia tukiulilia umeme.  Baada ya kuzungumza safari hii, naamini umeme sasa utakuja kwenye maeneo ya Jimbo la Shinyanga Mjini, ambayo hayana umeme ikiwa ni pamoja na Geregani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ukiwasikiliza baadhi ya watu wanadhani kuwa mifugo ni kitu kisicho na maana yoyote.  Mifugo ni pesa, ni zao lenye thamani kubwa na mifugo haiharibu mazingira isipokuwa pale mtu anapoamua kubana sehemu inakuwa lile eneo halitoshi kulishia mifugo yake, ndiyo uharibifu unaweza ukatokea na mara nyingi watu wanaowabana wafugaji ni wakulima.  Mfugaji anatangulia sehemu Fulani, halafu baadaye wanakuja wakulima wanaanza kumbanabana, lakini hiyo si hoja yangu; mifugo ni zao kama ilivyo pamba, kinachotakiwa tuweke utaratibu, tuingize mifugo hii katika mfumo rasmi wa uchumi ili tuweze kuvuna kama tunavyovuna mazao mengine.

Kwa hiyo, watabadili mawazo yao watakapoona kumbe ng’ombe, mbuzi, kondoo au kuku ni pesa.  Lazima kuwe na mifumo itakayowezesha kuivuna hiyo na mifumo hii mwisho wake kule ni lazima kuwe na viwanda na machinjio kubwa na za kisasa. Ndiyo maana nimekuwa nikipigania sana kusaidia kwa namna yoyote ile uwekezaji wa kiwanda cha nyama cha Shinyanga ili hatimaye aweze kufaulu kwa sababu ndiye atakuwa mkombozi wa wafugaji wa Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba nikushukuru sana kwa kuunga mkono tena hoja hii na kwa kunipa fursa ya kuongea. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kupata fursa hii adhimu kwa jioni ya leo ili nami niwe mchangiaji katika hotuba nzuri ya Bajeti ya Waziri Mkuu ya Mwaka 2009/2010. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kazi anayoifanya na nimshukuru sana kwa usimamizi wa shughuli zote zinazohusiana na masuala ya maendeleo hususan kwa nchi yetu kwa ujumla. Pia nichukue fursa hii, kuwashukuru Mawaziri walio chini yake akiwemo Mheshimiwa Marmo, Mheshimiwa Celina Kombani na Naibu Mheshimiwa Aggrey Mwanri.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi sana na shukrani za dhati kwa Serikali ya Awamu ya Nne, chini ya Rais Jakaya Mrisho Kikwete, hasa kwa kipindi hiki cha mwaka 2005 – 2010, kutuletea Mkuu wa Mkoa, Mheshimiwa Parseko Ole Kone, ambaye ni mchapa kazi kweli kweli. Natumia fursa hii, kutoa pongezi kwake kwa sababu nataka niwaambie katika nafasi ya miaka hii ninayoitaja, moja ya hatua kubwa ambayo tumeifanya sisi kwa Mkoa wa Singida ni ile ya kuweza kuwa na uwezo wa kujitegemea sisi wenyewe, hasa kwa mazao ya chakula. Huu ni uwezo ambao sasa Singida tunao na hii imetokana na uwezo wake yeye Mheshimiwa Kone na Watendaji waliopo chini yake katika Mkoa wa Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia nimpongeze DC wangu, Grace Masaki, pamoja na Mkurugenzi wa Maendeleo wa Wilaya ya Iramba, Kijana Fwema, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya na sasa Iramba inaonekana kioo na maendeleo yanakwenda kwa kasi sana. Pamoja na pongezi hizo, katika kila penye mazuri basi lazima na mbaya yapo. Nimeeleza vizuri sana juu ya utendaji kazi zote nzuri kuanzia Ofisi ya Waziri Mkuu mpaka kufikia ngazi ya Wilaya yangu. Ninachotaka kusema, nitawarejesha kidogo tu kwenye Katiba ya nchi na nataka nizungumzie hasa nafasi ya Waziri Mkuu kwa mamlaka aliyonayo kiutendaji ili nije nifananishe na kuoanisha na baadhi ya Mawaziri jinsi wanavyotenda kazi hizi na hili ni lazima tuseme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, panapokuwa na mazuri tutasema na mabaya lazima tuseme ili watu waweze kujikosoa na wajirekebishe, tusiposema hapa tukizungumza pembeni tutakuwa hatutengenezi. Kwa ridhaa yako, naomba uniruhusu niisome ibara ya 52 ya Katiba ya Nchi inasema kwamba: " Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa na madaraka juu ya udhibiti, usimamizi na utekelezaji wa siku hadi hadi wa kazi na shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania." Ukienda ibara ya 53 atawajibika kwa Rais kuhusu utekelezaji wake wa kazi ambazo Rais ameziagiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wabunge ni wawakilishi wa wananchi na tunapokwenda kwa Mawaziri kuwaeleza matatizo, hatuendi kuwaeleza matatizo ya nyumbani kwetu; tunakwenda kueleza matatizo ya wananchi kama Rais anavyowaongoza wananchi. Leo tutawapongeza baadhi ya Mawaziri, lakini tupo watu tuna manung'uniko

na baadhi ya Mawaziri. Utaratibu aliotupa Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mzuri, hatutasita na tutakunong'oneza Mheshimiwa Waziri Mkuu ili ujue ni Mawaziri gani ambao wanataka kutuharibia utendaji wa kazi.

Upo utaratibu wa kuweza kufanya kazi kwa namna ya kuheshimiana kiukanda, uko utaratibu wa kuheshimiana kirafiki, uko utaratibu wa kuheshimiana kwa namna ya mtu anavyoonekana. Wabunge wote ni sawa na Wabunge wanawawakilisha wananchi. Ninapokuja kwako kukueleza matatizo, sijaja kukueleza matatizo ya nyumbani kwangu, nakueleza matatizo ya wananchi na ili iwe faida kwa taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inashangaza, unafika kwa Waziri anakwambia mimi nina watu 40,000,000, wote wananiangalia. Wewe ndiyo umeteuliwa kuwa Waziri wetu na ndiyo tunakutegemea unasema una watu 40,000,000 huwezi kuwahudumia; kama huwezi kazi nenda nyumbani kwako kafanye kazi na wanao, tuachie ofisi ili wafanye watu wengine wenye uwezo. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu mimi nakufahamu na uadilifu wako na bahati wamezangumza Wabunge waliopita kuwa una hofu ya Mwenyezi Mungu na hilo kweli mimi naamini; simamia watu wa namna hii wasikuangushe. Kuwa macho kabisa, sisi ni Wana-CCM na tunazungumza kwa mema na hatuna tatizo wala kinyongo na hatuwezi kuwa Mawaziri wote. Hatuwezi tukaenda *front bench* wote. Watakuwepo *back bencher* na sisi ndiyo tutakaozungumza na kukosoa utaratibu na utekelezaji wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, rasilimali za nchi zinakwenda kwa mgawanyo sawa sawa kabisa wala hakuna tatizo. Ndiyo maana tunafurahia sana yale yanayotendeka kule ni kutokana na mgawanyo wa rasilimali, lakini tatizo lililopo ni nani anakwenda kusimamia kule? Mawaziri hawa wako radhi wasafiri mara nne kwenda nje lakini ukiwaambia twende Iramba, watakuuliza barabara yako iko salama, hivi kule Iramba hoteli zenu zikoje? Sasa huu si utekelezaji wa shughuli za kimaendeleo. Tunaomba mziache ofisi mtembee kama Mkuu wetu wa Mkoa. Mimi lazima nirudie kumsifia sana Mheshimiwa Kone, kwa sababu anatembea na ukienda Ofisini huwezi kumkuta anakuwa vijijini. Sasa ninyi acheni ofisi, tembeeni mfike kwenye Wilayani, mfike kwenye Kata na vijiji ili mkasimamie hizi fedha ambazo tunapitisha hapa. Hatuwezi kupitisha pesa lakini usimamizi hakuna, ndiyo maana unaona watu wanapata mwanya wanafanya watakalo pesa zinaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uko usemi mmoja unasema kwamba, mbwa anamheshimu sana anayempa chakula, lakini yule anayetafuta chakula hamheshimu. Sasa mimi naamini, kwa sababu wale watu mko juu yao, wanaweza kuwasikiliza sana kuliko sisi. Sisi tutapiga kelele watasema hawa Wabunge tumewazoea kazi yao ndiyo hiyo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, katika kutekeleza haya ambayo tunapitisha, tuhakikishe kwamba, usimamizi wake unakuwa mzuri ili kuondoa manung'uniko yaliyopo miongoni mwa watu. Nizungumze suala hilo hilo linalohusiana na usimamizi hasa wa miradi inayohusiana na kilimo. Nimeshazungumza mara kadhaa ndani ya Bunge hili Tukufu, nilizungumza mwaka 2006, nikazungumza mwaka

2007/2008 na mwaka huu narudia. Nimesema kwa nafasi ndogo ya sisi baada ya kupata ubunifu na kuwa na mpango kazi mzuri uliosimamiwa na Mkuu wetu wa Mkoa wa Singida, tumeweza kujitosheleza, wananchi kwa kutumia elimu ile wanayopewa na viongozi wao, wameweza kufanya vizuri baadhi ya miradi.

Mimi nawaomba sana kwamba, nguvu ya uwezo wa kuwajengea uwezo watu wa Mkoa wa Singida hasa kilimo cha umwagiliaji itiliwe mkazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha umwagiliaji kitiliwe mkazo kwa sababu tutakapofanya tukawa na kilimo endelevu kwa Mkoa wa Singida, ardhi yetu ina rutuba na ardhi yetu inavumilia na wala haihitaji mbolea. Wenzetu wa Kusini wanazungumza mbolea ya Minjingu, sijui mbolea ya wapi, sisi hatuhitaji mbolea. Mbolea yetu sisi ni samadi na samadi ukipata basi tunapata mazao mengi kweli. Kwa hiyo, naomba sana katika mpango wa mwaka huu, hasa suala la tunapoingia kwenye Kilimo Kwanza, tutilie mkazo sekta ya ukulima wa umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kero zinazotusumbua hivi sasa. Kwa kumalizia kabisa, kuelekea hii Awamu ya Nne na hiki kipindi cha mwaka 2009, kero kubwa ambayo ipo Vijijini pamoja na kwenye Kata ni juu ya Watendaji wa Vijiji na Watendaji wa Kata. Hawa imekuwa ni kero sana kwa wananchi; hawasikii na ni watu ambao wanafanya maamuzi yao. Wako Watendaji wanafikia hatua ya kuchapa wananchi. Sasa Watendaji wa namna hii, naomba msiwavumilie na ninaomba kupitia Ofisi yako, Mheshimiwa Waziri Mkuu, hawa watu wasivumiliwe.

Kero ya pili ni maji, ambayo ni kero mama. Tumeanza kuzungumzia Miradi ya Benki ya Dunia toka mwaka 2006 na huu ni mwaka wa nne na tutakwenda mwaka wa tano, ile miradi ya awamu ya kwanza haijakamilika. Ninaomba Serikali tuhakikishe ile miradi ya awamu ya kwanza inakamilika ili twende kwenye miradi ya awamu ya pili. Tukienda miradi ya awamu ya pili, angalau kila Wilaya ikawa na miradi kumi kumi na maji yakatoka, tunakuwa na jambo la kusemea na ile asilimia 65 tutakuwa tumeifikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kero nyingine ya mwisho ambayo niimalizie ni suala la barabara kati ya Dar es Salaam mpaka Mwanza. Naelewa Serikali kwa kiwango kikubwa, nashukuru barabara ya kati mpaka Mwanza japo mmeikamilisha kwa nusu kiwango, lile eneo lililobakia la Manyoni – Isuna, naomba Serikali iweke nguvu zake zote ili tuondokane na ile aibu. Km 60 hizi tuzimalizie jamani ili watu wa Mikoa ya Kati na hawa watu wa kupita katikati waweze kupita bila tatizo na ili tuoneshe kwamba, nchi yetu sasa kweli tunaunganisha kwa kupanda taxi kutoka Mtwara mpaka Mwanza.

Ninachotaka kukisema juu ya barabara, nawashukuru sana Serikali, mmeweza kui-*upgrade* barabara yetu ya Kiomboi – Kisiriri – Kidaru na baadae unakwenda Ibaga mpaka Kidarafa kuwa Barabara ya Mkoa. Katika mpango sijaona mwaka huu itakuwaje hii barabara. Uchumi umefunguka kwa kiwango, kadiri inavyoonekana barabara ile ikitengenezwa itaweza kutuunganisha kiuchumi na itatuunganisha na Wilaya ya Mbulu, Mkoa wa Manyara. Kwa hiyo, tutakuwa na uwezo wa kufanya kazi kwa muda wote, kwa

sababu wananchi wa eneo lile ni wakulima wazuri sana na ninaamini uchumi utafunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniita niweze kuchangia hoja hii ya Waziri Mkuu. Kobe huwa anaweza kufanya mapinduzi, pale tu anapothubutu kutoa shingo yake nje ya gamba lake na kwa kufanya hivyo huwa ana-*risk,* kwa sababu shingo ni nyembamba, kwa hiyo, anaweza akapoteza shingo kwa sababu ya ulaini wake; lakini hawezi kutembea bila kuthubutu kutoa shingo nje ya gamba lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu Hotuba ya Waziri Mkuu, inafanana na Hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi; wote wanasema Kilimo Kwanza. Bahati nzuri, tumekuwa naye mahali pengi na anachosema ndicho hicho. Wakati fulani Mheshimiwa Benjamin Mkapa akiwa Rais alisema hivi: "Mtaji wa maskini ni nguvu yake mwenyewe." Basi nilidhani kwamba, mtaji wa Kiongozi bora ni tabia yake, vitendo vyake na kauli zake. Kwa Lugha ya Kiingereza *decency is power* katika *leadership. If you are dirty, corrupt,* huwezi kuwa na nguvu katika kuongoza watu na nadhani ndiyo nguvu tunayoisema kwa Mheshimiwa Pinda. *(Makofi)*

*Decent* ni nguvu inayomsaidia kuheshimika na kusikilizwa. Watu wanatujua na tusidhani kwamba tumejificha. Sasa kabla sijasema mengi, napenda nimpongeze kwa hotuba yake nzuri na ya kina, pamoja na wasaidizi wake ambao wamechangia kufanya hiki kitu kizuri. Nadhani tusiishie hapa, hatua ya pili ni kusimamia utekelezaji wa hotuba yake hii nzuri. Sasa nauliza hapa, maana na yeye anasema Kilimo Kwanza. Leo asubuhi nilikwenda kukaa naye pale ni kama tulikutana na Mzee Malecela, maana mengine tumesema yale yale. Sasa mimi nauliza; Kilimo Kwanza ni pamoja Ng'ombe Kwanza, au Ufugaji Kwanza au vipi? Nadhani ndivyo hivyo; lakini ni lazima tuwe wakweli, tusiposema ukweli au kusubiri watu wafe ndipo tuje tuseme ukweli, nchi hii itaangamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nikiwa Njombe, nimekuta magari 40 yameongozana yamebeba mahindi kupeleka Arusha kwa sababu ya njaa. Mimi sina sababu ya ubishi kati ya umuhimu wa ng'ombe na maziwa na nafaka, ubishi huu hauna sababu. Sayansi inasema; kadiri mnavyozidi kuongezeka, eneo dogo la ardhi lazima mlitumie kuzalisha kile ambacho mtalisha watu wengi zaidi. Ningefurahi kama ningeona magari yale yamejaza ng'ombe kupeleka Arusha kwa ajili ya kuokoa njaa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosema hapa ni kwamba, kwato za ng'ombe zinaua ardhi na ardhi inazidi kuchakaa na nchi hii inaweza ikawa *net produce* ya chakula katika Afrika ya Mashariki, kwa sababu ina mabonde kama ya Rukwa, Pangani, Kilombero, Ruaha, Ruvuma, Rufiji, Lwiche na Malagarasi. Yote haya ndiyo maghala ya chakula katika dunia ambayo ardhi inazidi kwisha. Najua sababu za kisiasa na uoga, kwa sababu hizo, sasa tunasema mambo haya ya Kilimo Kwanza mimi nauliza mashamba ya ng'ombe yatakuwa wapi? Mashamba ya nafaka yatakuwa wapi na yako wapi? Kilosa

kwa miaka zaidi ya kumi wamekuwa wakipigana, mara mfukuze DC mara nani, mpaka hivi sasa hakuna amani ng'ombe wako wapi na mpaka wake ni upi haijulikani.

Ng'ombe wanatembea kama wakati wa Warumi *Taxi Romana,* yaani *peace within the Roman Empire.* Utatembea kokote kule ilimradi unatembea tu kwa sababu ni nchi yako basi unaruhusiwa kwenda na kurudi popote kule na anasema ni sawasawa acha wananchi wenyewe waongee. Waongee nini? Huwaambii kuwa hivi sasa tuna ng'ombe zaidi ya milioni 18; hivi wako wapi hawa ng'ombe? Utasema wako shamba gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mahindi tunajua yako wapi. Kwa hiyo, hapa unasema kwamba ukiwaudhi wafugaji utakosa kura, kwa hiyo, endeleeni kufuga; hivi vijiji vingapi vimegawanywa? Mashamba yako wapi hawa watu wanahangaika tu ni kama wameachwa kwa miaka tangu tupate uhuru. Mimi silaumu nasema hawana mahali wanatembea tembea, mara Njombe mala wapi; utawezaje kuwa na ng'ombe elfu 10 leo karne ya 21 halafu ufuge? Huku si kufuga ni kuchunga na utachungaje wakati ardhi haiongezeki watu wanaongezeka. Kwa hiyo, nadhani tumefikia wakati wa kusema ukweli hata kama haupendezi. Hali hii haiwezekani ni lazima Serikali ikae, iunde Kamati, tupange na mashamba yajulikane. Mashamba ya ng'ombe yanakuwa kwenye *semi-arid areas.* Sio kwamba, Mungu hakujua, ndiyo maana ng'ombe wanastawi eneo lile la Mwanza, Shinyanga, Tabora na Dodoma, maeneo ya ng'ombe sio kule kusini. *(Makofi)*

Kule ukipitisha ng'ombe elfu kumi kwa mara moja, wakipita tu wameua nyasi zote na ardhi ile imekwisha. Sasa unasema peleka na kule tena. Mimi nashangaa, hawa watu wa namna gani? Wamesoma lakini hawakusoma, wapelekwe ng'ombe Lindi na Mtwara yote, watembee kule kwenye korosho na tushukuru Mungu kwamba kule kuna korosho. Wakipita hivi nyasi za shida hazitaota milele, sasa unasema wakapite huko. Mna-*create* Jangwa la Sahara, mnataka Tanzania kuwa Sahara ya pili, kwa vitendo vyetu hivi. Tunajua mambo mbaya, lakini kama kawaida yetu tunadhani muujiza utakuja kutoa jawabu. Nadhani hili ni eneo moja ambalo ningeshauri tulifanyie kazi, yako wapi mashamba ya ng'ombe, hakuna. Mashamba ya mpunga yapo, ya mahindi yapo haya mengine ya ng'ombe yako wapi? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala ambalo nadhani ni vizuri niliseme hapa ni haya mabonde yawe maghala ya chakula ya Tanzania. Maeneo haya tuyatunze yawe kwa ajili ya kuzalisha nafaka, ambazo ndizo tutalisha dunia na ndiyo itakuwa nguvu yetu. Tukipoteza mabonde haya tumekwisha. Sasa kama haya tunashindwa kuyatunza, unasema uchimbe mabwawa mengine tena wakati haya unayaua, sijui kama unafikiria; gharama hizo ziko wapi, Mungu amekujalia kuwa na Bonde la Rufuji na Mabonde ya Kilombero, Lwiche, lakini huyaoni unasema ufikirie mengine. Hii staili ya kuficha ukweli katika kujenga nchi haitusaidii.

Kingine ambacho ningedhani Mheshimiwa Waziri Mkuu, angetilia mkazo katika hotuba yake ni hivi vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kijiji maana yake nini kwa Tanzania hapa? Mradi watu wanakaa pamoja huko porini pasipo na umeme ndiyo kijiji au nini? Kuna wakati tuligawa kwa *population* ya watu tukaweka mipaka na utawala. Kwa hiyo, robo tatu ya vijiji ni vitovu vya utawala na huduma; sio viwanda mama au mahali pa kuzalishia mali.

Nadhani pendekezo kwamba tuunde Tume ya kuangalia vijiji vyetu ili viwe vya kuzalisha mali *is timely.* Vijiji hivi viliundwa mwaka 1973, mahali pengine sasa hivi ni mnyororo wa vijiji kama pingiri za kwenye mnyororo. Unatoka pale Makambako mpaka Njombe ni vijiji, unatoka Makambako mpaka Mbeya ni vijiji.

Sasa huu utawala wa namna hii hatuuoni? Halafu unasema kila mtu alipwe hata kwa sababu ya kukaa tu. Ukisema upime vijiji hivi awe na mipaka ili atatue tatizo, badala ya kusema hapana, tuli-*define* kijiji kwa kupanua *radius* halafu tuongeze utawala na aina ya watu, usafiri na maslahi ili kiwe kijiji cha kisasa badala ya kuendeleza kijiji cha watu 500 wakiongezeka tunagawana; kwa nini tusigawe kwa sababu tunataka maslahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tupunguze vituko katika kuendesha nchi, gharama ni kubwa mno; hivi leo kama mtu angepita na ndege juu wakati Mawaziri wote wanatembea na Waziri Mkuu naye anatembea wote wako barabarani; watoto wa shule, walimu wanakijiji, wote wanasubiri kupokea viongozi. Magari yote yako pale, Wabunge wote wako pale, wataalamu wote wako pale na nchi ni maskini lakini hatuoni. Wanasema watu wanawapenda, shule zote hawafundishi. Mimi ninapendekeza kwamba, hii ni nchi yetu, tusisubiri mpaka tufe ndipo tuseme. Kama kiongozi anafika Iringa hivi DC na watu wengine wa Ludewa na wote wale wanakuja kutafuta nini; wa Makete wanatafuta nini? Si wasubiri aende kwao? Baada ya kutembelea Mkoa wote wakati wa kutoa *summary* sasa ndipo waje pale Iringa, kwa sababu ameyasema mambo tofauti. Vinginevyo, hii *behavior* haifanani na umaskini wetu. *We are poor*, lakini tuna *behave* kama mamilionea kumbe hata mamilionea hawa-*behave* namna hiyo. Kwa hiyo, nilidhani nalo hili tulichukue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vikao, mikutano, semina; siku hizi kila ukimpigia simu Katibu Mkuu yupo kwenye kikao, wote wako kwenye vikao. Hata pale ambapo Sheria inamruhusu yeye aamue anaitisha kikao kwa sababu anataka uamuzi huu uonekane ni wa wengi ili asikamatwe yeye peke yake wakati madaraka yanamruhusu aamue. Kwa hiyo, *government is not moving.* Lazima Serikali itembee kwenye karatasi lakini isitembee haraka. Kama kila siku Katibu Mkuu yupo kwenye vikao, sasa hivi ni mabingwa wa vikao tu na kuvaa tai kusubiri chai. Hii *culture* inavyozidi kujengeka katika nchi yetu, nadhani tutaua nchi. Maboresho haya yametuua lakini yanaonekana mazuri, sasa mengine tutasema siku nyingine. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni Sera ya Kujitegemea. Tulikuwa na sera nzuri, sasa hivi Mwenyekiti bora wa kijiji ni yule anayejua kuomba na kutoa risala nzuri na kuongea vizuri na Mbunge na wageni. Kwa hiyo, lugha ya wahisani na wafadhili sasa ndiyo lugha inayotawala vijiji. Tutawezaje kuendesha nchi namna hiyo wakati sisi ni maskini na *vocabulary* inayotawala ni ya ombaomba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nimeliona hapa; huenda ni vizuri tuanze kufikiria uwezekano wa kupima haya tunayoamua na tunakokwenda. Mimi nashukuru, elimu tumefanya tuliyoyafanya lakini sijui, labda nitapewa nafasi ya kuongea wakati wa elimu.

Tusipoangalia, kama elimu haitatui matatizo ila inaongeza matatizo ni ya nini; si afadhali tungetumia fedha hii kulima maharage kuliko kuleta watu ambao ni problem katika nchi? *Psychologically,* Makwetta utakosaje kujenga shule ya sekondari wakati wenzako wanajenga na wanasema ni kitu kizuri. Shule sio majengo, si Walimu peke yao, wala si wanafunzi peke yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya mwisho niweze na mimi kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nampongeza yeye mwenyewe binafsi na wasaidizi wake; Mheshimiwa Celina Kombani, Mheshimiwa Aggrey Mwanri na Mheshimiwa Philip Marmo, nawapongeza sana kwa kazi nzuri wanayofanya katika kusukuma gurudumu la TAMISEMI na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mikoa ambayo inaitwa *The Big Four,* kwa upande wa kilimo na hasa katika uzalishaji wa chakula hapa nchini. Mikoa hiyo ni Ruvuma, Rukwa, Mbeya na Iringa. Vile vile kwa upande wa mifugo kuna *The Big Four*; kuna Mkoa wa Shinyanga, Mkoa wa Mwanza, Mkoa wa Mara na Mkoa wa Arusha. Kwa hiyo, kama ni Kilimo Kwanza, basi na Mifugo Kwanza! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natiwa faraja na jitihada za Serikali, kutenga maeneo ya wafugaji. Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake alituambia kwamba, katika kipindi cha mwaka 2006/2007 na 2008/2009, jumla ya hekta 1,391,109 zilitengwa katika Mikoa 13 na Wilaya 31. Nilitaka Mheshimiwa Waziri Mkuu, atueleze baadae atakapokuwa anahitimisha kwamba, je, Wilaya ya Ngorongoro iko katika hizi Wilaya 31 ambazo zimetengwa maeneo ya wafugaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimueleze Mheshimiwa Makwetta, namheshimu sana, lakini ni kwamba, maeneo ya wafugaji, Serikali imeyachukua kwa nia njema tu na kwa ajili ya majukumu mengine mbalimbali ya Serikali, imekuwa ikichukua na kutumia maeneo ya wafugaji kwa ajili ya mambo mbalimbali ya Kitaifa. Kwa mfano, Hifadhi za Taifa karibu zote na Mapori ya Akiba yametoka katika maeneo ya wafugaji. Pia mashamba makubwa ya kilimo kwa ajili ya chakula, yamechukuliwa toka maeneo ya wafugaji. Siyo hayo tu, lakini maeneo ya wawekezaji wa ndani na nje kupitia TIC, wamepewa maeneo ya wafugaji.

Anaposema mashamba yako wapi ya mifugo; kuna *ranch* kama Kongwa na nyingine chache. Kwa sababu ardhi ya wafugaji imekuwa finyu mno, ndio maana sasa maeneo ya kuchunga nayo yamekuwa ni finyu sana. Wakumbuke tu kwamba, pia

miundombinu ya mifugo imekuwa ni duni sana. Kwa mfano, maabara ya mifugo, majosho, malambo, masoko na minada ya mifugo, vituo vya utafiti, viwanda vya kusindika mazao ya mifugo, miundombinu hii yote ni duni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limetuathiri sana ni ukame ambao kwa mwaka mzima katika maeneo ambayo ni tambarare, maeneo ambayo mifugo inategemea, hakuna mvua. Nataka niiombe Serikali kwamba, hili ni janga na Serikali katika bajeti yake iangalie uwezekano wa kuchimba mabwawa katika maeneo yale, kuchimba visima vya maji ili kuondoa msongamano wa mifugo katika maeneo ambayo yamepata neema kidogo ya mvua. Kutokana na ukame huu, ndio maana mifugo ya Longido, sasa hivi iko Ngorongoro, mifugo ya Longido imekwenda Simanjiro, mifugo ya Longido iko Monduli. Siyo hiyo tu, pia mifugo ya Simanjiro kwa ndugu yangu Sendeka, imekwenda Kilindi kwa ndugu yetu Beatrice Shellukindo na amewapokea. Hii ni kwa sababu ya hali ya dharura, hili ni janga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata mifugo kutoka Ngorongoro sasa hivi mingine imeelekea Maswa *Game Reserve*, lakini ni maeneo ambayo yanahifadhiwa, hawawezi kuingia. Hata wanyamapori, wakizidiwa nao wanavuka mipaka yao wanakuja maeneo ya vijiji. Sasa kwa nini ninyi mnataka mtugombanishe na wanyamapori? Tunaheshimiana sana, wala hakuna tatizo lolote katika hilo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupunguza makali ya ukame, nashauri Serikali kujenga mabwawa kama nilivyosema na visima vya maji katika maeneo kame na katika Jimbo langu la uchaguzi ni maeneo ya Olbalbal, Piyaya, Bulati, Malambo, Masusu na Kakesyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namna nyingine ya kujaribu kusaidia hii miundombinu ni kufufua miundombinu ya maji iliyokuwa imeharibika. Kwa mfano, wakati wa ukoloni walitengeneza bomba la maji kule Mekeke katika Kijiji cha Enduleni, lakini pia kulikuwa na *Wind Mill* ya kuvuta maji kutoka ardhini kule Kakesyo na Njueta, lakini pia kulikuwa na Mradi wa Maji kutoka Oldonyo Sambu kwenda Masusu, huu ni mradi mkubwa ulianzishwa na Marehemu Sokoine, lakini basi kwa sababu zile DPs za kuchota maji katikati hazijawekewa, basi wananchi wakahujumu mradi ule. Naiomba Serikali iangalie maeneo kame ili iweze kuweka miundombinu ya maji na hivyo kunusuru hali ya mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Ngorongoro kwa mujibu wa taratibu za TANESCO, ilikuwa ipate umeme mwaka 2015, lakini nafarijika kwamba katika bajeti hii TANESCO imeomba jumla ya shilingi bilioni 312 kwa ajili ya kununua jenereta ya kuzalisha umeme katika maeneo ambayo hayana umeme wa Gridi ya Taifa. Maeneo hayo ni Makao Makuu ya Wilaya ya Ngorongoro, Loliondo, Kasulu, Kibondo na Sumbawanga.

TANESCO wanasema, kama Serikali itaidhinisha hizi fedha, basi hadi kufikia Juni, 2010, hii kazi ya kuweka majenereta haya ya kuzalisha umeme katika maeneo ambayo nimeyataja, itakuwa tayari.

Sasa nataka niiombe Serikali, niiombe Wizara iidhinishe hizi pesa ziende TANESCO na sisi tuweze kupata umeme. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumetekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2005 mpaka 2010 kwamba, Makao Makuu zote za Wilaya ziwe zimepata umeme ifikapo 2010. Kwa hiyo, tukiweza kupata hizi fedha, naiomba sana Serikali iidhinishe hizi fedha kwa TANESCO ili na sisi tuweze kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Mheshimiwa Rais alivyokwenda Loliondo tarehe 20 Machi, 2007, aliwaahidi Wananchi wa Loliondo kwamba, watapata umeme japo wa jenereta kwa kuanzia wakati taratibu zinaendelea kuandaliwa za kupata umme wa gridi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhamira ya Serikali kuunganisha nchi nzima na mtandao mzuri wa barabara zinazopitika wakati wote. Hapa ndipo namkumbuka Rais wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, alikuwa na dhamira hii ya kuunganisha mikoa yote kwa barabara kuanzia Kusini kwenda Kaskazini, Mashariki kwenda Magharibi na Jemedari wake aliyekuwa Waziri wa Miundombinu wakati ule Mheshimiwa Magufuli, kuna wakati alisema gari dogo litatoka Kaskazini kwenda Kusini kwa barabara ya lami. Hali ya kubadilisha badilisha Mawaziri, wanashindwa kutekeleza ahadi zao kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna njia mbili tu za kufika Makao Makuu ya Ngorongoro kule Loliondo; unaweza ukapita Geti la Ngorongoro ukaelekea Mbugani ukaenda huko. Njia ya pili unapita Mto wa Mbu, Kigongoni, Selela, Engaruka, Engaresero unakwenda mpaka Loliondo. Ilikuwa ni azma ya Serikali kujenga barabara kupitia kote huko ili kuweza kuunganisha uchumi wa Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Mara.

Nadhani azma hiyo ya Serikali bado ipo, ingawa kwa mwaka huu wa fedha, sijaona kama hiyo barabara imetengewa hela. Kabla ya tarehe 30 Juni, ni vizuri hela iliyokuwa imetengwa kwa ajili ya barabara ile ikatoka iweze kufanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kulikuwa na ahadi ya Rais ya kutengeneza barabara kutoka Armanie hadi Piyaya na hii ni kazi ya Halmashauri ya Wilaya na wameanza.

Vilevile Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro wanatengeneza barabara nyingine kuanzia Longoku kwenda Olbalbal - Njurata - Nasere-*rock* hadi Loliondo. Mheshimiwa Rais alisema kwamba, wananchi hawana sababu ya kupita mbugani, barabara tuzielekeze waliko wananchi ili waweze kunufaika nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Uchaguzi, nina tatizo kubwa sana la mawasiliano. Namshukuru sana Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari; alikuja Ngorongoro katika Kijiji cha Ngaresero na akasikia kilio cha wananchi, akaleta makampuni yote yanayohusika na mawasiliano, kwa mfano, tiGO, ZANTEL, TTCL, ZAIN na VODACOM. Alikuja nao

wote na baada ya kumaliza ziara yake, akawaandikia wote barua na nyingine akaandika kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa sababu kulikuwa na tatizo la *Environmental Impact Assessment* kwamba, ukitaka kuweka minara ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro ni lazima kufanya tahmini ya mazingira. Kwa hiyo, akamwandikia Mheshimiwa Maige, naye ali-*respond* kibali kimetoka. Naomba tuendelee kufuatilia tupate mawasiliano. Namshukuru sana kwa kazi nzuri aliyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sitaki kugongewa kengele, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa sababu tumeweza kupata wachangiaji 12 kwa jioni hii. Kwa hiyo, mtakuta kwamba, idadi kubwa ya Wabunge watakosa nafasi kwa sababu siku nzima itakuwa ya kesho na Siku ya Alhamisi labda itakuwa asubuhi, jioni itabidi Ofisi ya Waziri Mkuu iweze kutupatia majibu yetu. Kwa hiyo, mnakuta kwamba hiyo kazi itakuwa nzito.

Ninayo matangazo mawili, ambayo yametoka Ofisi ya Katibu wa Bunge; anaomba niwatangazie Wabunge wote kuwa, kesho Siku ya Jumatano, tarehe 24 Juni, 2009, kutakuwa na Onesho la Filamu iitwayo Crimson Wings, inayoonesha maisha ya ndege waitwao Laser Flamingo na utajiri wa bayoanuai na hazina nyingi za asili zilizoko katika Bonde la Ziwa Natron.

Filamu hiyo inaratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na itafanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa kuanzia saa 7.00 mchana. Mnakumbuka tumekuwa na mazungumzo mengi kuhusu Lake Natron na hawa Flamingo, nadhani itakuwa ni wakati mzuri kuweza kuona yale yanayoendelea hivi sasa. Kesho saa 7.00 mchana kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa.

Tangazo lingine nalo linatokana na Ofisi kwamba, Wabunge wote wanatangaziwa kuwa katika Viwanja vya Maonesho Bungeni yapo maonesho yanayohusu teknolojia mpya ya ujenzi wa nyumba kwa gharama nafuu.

Maonesho hayo yanafanywa na Lubana Construction Company Limited na kwamba, kampuni hii imewalenga ninyi Waheshimiwa Wabunge ili muweze kuifikisha teknolojia hiyo kwa Wakurugenzi wa Halmashauri wa Wilaya zenu na kwa faida ya Wananchi wa Majimbo yenu.

Aidha, Mheshimiwa Waziri Mkuu, amekwisha waelekeza Wakurugenzi wa Halmashauri zote Tanzania Bara, kuitumia teknolojia hiyo katika ujenzi wa nyumba kwa gharama nafuu. Maonesho hayo yatamalizika Siku ya Alhamisi tarehe 25 Juni, 2009. Kwa hiyo, mnakaribishwa kwenda kuona, kuuliza maswali na kujifunza zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, kesho baada ya kipindi cha maswali, wafuatao wajiandae: Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshmiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Elietta Switi na Mheshimiwa Zainab Vullu. *(Kicheko)*

Nina matatizo, nadhani wale walioamua kwenda kupanga orodha, walikuwa wanapanga Mikoa; wanatoka huku, wanatoka kule; nadhani ndicho kilichotokea. Kwa hiyo, niliowatangaza hao wajiandae ndio watakaoanza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo haya, naomba niwashukuru sana kwa ushirikiano mlionipa kwa siku ya leo. Niwatakie jioni njema na mapumziko mema mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 01.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano,*
*Tarehe 24 Juni, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*